*Nakala ya Mtandao (Online Document)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tatu - Tarehe 19 Machi, 2015**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alisoma Dua*

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu!

**MASWALI NA MAJIBU**

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, swali letu la kwanza ni ofisi ya Waziri Mkuu litaulizwa na Mheshimiwa Ritta Kabati.

Na. 31

**Hitaji la Gari la Wagonjwa Hospitali ya Wilaya ya Iringa**

**MHE. RITTA E. KABATI** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka gari la wagonjwa katika hospitali ya Wilaya ya Iringa?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ritta Enespher Kabati, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Hospitali Teule ya Wilaya ya Iringa (Tosamaganga) haina gari madhubuti la kuhudumia wagonjwa kutokana na uchakavu wa gari lililopo, hali inayosababisha gari hilo kuharibika mara kwa mara na kushindwa kutengenezeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuimarisha huduma za Rufaa katika hospitali hiyo Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imepanga kutumia shilingi milioni 150 kutokana na Bajeti ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri, kwa mwaka wa fedha wa 2015/2016 kwa ajili ya ununuzi wa gari la kubebea wagonjwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kukabiliana na kadhia hii ya utoaji wa huduma za rufaa kwa hospitali hii ya ngazi ya Wilaya, Halmashauri imekuwa ikitumia magari ya Vituo vya Afya vya Idodi, Isimani, Kimande, Kiponzelo, Nzii na Wapaaga ambavyo kwa sasa vituo hivi ndivyo vinavyohudumiwa na hospitali hii. Vituo hivyo vya Afya vina magari ya wagonjwa ambayo yanatumika kutoa huduma ya za rufaa katika ngazi za Wilaya, Mkoa na hadi ngazi ya Taifa pale inapohitajika.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi niulize maswali, ninayo maswali mawili tu madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake na kwa kweli naomba tu nimfagilie kwa kazi nzuri ambayo amekuwa akiifanya hasa katika Mkoa wetu wa Iringa.

Ninaomba kumwuliza kwamba ni vigezo gani hasa huwa vinatumika katika kutoa haya magari ya wagonjwa katika Wilaya zetu, kwa sababu Wilaya zetu zote za Mkoa mfano, Wilaya ya Kilolo, Wilaya ya Mufindi, Wilaya ya Iringa na hiyo ya Manispaa hakuna magari ya wagonjwa na hata hospitali yetu hiyo kubwa ya Mkoa magari yake ni chakavu sana.

Vilevile kumekuwa na matukio mbalimbali ya ajali ambayo yamekuwa yakitokea. Hata juzi ajali imeua watu hamsini (50), majanga ya moto na kuna Mlima pale Kitonga.

Swali la Pili nimwulize kwamba, kumekuwa na ongezeko kubwa sana kwenye Manispaa yetu ya Iringa katika Jimbo la Iringa Mjini. Lakini ile hospitali bila wewe isingefunguliwa. Ulikuja na ukaenda tukaifungua, lakini hakuna gari la wagonjwa na hospitali ile kuna wazazi ambao wamekuwa wakichukuliwa kwenye magari ambayo siyo *special* kwa ajili ya kuwapeleka kwenye hospitali ya Mkoa. Tayari walikuwa wameshaleta maombi maalum mara tano ya kupatiwa gari la wagonjwa.

Je, ni utaratibu gani sasa unatumika kushughulikia haya Maombi Maalum?

Aidha nikuombe kwa kweli kwa sababu kwenda Iringa hapo ni masaa mawili tu ikiwezekana tungeenda ukajionee wewe mwenyewe. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, jibu sahihi ni muende wote kipindi hiki hiki. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kwa niaba ya Serikali na kwa niaba ya ofisi ya Waziri Mkuu naomba kumshukuru sana katika mazingira ya leo Mbunge kusimama hapa na kufurahi na kusema kwamba kazi inayofanyika ni nzuri. Ni jambo ambalo linatia moyo na ninashukuru sana.

*Equally*, niseme pia kwa sababu amesema nilikwenda katika hii hospitali wanafahamu na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa wanafahamu nilifika pale. Jitihada kubwa sana Mbunge huyu amesimama imara sana katika kuhakikisha kwamba hospitali ile inafunguliwa. Kwa hiyo, mimi napenda nimpongeze kwa kazi nzuri anazofanya katika hospitali hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu vigezo ambavyo anavizungumzia Mheshimiwa Ritta najua kwamba ni kwanini anauliza swali hili. Swali linaulizwa kwa sababu kuna wakati fulani *UNDP* ilitusaidia kupata magari na kuna wakati fulani *United Nations High Commissioner for Refugees* naye aliwahi kusaidia. Baadaye sasa kwa vile hawa wote sasa hawatoi haya magari unaona swali kama hili linakuja hapa kwa sababu programu hizo hatunazo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunachofanya hapa ni kwamba hawa wote unaosikia kwamba wana magari ni kwamba wanai-*factor* katika Bajeti yao. Yaani wanaangalia katika *own source*, wanaangalia katika mipango yao kuna hela zile wakati ule wa *Local Government Capital Development Grant* wanaingiza mle ndani. Kwa hiyo, wanapeleka kule.

Lakini inapotokea kwamba kuna mahali ambapo tumepata magari haya tunaangalia sana maeneo yaliyopo pembezoni, wenzetu waliopo katika maeneo ya maziwa, waliopo katika maeneo ambayo kwa kweli unajua kabisa usipopeleka gari la wagonjwa kule au usipopeleka boti kule akina mama kule watakufa tu.

Kwa hiyo, ndivyo vitu tunavyoviangalia. Tunaangalia hali halisi iliyopo katika hospitali ile kama ilivyoelezwa hapa, tukiona kabisa hapa pana tatizo tutapoteza maisha ya mama na mtoto au na watu wengine na wananchi waliopo kule tunafanya hivyo, ndicho tunachokiangalia. Kwa sasa hivi tunachofanya ni hicho. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, amezungumza habari ya kitu kinachoitwa Maombi Maalum. Hawa Wabunge wenzangu wote mmesikia maelekezo ya Serikali ni kwamba Maombi Maalum hatuna huo utaratibu tena, kitu ambacho mtu anaweza akafanya ni kuandika andiko, andiko likatafutiwa *Development Partners* wakatusaidia katika jambo hilo. Lakini kwamba kuna maombi maalum, mimi nimekuwa nasoma kidogo wakati tunapokutana katika Kamati tumeona kitu cha namna hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili ongezeko la Manispaa katika hii hospitali ya Iringa kama alivyosema, ambacho tunaweza tukafanya hapa kwa sababu sasa hivi ndiyo tunaandaa Bajeti, tutahakikisha kwamba tunazungumza na wenzetu wa Iringa ili tuhakikishe kwamba hii wanaiingiza kwa sababu kweli pale pana *problem* kubwa, pale pana magari mengine Hyundai zimechoka choka hazifanyi kazi tutasaidia kuona kwamba wanaingiza katika Bajeti zao kwa sababu sasa hivi ndiyo shughuli inayofanyika. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Msigwa kwa kifupi.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninakushukuru. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri, mimi ndiye Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini na ninayajua mazingira ya Jimbo vizuri zaidi, niseme tu Mheshimiwa Waziri unapojibu maswali hunitendei haki, kwa sababu hospitali ile ya Iringa Mjini haikuanza kabla sijatoa vitanda na magodoro katika hospitali ile. Kwa hiyo, kumwagia sifa Mbunge wa Viti Maalum, kwamba yeye ndiyo amefanya juhudi kubwa si haki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu ni juhudi gani za makusudi baada ya Manispaa ya Iringa Mjini, kufanya juhudi kubwa kuijenga ile Hospitali na mimi kama Mbunge nilisaidia kuanzisha ile Hospitali ianze na juzi Waziri Mkuu alipokuja alinimwagia sifa na wewe ulizisikia, Serikali itatusaidiaje ili tupate hilo gari la wagonjwa tuendelee kufanya kazi vizuri?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, swali nililokuwa ninajibu hapa lilikuwa ni swali la Mheshimiwa Ritta Kabati, ndiye aliyeuliza swali. Mimi Mheshimiwa Msigwa hakuuliza au maswali haya hayakuulizwa *jointly*, kwa hiyo niwajibie wote.

Mimi ninachosema nilikuwa najibu kuhusu Mheshimiwa Ritta Kabati, kwa sababu ndiye swali lililoletwa hapa. Mimi nataka niseme kitu kimoja hapa na wala mimi sitaki kuingia katika *conflicts* hizi kwamba Mheshimiwa Msigwa amefanyakazi amepeleka vitanda pale niliona kwa macho yangu.

Lakini wananchi wanachohitaji hapa siyo kwamba ni nani ameleta hapa, tunahitaji *concertedefforts*, tunataka watu wote waliopo kule Mwenyekiti wa Halmashauri atusaidie, Mbunge wa Viti Maalum atusaidie, Mbunge mwenyewe wa Jimbo atusaidie, tunataka Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya watusaidie na tunataka sisi Wabunge wote tusaidiane hapa. Kwa

hiyo ni kweli kwamba pale wananchi wenyewe wamefanyakazi kubwa kwa kushirikiana na viongozi wao na hiyo ndiyo *credit* ambayo ninaileta kwako.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vile ameuliza mimi najua kwamba tulipokuja pale katika ile hospitali ilikuwepo na vitanda vililetwa pale, lakini *equally* ni kweli pia Mheshimiwa Ritta Kabati na yeye amechangia sana kama Mbunge wa Viti Maalum katika hilo eneo na wewe umechangia sana katika hilo eneo, wote mmechangia sasa ninafanya makosa gani?

**MWENYEKITI:** Ahsante sana, tunaendelea Waheshimwia Wabunge leo tuna miswada miwili na yote hiyo inatakiwa iishe. Kwa hiyo, muda wetu ni mdogo sana. Mheshimiwa Mkosamali.

Na. 32

**Changamoto Zilizojitokeza Kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa**

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI** aliuliza:-

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2014 umekuwa na changamoto nyingi sana:-

(a) Je, ni kesi ngapi zimefunguliwa Mahakamani kutokana na uchaguzi huo kwa nchi nzima na zitaisha lini ikiwa zipo kesi za mwaka 2009 zimeisha mwaka 2014?

(b) Je, ni kwa nini wananchi wa Kitongoji cha Nduta wamezuiwa kupiga kura?

(c) Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria ili Uchaguzi wa Serikali za Mitaa usimamiwe na Tume huru ya Uchaguzi?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Jenista nani anajibu hilo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Felix Francis Mkosamali, Mbunge wa Muhambwe, lenye sehemu (a), (b), na (c), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa za mwaka 2014 ilielekeza hatua stahiki za kuchukua kwa yeyote ambaye hakuridhika na matokeo ya Uchaguzi ikiwemo kufungua kesi mahakamani.

Aidha, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri Ya Muungano wa Tanzania kesi hii hushughulikiwa na muhimili mwingine wa dola kwa maana ya Mahakama. Hata hivyo, taarifa zilizopo ofisi ya Waziri Mkuu TAMISEMI zinaonesha kuwa zipo kesi 65 ambazo zimefunguliwa Mahakamani zinazohusiana na Uchaguzi huo. Kuhusu muda wa kwisha kwa kesi hizo Mahakama kupitia mpango wa maboresho wa Mahakama zimejielekeza kuwa kesi hizo zisichukue si zaidi ya mwaka mmoja kwisha, isipokuwa kwa zile ambazo mashauri yake yanahitaji uchunguzi wa muda mrefu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sifa ya mtu Kupiga Kura ni lazima awe mkazi wa eneo husika. Kilichojitokeza katika kitongoji cha Nduta ni baadhi ya wananchi kutaka

kupiga kura wakati siyo wakazi wa eneo hilo na hawakuwemo kwenye daftari la Mpiga Kura la Kitongoji hicho.

Wananchi hao walishauriwa kwenda Kupiga Kura katika maeneo wanayotoka na kimsingi hawakuridhishwa na maelekezo hayo na hivyo walifungua kesi Na. 4/2014 katika Mahakama ya Wilaya ya Kibondo wakilalamikia kitendo cha kuzuiwa Kupiga Kura. Kwa mantiki hiyo Serikali haiwezi kuendelea kujadili suala hili hadi hapo uamuzi wa mahakama kuhusu kesi hiyo utakapokuwa umetolewa.

(c) Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba inayopendekezwa, Ibara ya 210(1) inaeleza juu ya kuundwa kwa Tume Huru ya Uchaguzi ambayo moja ya majukumu yake itakuwa ni kusimamia chaguzi mbalimbali nchini.

Ningependa kumshauri Mheshimiwa Mbunge Felix Francis Mkosamali kuwa avute subira wakati mchakato wa Katiba hii inayopendekezwa ukiwa unaendelea. Uwezekano wa kuwasilishwa kwa Muswada wa Sheria utakaoelekeza Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na Tume Huru ya Uchaguzi utategemea matokeo ya kukamilika kwa mchakato wa Katiba Inayopendekezwa.

**MHE. FELIX F. MKOSAMALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ninashukuru. Nina maswali ya nyongeza mawili.

Moja; kesi za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa zilizofunguliwa mwaka 2009 baadhi ya kesi hizo zimekaa miaka mitano watu wapo Mahakamani, kwa nini Serikali isilete Kanuni ili wananchi wapate haki kama mtu ameshindwa ameibiwa kura, amenyang'anywa au amefanywa nini apate haki yake ndani ya muda, kuliko kesi kama zilivyokuwa mwaka 2009 zimekaa miaka mitano watu wakashindwa kupata haki yao. Kwa nini msilete Kanuni kesi hizi za Mbunge ziishe ndani ya mwaka mmoja, kama ilivyo kwenye kesi za Ubunge na Udiwani ambapo sheria za Uchaguzi zinaeleza kwamba kesi hizi zitaisha ndani ya miezi 18.

Swali la Pili; upo tayari kuwachukulia hatua watu waliokupa habari hizi za uwongo, kuwazuia zaidi ya watu 1500 Kupiga Kura na kutoa majibu ya uwongo, unaweza ukawachukulia hatua na nilikupigia simu siku ya Uchaguzi kwamba zaidi ya watu hawa wamevunjiwa haki za za kikatiba na wamekupa majibu ya uwongo. Unaweza kuchukua hatua kwa sababu Kibondo wanaendelea kuwanyanyasa watu hawa, wamefunga shule kwenye kijiji hiki na mambo mengine, wananchi hawapati huduma ya shule na mambo mengine. *(Makofi)*

Je, unaweza kuchukua hatua dhidi ya hii na wanakiuka mambo yaliyopo Mahakamani? *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri kwa kifupi sana.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba mnisikilize vizuri. Hivi ninavyozungumza hapa mimi ninatokea Kigoma. Hili jambo la Mheshimiwa Mkosamali, amenishirikisha sana na *for your information file* lote lile la Kigoma hili hapa.

Kesi zote hizi ninazozungumza hizi hapa. Kinachonifunga mimi hapa nisiseme maneno haya ni kwamba hili jambo lipo Mahakamani na utaratibu wetu ni wa *West Minister Model whereby we have Judiciary*, *Executive and the Legislature*. Hili jambo lisingekuwa limekwenda Mahakamani mimi ningejibu kila kitu kinachosemwa hapa kwa sababu ninayo majibu haya, lakini sasa nifanyeje utaratibu wa kuendesha nchi ndiyo huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme kwamba jambo hili ndilo, habari ya kuchukua hatua kwa watu ambao wamekiuka taratibu mlisikia tumetangaza hapa tumewasimamisha hapa karibu Wakurugenzi Watendaji Watano na sasa hivi tunaendelea kuchunguza na ninataka niwaambie kwamba wale wote ambao tunajua tukija kupata ukweli kwamba tumedanganywa au kuna mahali popote tumepotoshwa tutachukua hatua.

Kwa hiyo hakuna habari ya kwamba nimedanganywa hapa, mimi*I am on top of business* katika jambo hili. Ninaelewa na ninatokea kule Kigoma *it is unfortunate* kwamba hapa tunapoambiwa jambo hili lipo Mahakamani na kesi hiyo ninayo hapa imefunguliwa hapa, kila kitu, idadi ya watu waliokwenda kule nina kila kitu lakini sasa nimefungwa mikono.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea, kesi ipo Mahakamani. Wizara ya Katiba na Sheria Mheshimiwa Amina Abdulla Amour.

Na. 33

**Kushtaki na Kushtakiwa kwa Serikali**

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR** aliuliza:-

Kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali inaweza kushtaki au kushitakiwa:-

(a) Je, katika kipindi cha miaka mitano (5) iliyopita ni kesi ngapi za kushtaki na ngapi za kushtakiwa kwa Serikali zimefunguliwa?

(b) Je, ni kesi ngapi Serikali imeshinda na ngapi imeshindwa?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Amina Abdulla Amour, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha 2010 hadi 2014 jumla ya kesi 1,192 zilifunguliwa Mahakamani ambapo Serikali ni miongoni mwa wadaawa katika kesi hizi. Katika kesi hizo Serikali imefungua jumla ya kesi 13 kama Mshtaki yaani mdai na imeshitakiwa katika jumla ya kesi 1,179 kama Mdaawa.

(b) Katika kipindi cha mwaka 2010 - 2014 jumla ya kesi zilizosikilizwa na kwisha Mahakamani ni 591 ambapo Serikali imeshinda jumla ya kesi 511 na imeshindwa jumla ya kesi 80, kesi ambazo bado zinaendelea kusikilizwa Mahakani ni 601.

**MHE. AMINA ABDULLA AMOUR:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Kwa kuwa Serikali imeshtakiwa mara nyingi kuliko ilivyoshtaki.

Je, kwa nini Serikali haitimizi wajibu wake ikafikia kushtakiwa mara nyingi.

Swali la Pili. Kuna kesi 601 ambazo zinaendelea na za muda mrefu, kwa nini Serikali isizifanyie haraka hizo kesi zikamalizika kwa wakati ili haki itendeke.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni kwanini Serikali haitimizi wajibu wake ili kuepusha kushtakiwa. Kwanza naomba niseme msingi wa kupeleka au

kushtaki Serikali ni jambo la Kikatiba lipo chini ya Ibara ya 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Lakini pia ipo chini ya sheria inaitwa *Government Proceeding Act,* Sura ya 5 ya sheria za Tanzania. Kwa hiyo hilo ni suala la Kikatiba hatuwezi kuzuia watu wasije kushtaki mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini kitu ambacho tunajitahidi sasa kufanya kama unavyosema ili kuepusha Serikali isiwe inashitakiwa mara kwa mara, kwanza ni kujenga uwezo wa Kisheria kwa watumishi waliopo. Kwa sababu, kesi nyingi unakuta Mtendaji labda amevunja Kanuni amevunja Sheria. Kwa hiyo, tunawasisitiza Watendaji wa Serikali kuhakikisha maamuzi yao, matendo yao, yanafanyika kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu. Hilo ni suala ambalo tunalisisitiza sana kuhakikisha tunapunguza vitendo vya kushitakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini la pili pia, ambalo tumelifanya kama Serikali ni kuhakikisha kwamba, tunaimarisha vitengo vya Sheria katika Wizara, Taasisi na Wakala wa Serikali, kuhakikisha kwamba, Sheria zinafuatwa. Suala jingine ambalo tunalifanya kwa kiasi kikubwa ni kuhakikisha pia, sasa na wananchi na wenyewe wanajua mipaka na wajibu wao kwa Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili alilouliza, hizi kesi ambazo tumeshinda lini zitamalizika? Tunajitahidi sasa hivi kuchukua hatua mbalimbali ikiwemo kuimarisha Ofisi ya Mwendesha Mashtaka kuhakikisha upelelezi unakamilika haraka iwezekanavyo.

Lakini pia, kama nilivyosema juzi tunazo Kamati za kusukuma kesi, tunaita *Case Flow Management Committees* katika ngazi za Wilaya, ngazi ya Mkoa na Ngazi za Mahakama Kuu kuhakikisha kwamba, tunachambua sababu za kusababisha kesi nyingi kuchelewa kuamuliwa Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. HAMAD MOHAMED RASHID:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nchi yetu inajitahidi sana kujenga Utawala wa Sheria. Kumekuwa na malalamiko mengi ya wananchi ambao wamepata hukumu Mahakamani kuishitaki Serikali ikashindwa. Lakini Serikali kutoa haki kwa wale walioshinda Mahakamani limekuwa ni tatizo sugu sana na watu wamefika mpaka kwenda kwenye Kamati za Maadili, na kadhalika. Lakini bado utekelezaji huo hautekelezwi.

Je, Serikali kwa nini inaendelea kuvunja amri za Mahakama?

**MWENASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali haivunji hizo haki za wananchi. Mara ambapo Mahakama imetoa maamuzi na Serikali ina haki yake, kama haikuridhika inakata rufaa na haijulikani hiyo rufaa itamalizika lini. Kwa ufupi tu niseme kwamba, Serikali imekuwa ikitekeleza wajibu wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

Na. 34

**Ukosefu wa Mahakama Wilaya ya Mbogwe**

**MHE. AUGUSTINO M. MASELLE** aliuliza:-

Wilaya ya Mbogwe inakabiliwa na uhaba mkubwa wa huduma za Kimahakama kwa sababu, hakuna Mahakama ya Wilaya zaidi ya Mahakama mbili za Mwanzo:-

(a) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama za Mwanzo ili kusogeza huduma karibu na wananchi?

(b) Je, ni lini Serikali itajenga Mahakama ya Wilaya ya Mbogwe?

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria, ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mahakama inaendelea na mpango wake wa kujenga Majengo ya Mahakama nchini kulingana na upatikanaji wa fedha, ili kusogeza huduma karibu na wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Mpya ya Mbogwe upo kwenye Mpango wa Ujenzi wa Mwaka 2014/2015. Hata hivyo, mradi huu haujatekelezwa kutokana na ukosefu wa fedha za Miradi ya Maendeleo.

Aidha, ujenzi wa Mahakama ya Wilaya ya Mbogwe utatekelezwa pindi Mahakama itakapopatiwa fedha.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELLE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kumwuliza Naibu Waziri Maswali mawili madogo ya Nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la kwanza. Kwa kuwa, Wilaya ya Mbogwe ni Wilaya Mpya na Idara nyingi za Serikali tayari zina Wakuu wa Idara, lakini Mahakama haijaleta Mkuu wa Idara ya Mahakama kwa maana ya Hakimu wa Mahakama ya Wilaya.

Je, ni lini Serikali itafanya uteuzi huo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, huduma kwa wananchi ili ziweze kutekelezwa kwa urahisi zinahitaji nyenzo na vitendea kazi kama magari na pikipiki na vifaa vya kiofisi.

Je, Serikali ina mpango gani kuipatia Mahakama ya Wilaya ya Mbogwe usafiri kama gari na pikipiki? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Katiba na Sheria ningependa kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Augustino Manyanda Maselle, Mbunge wa Mbogwe, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza sitamtendea haki Mheshimiwa Maselle, kama sitampongeza kwa jitihada zake za kuhakikisha haki inapatikana mapema na haraka katika

Jimbo la Mbogwe, katika Wilaya ya Mbogwe. Hata mwezi wa nne aliuliza swali kuwa ni lini sasa Mahakama hii ya Mbogwe itajengwa ili kuhakikisha wananchi nao wanapata haki. Mheshimiwa Agustino Maselle, hongera sana kwa kazi nzuri unayofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mkuu wa Idara ya Mahakama ni lini atateuliwa. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kipaumbele chetu sasa hivi katika Sekta nzima ya Utoaji Haki ni kuhakikisha tunayo majengo ya kutosha katika Mahakama zote za Wilaya, za Mwanzo na Mahakama Kuu, ikiwemo na suala la kuhakikisha kwamba, tumepeleka Mahakimu katika Mahakama za Wilaya.

Kwa hiyo, naomba nikuahidi kwamba, hilo ni suala ambalo tutalitekeleza haraka iwezekanavyo kama halijafanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika suala la huduma ya vitendea kazi, Bunge lako Tukufu ni shahidi. Mwaka huu wa fedha tuliweza kununua magari 137 na kusambaza katika Mahakama zote za Wilaya na tumeweza kununua pikipiki za kutosha katika Mahakama za Mwanzo. Naomba nifuatilie.

Lakini kwa nini Mbogwe haijapata, labda kwa kwa sababu pia, bado Mtendaji Mkuu pale hajateuliwa. Lakini nakuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba, wananchi wa Mbogwe waendelee kuwa na imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi (CCM), tutahakikisha utoaji haki haucheleweshwi na unapatikana mapema na kwa haraka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru. *(Makofi)*

Na. 35

**Kifuta Jasho kwa Ndugu wa Watu Waliouawa na Wanyama Wakali na Walioharibiwa Mazao yao**

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE** aliuliza:-

Tatizo la wanyama wakali la kuua watu na kusababisha mazao ya wananchi waishio karibu na hifadhi zetu limekuwa sugu. Kwa mfano, mwaka 2009 hadi 2014 watu wapatao 6 katika Jimbo la Karatu waliuawa na tembo/nyati na warithi wa hao waliouawa wamejitahidi kufuatilia kifuta machozi bila mafanikio:-

(a) Je, Serikali inatoa kauli gani kuhusu malipo ya kifuta machozi kwa hao ndugu?

(b) Mwaka 2009 hadi 2014 wananchi 292 wa vijiji saba (7) waliharibiwa mazao yao na Serikali ilifanya tathmini ya kifuta machozi kwa wananchi hao na ilipata jumla ya Shilingi 17,326,000/=.

Je, ni lini Serikali itawalipa Wananchi hao kifuta machozi chao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, naomba kutoa pole kwa wananchi wa Karatu walioathirika na wanyama wakali na waharibifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mchungaji Israel Natse, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeendelea kufuatilia suala la wananchi wa Karatu kuuawa na kujeruhiwa na wanyama wakali na kuelezwa kuwa watu 8 waliuawa na tembo, fisi na nyati katika kipindi cha mwaka 2011 mpaka 2014 na siyo watu 6 kama ilivyoelezwa na Mheshimiwa Mbunge.

Wizara imeendelea kuwasiliana mara kwa mara pamoja na kuandika barua kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri Karatu kumtaka awasilishe vielelezo vitakavyotambuliwa na kuhakikiwa kwa ajili ya malipo ya watu 8 waliouawa na watu watatu waliojeruhiwa kwa mujibu wa Kanuni ya Kifuta Machozi. Wizara yangu itakamilisha taratibu za malipo pale itakapopata nyaraka hizo muhimu.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara ilipokea maombi ya malipo ya kifuta machozi kutoka kwa wananchi wa Karatu ambao mazao yao yaliharibiwa na wanyama waharibifu. Uhakiki wa maombi hayo ulibaini kuwa jumla ya wananchi 222 badala ya 292 wa Vijiji vya Mangula Juu, Fihalamo, Ositeri, Kambi ya Simba, Kitete, *Upper Kitete* na Karatu Mjini waliathirika kutokana na wanyamapori hao. Uhakiki huo pia, ulibaini kuwa jumla ya ekari 346.5 za mazao ya aina mbalimbali ziliharibiwa.

Kutokana na uhakiki huo ilibainika kuwa, jumla ya madai ya wananchi ni 20,371,000/= badala ya 17,326,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi ya uhakiki wa orodha ya awali ya Vijiji 7 ilishawasilishwa kutoka Wilaya ya Karatu yenye madai ya kifuta jasho kutokana na uharibifu wa mazao ya wananchi na imekamilika. Taratibu za malipo zinafanyika, ili wananchi hawa waweze kulipwa madai yao kabla ya tarehe 31 Juni, 2015.

**MHE. MCH. ISRAEL Y. NATSE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme kidogo kama Mchungaji leo, maana wamesema nina kauli kali. Naomba kunukuu sehemu ya majibu ya Naibu Waziri: "Wizara imeendelea kuwasiliana mara kwa mara na kuandika barua kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Karatu kumtaka awasilishe vielelezo vitakavyochambuliwa na kuhakikiwa kwa ajili ya malipo ya watu 8 waliouawa na watu 3 waliojeruhiwa. Kwa mujibu wa Kanuni ya Kifuta Machozi Wizara yangu itakamilisha taratibu za malipo pale itakapopata nyaraka hizo muhimu."Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwa kuwa, wananchi hawa wamefuatilia tangu 2009 mpaka 2014. Kumbe Wizara imekuwa ikiwasiliana na Mkurugenzi Mtendaji na Ofisi yake na ikachukuliwa kwa uzembe tu kuachwa mpaka leo na Wizara inasema itashughulikia itakapopata nyaraka hizo. Naomba Kauli ya Serikali kuhusu Watendaji hao, Mkurugenzi Mtendaji na watu wake, wachukuliwe hatua zipi Waziri aniambie, wananchi 222 hawawezi kuteseka?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili. Kwa kuwa, madai haya ni ya muda mrefu na Wizara imekiri kwamba, malipo yatafanyika kabla ya Juni 31, 30 *anyway* 2015, hii ni sawa na haki iliyokataliwa! Maana unaichelewesha hiyo haki kwa muda mrefu na kuipeleka mwisho wa mwaka wa fedha. Naomba Waziri aniambie kwa hakika malipo haya yatalipwa lini na wananchi wanufaike? Ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii, naomba kumjibu Mheshimiwa Mchungaji Natse, maswali yake mawili kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza na swali la pili ambalo amesema madai. Tumesema katika maelezo yetu kwamba, ifikapo tarehe 30 Juni, mwaka huu 2015 tutahakikisha wale wananchi 222 wamelipwa, ifikapo. Ina maana hii iko *between* kati ya sasa mpaka Juni, 30.

Sasa nataka nimhakikishie tu kwamba, vielelezo vyote vya msingi kama Serikali tumevipata na tuko kwenye maandalizi ya kulipa kwa sababu, madai yako mengi katika nchi nzima. Kwa hiyo, tunalipa *quarter* kwa *quarter*. Kwa hiyo, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mchungaji kwamba, hawa wahanga tutawalipa na tuko tayari kuwalipa na haki zao za msingi watazipata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikija swali la (a). Ni juzi tumemwandikia tena barua Mkurugenzi wa Halmashauri kumkumbushia kwamba, kuna watu wanadai haki zao za msingi. Sasa nataka nimhakikishie tu kwamba, mimi nitafuatilia kuhakikisha tunapata haya majibu na hizi haki za hawa wananchi wanane (8) waliokufa kutokana na wanyama wakali tunawalipa haki zao zote. *(Makofi)*

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Wanyama waharibifu wamekuwa wakisumbua sana Jimbo la Rombo, hasa tembo Ukanda wa Chini na nyani Ukanda wa Juu. Madai ya fidia kwa wananchi hawa yako pia Wizarani muda mrefu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninaomba Waziri atoe jibu la jumla ni lini wananchi wa Rombo, Karatu na maeneo mengine ambayo wanyama hawa wamekuwa wakiuwa wananchi, wakiharibu mazao yao watakapopata fidia zao?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nimjibu swali kaka yangu, Mbunge wa Rombo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli na hapa tuna orodha ya madai yote. Sasa tutalipa kutokana na jinsi watu walivyoleta madai yao na kama vielelezo vimekamilika tutaendelea kulipa. Tatizo ni kwamba, madai yanakuja Wizarani, lakini yanakuwa hayana vielelezo vya kutosha.

Na. 36

**Kurekebisha Mipaka na Kuongeza Watumishi wa Pori la LWAFI Game Reserve**

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA** aliuliza:-

Hifadhi ya Wanyamapori *(TANAPA)* walishaombwa kurekebisha mipaka ya Pori la *Lwafi Game Reserve* ili kutoa ardhi zaidi kwa wananchi wa Vijiji vya Mtapenda, China, King'ombe, Mlambo, Namasi, Msamba na Ng'undwe ambao wana uhaba mkubwa wa ardhi:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kutekeleza hilo?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuongeza watumishi wa Pori hilo, kwa kuwa waliopo sasa ni wachache sana?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kujibu swali la Mheshimiwa Desderius John Mipata, Mbunge wa Nkasi Kusini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Mwenyekiti, Pori la Akiba la Lwafi lilitangazwa kwenye Gazeti la Serikali Namba 284 la terehe 24 Desemba, 1993. Pori hili lina eneo la ukubwa wa kilometa za mraba 2228 na lipo Wilaya ya Nkasi na Mpanda. Pori hili lilikabidhiwa Wizara ya Maliasili na Utalii tarehe 8 Aprili, 2011.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uanzishwaji wa maeneo ya Hifadhi hufanyika kwa kufuata taratibu zinazoainishwa Kisheria. Hali kadhalika utaratibu wa kuainishwa maeneo yaliyohifadhiwa kuwa ardhi ya Kijiji hufuata utaratibu huo huo. Wizara haijatoa ahadi yoyote ya kurekebisha mipaka wala hakuna mipango ya kutengua mipaka ya pori hilo kwa ajili ya kumega ardhi na kuwaongezea wananchi wa vijiji vinavyozunguka.

(b) Mheshimiwa Mwenyekiti, Wizara inatambua suala la upungufu wa watumishi katika Pori la Akiba la Lwafi na mapori mengine nchini. Jumla ya watumishi 459 wakiwemo Maafisa Wanyamapori 27 na Wahifadhi Wanyamapori 332 wameajiriwa. Kati ya hao watumishi 9 wamepelekwa pori hilo na hivyo kuongeza idadi ya watumishi kutoka 8 hadi 17. Wizara itaendelea kuomba Kibali cha kuajiri Watumishi wengine, ili kutosheleza mahitaji.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nina maswali mawili ya nyongeza:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado wananchi wa Vijiji vya Nkata, King'ombe, Mlambo, Mtapenda, China, Namasi, Kasaba na Ng'undwe wana uhaba mkubwa sana wa ardhi. Serikali sijaona kama wametoa ufafanuzi ni njia zipi wazitumie, ili wakidhi haja ya Kisheria ya kuweza kupata kutatua tatizo lao la ukosefu wa ardhi; ningeomba kwa muhtasari Mheshimiwa Waziri atufafanulie wananchi watumie njia gani? Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili. Pamekuwepo na mahusiano sio mazuri sana kati ya Wahifadhi wachache wa *Lwafi Game Reserve* na wananchi wanaozunguka vijiji vile. Ninatolea mfano mwezi wa kwanza (Januari) Kijiji cha Ng'undwe waliwavamia wananchi na kuwafuata majumbani na kuwacharaza viboko. Sasa kwa wahifadhi wa tabia ya namna hiyo Serikali ina kauli gani?

Maana wananchi wanachukulia kwamba, ni ukatili tu wa Serikali kumbe sivyo!

Kwa hiyo, kwa watu wa namna hiyo, Serikali ina kauli gani?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba kumjibu Mheshimiwa Mipata, maswali yake (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli, historia ya pori hili lilikuwa linamilikiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Wilaya ya Nkasi wenyewe kwa hiyari yao waliamua kulitoa kwa Wizara ya Maliasili na Utalii. Sasa vigezo vilevile vilivyotumika kutukabidhi pori hili, wanatakiwa warudi kwenye vigezo vilevile kuomba kama wanataka kipande cha ardhi warudishiwe kwenye eneo lao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la mahusiano; ni kweli kuna baadhi ya maeneo kuna mahusiano siyo mazuri. Hakika Askari wetu hawaruhusiwi kutoa adhabu kwa sababu, taratibu za Kisheria zinajulikana, kama mtu kafanya kosa anatakiwa apelekwe kwa taratibu za Kisheria.

Mheshimiwa Mbunge, kama itatokea jambo hili linajitokeza tena ni suala la msingi kutuletea taarifa mapema ili haki zitendeke. Mpaka sasa hivi kuna baadhi ya Askari tumeshawachukulia hatua kwa kuwasimamisha kazi kwa vitendo vibaya wanavyovifanya katika maeneo ya hifadhi zetu.

**MHE. SAID A. ARFI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, *Ubende WMA* tatizo lake linafanana sana na hili la Lwafi kwamba, limehodhi eneo kubwa la kilimo la wananchi. Uanzishwaji wa *Ubende WMA* haukuzingatia taratibu za kuwashirikisha wanavijiji katika Mikutano Mikuu ili kutoa maeneo yao na mgogoro huu ni wa muda mrefu.

Je, Waziri atakuwa tayari kwenda kushughulikia mgogoro huu na kupata ufumbuzi tukifuatana naye?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, niko tayari kufuatana na Mheshimiwa Mbunge kwenye eneo husika, lakini nataka nimwambie tu *WMA* ni eneo la wananchi. Kwa hiyo, mipango ya matumizi bora ya ardhi wanapanga wananchi wenyewe. Kwa hiyo, ni mali yao siyo mali ya Wizara kwa hiyo tutakuwa pamoja kwenda kushughulika na hawa wananchi.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naomba niishukuru serikali kwa kuanza kushughulikia tatizo la mpaka kati ya vijiji kumi na moja na pori la akiba la Mkungunero. Lakini sambamba na hilo kuna tatizo lingine sugu la wananchi katika vijiji vitatu na pori la akiba la Swagaswaga.

Wananchi hawa wanapata dhiki, wanasukumwa, wanateswa sasa ni lini Serikali itakwenda kuangalia tatizo hili na kupata utatuzi wake. Nimeshaongea sana na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri naomba jibu ili wananchi wa vijiji hivyo vitatu wapate amani. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza naomba nimpongeze sana Mheshimiwa zabein Mhita, kwa kufuatilia sana masuala haya na tulikubaliana tufanye kazi hatua kwa hatua *so long* tumeshashughulikia kwa kina suala la Mkungunero. Nataka nimhakikishie tu baada ya Bunge hili tutaenda kushughulikia suala la pori la akiba Swagaswaga.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri nakupongeza sana majibu yako sahihi na ni mafupi, Mheshimiwa Ignas Malocha.

**MHE. IGNAS A. MALOCHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru sana kwa kuniona ili niulize swali la nyongeza. Inaonyesha dhahiri kuwa Serikali inajali sana wanyamapori kuliko binadamu na sote tunafahamu kwamba ardhi haiongezeki, lakini binadamu wanaongezeka.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kufanya marekebisho katika baadhi ya mapori ya akiba ili kuwezesha wananchi kupata maeneo ya kulima na kufuga? Kwa mfano pori la akiba la *Uwanda Game Reserve* na mapori mengine yaliyopo nchini?

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Maliasili na Utalii naomba nimjibu Mheshimiwa Mbunge swali lake kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu tumeshaanza kuangalia mapori ya akiba na mapori tengefu, yale ambayo tutaona kwamba hayakidhi vigezo vya kuendelea kuwa mapori ya hifadhi tutayarudisha. *(Makofi)*

Na. 37

**Watanzania Waishio Nje ya Nchi Kujiandikisha Kwenye Balozi za Uingereza**

**MHE. JOHN P. LWANJI** aliuliza:-

Ni miaka 54 sasa tangu tujipatie uhuru raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi hutakiwa kujiandikisha majina yao na anuani zao katika ofisi za Ubalozi wa Uingereza pale ambapo Ofisi za Ubalozi wa Tanzania haziko karibu.

Je, ni kwa nini iwe ofisi za Ubalozi wa Uingereza tu wakati kuna nchi zingine nyingi ambazo Tanzania ina mahusiano mazuri na ya karibu zaidi?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa John Paul Lwanji, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, raia wa Tanzania wanaoishi nje ya nchi wanashauriwa kujiandikisha majina yao na anuani zao katika Ofisi za Ubalozi wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kama hakuna ubalozi wa Tanzania katika nchi husika, wajiandikishe Ofisi ya Ubalozi wa Uingereza. Ushauri huo unalenga kurahisisha utoaji wa msaada au huduma za dharura na ulinzi ambapo raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania anastahili kupata ikiwa imetokea msukosuko au shida yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama inavyofahamika baada ya Vita Kuu ya Pili ya Dunia na hali ilivyokuwa kwa makoloni mengine ya Uingereza, Tanzania ilikuwa chini ya uangalizi wa Uingereza ambapo tulitambuliwa kuwa ni raia wa Jumuiya ya Madola chini ya Sheria ya Uraia ya Uingereza na Sheria nyingine zilizotumika baada ya uhuru. Swali hili limekuwa ni la kihistoria na kimapokeo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika jumuiya ya Afrika Mashariki kwa sasa nchi wanachama wapo katika hatua za kujadili namna ya kufanya Pasipoti za nchi hizo kuwa za Kimataifa pia kuingia katika ushirikiano wa Kidiplomasia na Kimabalozi ambapo raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wataweza kujiandikisha au kupata huduma katika balozi za nchi wanachama pale ambapo ofisi za Ubalozi wa Tanzania hazipo karibu.

**MHE. JOHN P. LWANJI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani. Nina maswali mawili ya nyongeza. Kwanza ili kuimarisha mahusiano na nchi rafiki hasa kwa kipindi hiki ni kwa nini Serikali haikasimu nchi nyingine? Kwa mfano kikanda kwamba watu wanaoishi nchi za Mashariki ya Mbali kama Uchina ambapo Wachina ni marafiki zetu kwa muda mrefu.

Ni kwa nini watu wetu wasiruhusiwe kuandikisha huko na katika balozi hizo na Amerika. Kwa mfano tumekuwa na mahusiano mazuri tu kwa muda wa miaka mingi kwa nini waende kwenye Ubalozi huo wa Uingereza tu, kitu ambacho kinatukumbusha historia ya ukoloni?

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ningependa kujua kama wanajiandikisha ili kuweza kupata misaada ya dharura na haki nyingine Serikali inasema nini juu ya haki za hawa raia wa Tanzania wanaoishi nje juu ya kujiandikisha kwa ajili ya Upigaji Kura?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa John Paul Lwanji, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama nilivyosema hili suala la kutakiwa watu wajiandikishe kwenye Ubalozi wa Uingereza pale ambapo Tanzania haina Ubalozi, ni suala la kihistoria na linaweza likarekebishika siyo historia ambayo imeandikwa kama *Biblia* au *Quran*.

Wazo la kuwa tufikirie kuandikisha kwenye Balozi au Uchina au Marekani ni suala la kuliweka na kwa hili Serikali iko *flexible* baada ya kutazama faida zake. Faida kubwa ni uwezo, lakini pia ni mtandao mpana wa Balozi za Uingereza kuliko sehemu nyingine. Kwa hiyo, tutaliangalia hili wazo na nafikiri siyo tatizo kujipanua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu swali la kujiandikisha na Kupiga Kura kwa Watanzania nafikiri ni wazo zuri ambalo tumekuwa tunalizungumza hapa na sisi ambao tunaweza tukaamua kwamba wapige kura, wapige vipi na kwa utaratibu gani, kwa sababu ni suala la Sheria ya Uchaguzi ambayo pengine tunaweza tukapata fursa ya kuisemea vizuri wakati ukifika. *(Makofi)*

Na. 38

**Watanzania Waliofungwa Nje ya Nchi**

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO (K.n.y. MHE. REBECCA M. MNGODO)** aliuliza:-

Zaidi ya Wafungwa 130 Watanzania wanatumikia kifungo nchini China na Umoja wa Mataifa umetoa idhini ya wafungwa wanaotumikia vifungo nje ya nchi zao kurudishwa na kutumikia vifungo hivyo nchini mwao.

Je, Tanzania imerudisha wafungwa wangapi waliopo magerezani nje ya nchi hususan China?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Rebecca Mngodo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Tanzania inatambua kuweko Watanzania waliofungwa nchi za nje na wanatumikia vifungo vyao katika magereza yaliyo katika nchi hizo ikiwemo Uchina. Utaratibu wa wafungwa waliofungwa nchi za nje kurudishwa na kutumikia adhabu za nchi zao nchini kwao upo kisheria na kunatakiwa kuwepo makubaliano tu ya mkataba na kubadilishana wafungwa baina ya nchi mbili husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinazoishia mwaka 2014 zinaonyesha kuwa kuna wafungwa wa Tanzania 185 wanaotumikia vifungo mbalimbali katika magereza nchini China. Hata hivyo Serikali ya Tanzania bado haina mkataba wa kubadilishana wafungwa na nchi ya China. Mpaka sasa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilikuwa na mkataba na nchi mbili ambazo ni Mauritius na Thailand na imeshapokea wafungwa kumi Watanzania waliokuwa wamefungwa nchini Mauritius kuja kutumikia adhabu zao hapa nchini. Hata hivyo mkataba wa Mauritius umemalizika muda wake.

**MHE. SUSAN A. J. LYIMO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi yakuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Mheshimiwa Waziri ambayo kimsingi siyaafiki sana ni kwamba Tanzania na China wamekuwa marafiki wa muda mrefu sana toka enzi ya Mao Tse Tung, lakini vile vile ukiangalia wafungwa tumeenda China wafungwa wa Tanzania ni wengi sana na wafungwa hao wengi wao ni wa madawa ya kulevya. Vile vile tunatambua kwamba nchi ya China wafungwa wa madawa ya kulevya huwa wananyongwa wakati hapa Tanzania hawanyongwi.

Je, Serikali haioni kuna umuhimu mkubwa sana wa kuwa na mkataba huo na China ili Watanzania hawa waweze kurudi nyumbani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili kwa kuwa wafungwa hawa ni wa madawa ya kulevya.

Je, ni kweli kwamba Serikali inaona kigugumizi kuwa na huu mkataba kwa kuwa wanajua kwamba wafungwa hawa wakirudi hapa nchini watawataja vigogo ambao wamewatuma kwa sababu tunajua kwamba vigogo ndiyo wanahusika na biashara hii? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kwamba kuna wafungwa wengi sana nchini China na anashangaa kwa nini Serikali haijafanya mkataba na China. Mazungumzo na China, yanaendelea lakini hata yangeendelea yakamalizika tusingewasaidia wafungwa ambao wamehukumiwa kunyongwa kama anavyosema na pengine ingekuwa haina ladha pia kusema tunawaondoa kule wakati kifungo chao ni kunyongwa lazima wanyongwe kule. Kama wangekuwa na kifungo ambacho kina muda hao ndiyo ambao tunaweza tukawasaidia kwa utaratibu huu wa kubadilishana wa kunyongwa mtabadilishana kitu gani? Sijaelewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hisia kwamba hatufanyi mazungumzo na China kwa sababu watatajwa vigogo. Kwa kweli hili siyo dhumuni kwa vyovyote kwa Serikali na Serikali ina nia nzuri na hata huko walipo Serikali inafika. Serikali ya Tanzania kupitia Balozi zake au Ubalozi wa China huko wengine huwa wanapata siku wanawatembelea hawa na Wachina wenyewe wamekuwa wanafanya mazungumzo ya mara kwa mara.

Niwaambieni tu kitu kimoja kwamba katika wafungwa ambao walihukumiwa kunyongwa China wa nchi zote wameshanyongwa wakabakishwa Watanzania, madhumuni wamategemea pengine tunaweza tukazungumza au wakapunguziwa kifungo. Kwa hiyo, hiyo hisia ya Mheshimiwa kwa kweli siyo ambayo Serikali inaifikiria.

**MHE. MUHAMMAD IBRAHIM SANYA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali moja dogo la nyongeza. Kwa kuwa mbali ya wafungwa ambao au

watuhumiwa ambao wako katika magereza au katika mahakama za nchi za nje, lakini Watanzania wengi ambao wamejiingiza katika biashara hii wanateseka na wanatangatanga katika miji mikuu kwa baadhi ya nchi za Asia na hata Afrika.

Unapotembelea kwa mfano *Bombay* katika mtaa wa *Mohamed Ally Road* utakuta Watanzania wengi ambao tayari wameshauza hata pasipoti zao na unapokwenda *Johannesburg* wako vile vile. Serikali ina mpango gani wa kufanya utafiti na kuwagundua hawa na kuwasaidia ili kuwarejesha nyumbani wasiteseke nchi za nje wakiwa hawana watu wa kuwasaidia?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI**: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda nijibu swali la Mheshimiwa Sanya, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba kwenye baadhi ya miji mikuu ya baadhi ya nchi kuna Watanzania wengi ambao wanazagaa na ni rahisi kuwaona na ukiwaona utawahurumia na hii ni kazi ya Serikali ya Tanzania kupitia balozi zao kuwapa misaada ambayo inahusika, lakini hasa ni ya kisheria na ushauri nasaha wa namna ya wengine wanaondoka kwa hiari zao na si rahisi kukubali kurudi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo moja ambalo linatokea ni kwamba watu hawa hata kama Watanzania wote wataitwa Ubalozini hawa hawawezi kuja *most of them*. Sasa namna ya kuwafikia ni ngumu lakini nafikiri kama Serikali tutajipanga ili tuone tunawasaidia kwa sababu ni Watanzania. *(Makofi)*

Na. 39

**Kufufua Viwanda Katika Jiji la Tanga**

**MHE. OMARI RASHID NUNDU** aliuliza:-

Ilani ya CCM ya Mwaka 2010 ilinuia kulirejeshea Jiji la Tanga Viwanda ambavyo vilibinafsishwa na vimeshindwa kufanya kazi kama ilivyotarajiwa na vingine kufungwa kabisa. Kwa mfano viwanda vya chuma, mbao, blanketi na mbolea.

(a) Je, Serikali imechukua hatua gani katika kutekeleza nia ya CCM ya urejeshaji wa Viwanda katika Jiji la Tanga?

(b) Je, Viwanda vipi vimefufuliwa na uzalishaji wake ukoje?

(c) Je, ni kwa nini Serikali isivichukue viwanda vya chuma, mbao na mbolea ambavyo wawekezaji wake hawajafanya lolote?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa viwanda na Biashara napenda kujibu swali la Mheshimiwa Omari Rashid Nundu, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kufanya masahihisho kidogo kwenye kipengele (c) kubadilisha Msajili wa Makampuni kuwa Msajili wa Hazina. Baada ya masahihisho hayo naomba nijibu swali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kupitia Mamlaka ya maeneo *EPZ* pamoja na Shirika la Maendeleo la Taifa *NDC* imeweka matayarisho na utaratibu wa kuvutia wawekezaji katika eneo la Tanga. Tayari Mamlaka ya *EPZ* imetenga hekta 1,363 katika eneo la neema Mkoani Tanga kwa ajili ya ujenzi wa viwanda na uthamini wa mali umekamilika.

Aidha *NDC* ina eneo la hekta 50 huko Kange Mkoani Tanga ambalo maandalizi ya kuliweka tayari kwa ajili ya kuvutia uwekezaji yanaendelea. Juhudi za kuvutia wawekezaji ili kuanzisha viwanda vipya zimefanyika pia ambapo kuna viwanda vingi vimeanzishwa kama vile kiwanda cha Maweni cha Saruji, *Athi River* cha chokaa, *Neelkanth* cha chokaa, *Tanga Pharmaceutical and Plastics Limited*, *Peepe Tanzania Limited*, *Pembe Flour Mill* na vinginevyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (b) kiwanda cha Saruji cha Tanga na *Tanga fresh* ni baadhi ya viwanda vilivyoboreshwa Mkoani Tanga ambavyo vinafanya kazi na kuongeza uzalishaji. Kiwanda cha *Tanga Fresh* kilichokuwa kinajulikana kama *Tanzania Diaries Limited,* Tanga, kilifufuliwa na sasa kinafanya kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, (c) kiwanda cha mbao na chuma kwa hivi sasa havifanyi kazi. Wizara yangu ilifanya mazungumzo na wamiliki wa viwanda hivi ili kubaini matatizo yanayowakabili na kukubaliana jinsi ya wao kuanza upya kutekeleza wa wajibu wa kimkakati.

Wizara imetambua kuwa tatizo la kiwanda cha mbao linatokana na gharama kubwa ya kupata malighafi Mufindi, Iringa hadi Tanga. Kuhusiana na kiwanda cha chuma kutokukamilika kwa makabidhiano baina ya mwekezaji na Msajili wa Hazina wa Hati zitakazo mwezesha mwekezaji kuendelea na kazi kumechelewesha ufanyajikazi wa kiwanda cha chuma. Wizara inafuatilia kwa karibu masuala hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwanda cha mbolea kilibinafsishwa kwa kuuzwa mali moja moja yaani *assets stripping* kutokana na kiwanda hicho kuchakaa sana ambapo mwaka 1991 bomba la hewa chafu lilianguka na hivyo kuwa hatari kwa maisha ya watu na kuongeza athari za uchafuzi wa mazingira ambapo uzalishaji ulisimamishwa.

Kwa bahati mbaya kiwanda hicho kilijengwa katikati ya makazi ya watu, hivyo kuifanya Serikali iamue kiwanda hicho kisiendelee na uzalishaji katika makazi ya watu ili kuepusha athari kwa wananchi wa eneo hilo, ahsante sana.

**MHE. OMARI RASHID NUNDU**: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Swali hili nilileta Juni, 2012. Kwa hiyo, nilitegemea sasa hivi lingepata majibu sahihi. Lakini kwa mkazi wa Tanga yoyote ataona kuwa haya majibu yaliyotolewa hapa hayaendani na hali halisi ilivyo hivi sasa. Lakini pia yanazusha maswali mengine. Kwa hiyo, basi nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la kwanza ni kiwanda cha *Tanga Fresh* ambacho nimeambiwa kilifufuliwa lakini hiki kilitoka tu *Tanzania Dairies* kikawa *Tanga Fresh*. *Tanga Fresh* ina matatizo sasa hivi na hiki kiwanda kinaweza kikafa na Kamati husika ilisema hapa katika Mkutano wa 18 kuwa zile pesa ambazo kiwanda hiki kimetozwa faini hazina mantiki, waliomba Wizara isaidie, sasa swali.

Wizara imefika hatua gani katika kuhakikisha kuwa fedha ambazo kiwanda cha *Tanga Fresh* kimetozwa kama faini zinaondolewa ili kiwanda kisiweze kuendelea kudhalilika na mwisho kufa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali la pili, katika majibu Mheshimiwa Waziri amesema kuwa Kiwanda cha *Fertilizer* iliamuliwa pasiwe na kiwanda tena pale, lakini kiwanda cha *fertilizer*

kilikuwa kina hekari kumi tu, lakini badala ya mtu kupewa hekari kumi hata kama angeendeleza Kiwanda cha *Fertilizer,* zimetolewa hekali 165 bila kuendeleza Kiwanda cha *Fertilizer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii inaonesha kuwa mtu huyo amepewa tu hiyo ardhi. Wakati *NDC* ina hekta hamsini tu za kuendeleza viwanda Tanga, mtu binafsi kwenye eneo ambalo halistahili kuwa na viwanda, amepewa hekali 165. Sasa wananchi wa Tanga wanataka kujua ni lini mtu huyu atanyang'anywa hiyo sehemu ili iweze kutumiwa kwa maendeleo ya Tanga?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kiwanda cha Tanga *Fresh*, Kiwanda hiki kilikuwa kimekiuka utaratibu wa *fair competition* yaani ufanyaji biashara wa haki. Kwa hiyo, ikachukuliwa hatua na *Fair Competition Commission* kwa kutozwa faini ya bilioni 4.2, ambayo baadaye walikuja kuridhiana kuwa ipunguzwe mpaka kufikia milioni mia nne na kitu. Sasa bado Kiwanda cha Tanga *Fresh* hawakuridhika na faini hiyo, wakapeleka suala hili kwa usuluhishi kwenye *Fair Competition Tribunal* ambayo sasa hivi hiyo kesi bado ipo na inaendelea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kufuatana na utaratibu uliopo kati ya miamala hauwezi sasa kwenda kuitoa ile kesi bila *Fair Competition Tribunal* kuiondoa au kutimiza uamuzi wa mwisho. Kwa hiyo, sisi kama Serikali tunaendelea kufuatilia kuangalia jinsi gani tatizo hili litatuliwa kwa njia ambayo itakuwa haina madhara kwa kiwanda, lakini vile vile na sheria ichukue mkondo wake. Kwa sababu kuna viwanda vingine kama *Murzah Oil* walifanya kosa kama hilo wakahukumiwa na wakalipa faini. Sasa itakuwa kama Serikali inakuwa na *double standard,* kwingine inatoa hukumu inaondoa, kwingine inachukua faini.

Kwa hiyo, hili jambo ambalo linabidi lijadiliwe kwa utaratibu ili liweze kufikia muafaka mzuri bila kuathiri kiwanda, lakini vile vile ili kutendea haki na viwanda vingine ambavyo wao huwa wanalipa faini kwa makosa hayo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusiana na Kiwanda cha *Fertilizer* juu ya hizo hekari 165 ambazo zilipewa bila kuendelezwa, naamini hili ni jambo ambalo itabidi tulifanyie kazi na kuangalia jinsi gani kama maeneo haya hayakuendelezwa, basi yachukuliwe, yatafutiwe mwekezaji ambaye anaweza akafanya kazi nzuri zaidi kwa kutumia maeneo hayo kwa ufanisi wa maendeleo ya Tanga. Ahsante.

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa fursa ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Haya matatizo ya kutofufuliwa kwa viwanda hayako Tanga peke yake, kwa sisi tunaotokea Mkoa wa Arusha, mimi na Mheshimiwa Lema tumeimba sana hapa suala la *General Tyre*, kiwanda ambacho kilikuwa kinaajiri watu wengi sana Mkoa wa Arusha miaka ile ambapo magari yalikuwa machache nchi hii. Leo magari ni mengi tulikuwa tunauza Afrika Mashariki yote kiwanda hakifufuliwi, hakuna ajira, vijana wanatapakaa mitaani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mara ya mwisho kwenye Bunge hili tumejibiwa kwamba Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* wanafufua kile kiwanda, lakini mpaka leo imekuwa ni ngonjera. Tunaomba kujua tu kwamba, hivi ni mpaka tumalize Ubunge ndiyo mtafufua kile kiwanda? Kinafufuliwa ama hakifufuliwi, kwa sababu wananchi wa Mkoa wa Arusha wanataka kufahamu, sintofahamu ya Kiwanda cha *General Tyre* nini kinachoendelea. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Naibu Waziri majibu, au Waziri wa Fedha una majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nina furaha na ufahari kuwaambia kuwa Kiwanda cha *General Tyre* kinafufuliwa. Kiwanda cha *General Tyre* kitafufuliwa sasa hivi.

*(Hapa Waheshimiwa Wabunge walikuwa wakijibishana na Mheshimiwa Naibu Waziri)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Kiwanda cha *General Tyre* kitafufuliwa mwaka huu.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, nami nisisitize kwamba sisi Wizara ya Fedha kupitia kwa *Treasury Registrar* kazi imekamilika na kwamba tuko katika mchakato na tuko kwenye *process* nzuri zaidi ya kukifufua hiki Kiwanda na *General* Tyre. Sasa hivi tutakwenda na kama alivyozungumza kwamba mwisho wa mwaka huu hiki kiwanda tayari kitakuwa kimeshafufuliwa.

**MHE. KHATIB SAID HAJI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Mheshimiwa Naibu Waziri alipojibu suala la Tanga *Fresh* amezungumzia kwamba suala hili bado liko katika mamlaka ya *Fair Competition*. Ikumbukwe kwamba Bunge hili lilipitisha azimio la kumaliza mgogoro huo. Hivi kuna taasisi iliyo juu zaidi kuliko Bunge hili na maamuzi yake?

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka Mheshimiwa Khatib afahamu kwamba suala hili tunavyolifuatilia sasa kwa kweli limekuwa ni suala la kisheria. Sasa masuala ya kisheria lazima twende kwa utaratibu wa kisheria. Tukifanya tofauti tutakuwa tumejiingiza kwenye matatizo ambayo aidha, tutakuwa tumeyategemea au hatukuyategemea. Hata hivyo, napenda kuwahakikishia wananchi wa Tanga kwamba, suala hili tunalifuatilia kwa ukaribu na litamalizika vizuri, kiwanda kitaendelea kutakuwa hakuna matatizo yoyote. Tunalifuatilia kwa karibu sana. (*Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Mkapa kwa niaba yake Mheshimiwa Njwayo!

Na. 40

**Huduma za mawasiliano ya simu**

**MHE. JUMA A. NJWAYO (K.n.y. MHE. DUSTAN D. MKAPA)** aliuliza:-

Kata ya Nangomba, Lumesule, Napacho na Chipuputa pamoja na Vijiji vya Chivirikiti, Marumba na Likokona hakuna huduma ya mawasiliano ya simu:-

Je, ni lini maeneo hayo yatapatiwa minara ya simu za mkononi?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Katika juhudi zake za kufikisha huduma ya mawasiliano nchi nzima, Serikali iliingia katika makubaliano na Kampuni ya *Viettel* kutoka Vietnam kufikisha huduma hiyo katika vijiji 4,000 nchini ndani ya miaka mitatu. Katika awamu ya kwanza ya utekelezaji wa makubaliano hayo, kampuni ya *Vietel* itafikisha mawasiliano katika vijiji zaidi ya 1,500 kabla ya mwezi Juni mwaka

huu, vikiwemo Vijiji vya Kata za Nangomba, Lumesule na Pacho, Chipuputa pamoja na Vijiji vya Chivirikiti na Likokona. Tayari wakandarasi wa kampuni hiyo wameshatembelea maeneo ya karibu na maeneo hayo yaani Kilimahewa, Mangaka, Chigwegwe, Lumesule na kuanza kazi za ujenzi wa minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo Kata ya Napacho, mnara utaanza kujengwa mwezi Mei, kwa gharama ya dola za Kimarekani 126,000. Aidha, Kata ya Marumba itapata mawasiliano kupitia kampuni ya *TTCL* mnamo mwezi Julai, mwaka huu.

**MHE. JUMA A. NJWAYO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Naomba kwanza kumpongeza Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yanayotia moyo sana, hata hivyo nina maswali mawili madogo ya nyongeza. La kwanza Jimbo hili na Wilaya hii ina matatizo makubwa sana ya mawasiliano, lakini pia Wilaya hii ndiyo ilikuwa Jimbo la Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Tatu, Mheshimiwa Benjamini William Mkapa.

Sasa pamoja na matatizo haya ya mawasiliano hatuoni kwamba kuna haja ya kufanya jitihada mahususi ili kuwapunguzia watu matatizo na mzee anaporudi kule likizo ya kupumzika pumzika asiwe anapata matatizo ya haya, maana ana mchango mkubwa kwenye Taifa hili? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, naomba kuipongeza Wizara kwa sababu katika Bunge la Kumi na Nane lilopita, waliahidi kusaidia minara tisa katika Jimbo langu la Tandahimba. Hivi ninavyoongea tayari minara miwili inakaribia kwisha; mmoja katika Kijiji cha Mdwani katika Kata ya Maputa na mwingine Kata ya Mkoreha, Kijiji cha Misufini, lakini bado tuna minara saba ile imebaki. Kuna uharaka gani wa kuhakikisha sasa na hiyo minara mingine inapatikana ili kuwaondolea matatizo wananchi wa Nanyumbu na wananchi wa Tandahimba?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye kabisa kwamba ipo haja ya kuhakikisha kwamba mzee Mkapa anapokwenda nyumbani kule Lupaso, basi mawasiliano yanakuwa hayana tatizo na ni kwa minajili hiyo na kwa kweli kote nchini siyo kwa mzee Mkapa tu, kote nchini, tumeamua kuongeza kasi kwa kushirikiana na Mfuko wetu wa Mawasiliano kwa Wote lakini na kampuni hii mpya ya mawasiliano ambayo msingi wake wa kuja hapa nchini ni kkupeleka mawasiliano vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kwamba walituomba orodha ya maeneo yote na sisi tukawapa orodha ya maeneo yote yasiyokuwa na mawasiliano na tukakubaliana kwamba huko ndiko watakakoanza na makubaliano yetu ni kwamba simu zianze kupigwa mwezi Julai.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napenda kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge wote kuanzia Mheshimiwa Njwayo na Mheshimiwa Mkapa kwamba yale maeneo yote ambayo hayana mawasiliano, basi huyu mtoa huduma mpya atafanya hivyo kabla ya mwezi Julai. Hata hivyo, hiyo haiondoi mipango yetu ya nyuma ya Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwa fedha zinazotolewa na Benki ya Dunia. Utaratibu huo pia utatumika kupeleka minara saba iliyobaki katika Jimbo la Tandahimba kabla ya mwezi Julai.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Ahsante pia kwa majibu yako mazuri Mheshimiwa Naibu Waziri, toka mwaka 2011 niliomba minara katika Kata ya Kizara na nikaenda na Waziri kule na akawahakikishia wananchi wa Kizara kwamba watapata mawasiliano. Mpaka leo hii Kata ya Kizara haina mawasiliano yoyote. Wananchi wameapa kwamba kama mawasiliano hayatafika, basi hakuna haja ya kukichagua Chama cha

Mapinduzi. Je, Serikali ina mpango gani wa kupeleka mawasiliano haraka katika Kata ya Kizara?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nataka nimwambie mambo mawili. Leo ni siku ya Alhamisi na siku ya Jumatatu ujumbe wa Kampuni ya *Tigo* ulikwenda Kizara kwenda kutazama eneo ambalo linapaswa kujenga mnara. Hilo la kwanza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya kazi kubwa sana ya kuweka mazingira ya uwekezaji katika kuhakikisha kwamba eneo kubwa la nchi yetu linafikiwa na mawasiliano. Pamoja na kwamba shughuli ya kupeleka mawasiliano ni ya sekta binafsi, lakini Serikali ya CCM kwa kutambua umuhimu wa kila mtu kupata mawasiliano imetumia njia zote kupitia Wizara yetu na Mifuko mbalimbali kuhakikisha kwamba itakapofika mwisho wa mwaka huu, basi Watanzania wote ambao wanastahili kupata mawasiliano, wanapata mawasiliano.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Tunaelewa suala la mawasiliano ni jambo muhimu sana na mara nyingi hapa ndani ya Bunge tumeomba katika Wilaya ya Karatu kuna Kata mbili na ndani ya Vijiji hivyo mawasiliano yana tabu sana ikiwemo Kata ya Mbulumbulu na Kata ya Bugeri na mliwahi kutuahidi hapa kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kwamba mtaleta minara ili wananchi waweze kupata mawasiliano. Tunataka kupata majibu, ni lini sasa Kata hizo zitapata mawasiliano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu eneo mahususi la Wilaya ya Karatu ambalo tuliahidi, ningependa Mheshimiwa tuonane, baada ya kipindi hiki ili nitazame eneo hilo mahususi tumefikia wapi. Hata hivyo, nataka niwahakikishie wananchi wa Karatu kwamba, kama Serikali yenye wajibu wa kuwahudumia tutahakikisha kwamba tunafikisha mawasiliano kule tulikoahidi, lakini majibu mahususi la eneo hilo mahususi tuonane na Mheshimiwa Mbunge nimpe taarifa.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwanza, naomba niipongeze Serikali kupitia Wizara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kusimamia makampuni haya ya kusambaza mawasiliano katika nchi yetu. Kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri tuliandika na kuomba baadhi ya maeneo ambayo hayana mawasiliano. Sasa nakumbusha tu tena, nina Kata nne ambazo ni Mputa, Mgombasi, Msisima na Limamu zenye watu wengi na wenye uwezo kiuchumi. Tunaomba sana iende ikawekwe minara na je, ni lini itatekelezwa kazi hiyo?

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu kwa kifupi! Waheshimiwa nawapa nafasi kwa sababu kidogo tunao muda na najua hii *issue* ya minara ni *very sensitive* kwenu.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Jimbo la Namtumbo, Wilaya ya Namtumbo, kwa miaka mingi licha ya changamoto ya mawasiliano bali changamoto nyingine za huduma za jamii imekuwa ni changamoto kubwa. Serikali ya Chama chetu kwa kutambua umuhimu wa kufikisha huduma hizo kwa wananchi, basi tumezungumza na wenzetu wa kampuni hii simu ya *Viettel*, pamoja na Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote kuhakikisha kwamba yale maeneo yote katika Wilaya ya Namtumbo ambayo hayana mawasiliano, yanapata mawasiliano kabla ya mwezi Julai mwaka huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba niwahakikishie wananchi wa Mheshimiwa Mbunge na tukitoka hapa nitampa taarifa ya mawasiliano. Namba za simu za wale

wanaofanya kazi katika Wilaya ya Namtumbo ili awapigie, wampe ratiba ya lini watapeleka mawasiliano katika Kata hizo alizozitaja.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Abdul, tutamalizia na Mheshimiwa Kafulila!

**MHE. ABDUL R. MTEKETA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Naomba kumwuliza swali la nyongeza Mheshimiwa Waziri kuhusu Kilombero, hasa hasa Masagati, Tanganyika Masagati na Uchindile, kwa sababu nilikuwa nawaona kila wakati Waziri na Naibu wake kuhusu suala hili mpaka leo hawajatekeleza. Naomba jibu. Ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri majibu! Umemwelewa swali lake?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli kwamba Mheshimiwa Mteketa amekuwa akija mara kwa mara akizungumza na sisi Wizarani kuhusu maeneo yasiyo na mawasiliano katika Wilaya na Jimbo la Kilombero na mimi mwenyewe nimefika Kilombero na nafahamu kwamba maeneo ya Tanganyika Masagati na kwingineko hakuna mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya ziara ya Kilombero nilikwenda na kuzungumza na Makampuni ya Simu na yakanionesha ratiba ya utekelezaji ya mipango yao ya kupeleka mawasiliano kwenye Jimbo hilo na tukawaomba waongeze kasi. Kwa hiyo, napenda nimhakikishie Mheshimiwa Mteketa kwamba tutarudi na kuwahimiza wale watoa huduma waliokuwa tayari na mipango ya kupeleka mawasiliano kwenye maeneo hayo, wafanye hivyo haraka wakati na sisi Serikali tukiendelea na mipango yetu mingine kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote.

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Suala la mawasiliano kwenye Mkoa wa Kigoma na hususan ukanda wa ziwa ambako hali ya usalama siyo nzuri sana, ni jambo ambalo nimeongea na Naibu Waziri na Waziri kwa muda mrefu. Mpaka sasa Kata ya Kalia ambayo ni miongoni mwa Kata za mpakani, mnara uko pale kwa takribani miezi sita haujawashwa, lakini wakati huo huo kuna Kata ya Mtegowanoti, kuna Kata ya Kandaga. Kata ambazo zipo ndani ya Tarafa ya Makao Makuu ya Wilaya, eneo ambalo kimsingi ni *strategic* kiutawala na kibiashara, lakini mpaka sasa hakuna mawasiliano ya simu. Kwa hiyo, ningependa majibu ya uhakika ya Naibu Waziri leo kwamba ni lini masuala ya mawasiliano katika maeneo haya ya kimkakati wanayafanyia kazi.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri, majibu kwa kifupi! Jiandae Mheshimiwa Deogratius!

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza Mheshimiwa Kafulila kama atatenda haki atakubali kwamba katika maeneo mengi aliyoleta hayana mawasiliano kwenye Jimbo lake, tumepeleka minara kadhaa. Hivyo, kazi imefanyika na yale ambayo alikuwa anakuja kuzungumza na sisi kwa kiasi fulani tumetekeleza. Kwa hiyo, ni dhahiri kwamba hatujamaliza maeneo yote kama aliyoyataja na safari ni hatua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana naye na sisi Serikalini tunaamini hivyo kwamba maeneo ya mpakani yana umuhimu wa kipekee wa kupata mawasiliano. Ndiyo maana tunao mpango maalum wa Serikali kutumia fedha zake wala siyo za watoa huduma, fedha zake za Mfuko kugharamia asilimia mia moja ya ujenzi wa minara katika maeneo ya mipakani kutokana na umuhimu wake kiusalama. Kwa hiyo, napenda niwahakikishie ndugu zetu wa Kigoma kwamba watapata mawasiliano haraka kutokana na mipango ambayo tunayo.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Mwaka jana nilizungumza kwa uchungu sana mpaka nikatumia usemi wa Kiingereza kwamba *it does pay to be a gentleman*. Mwaka 2012 nilimwandikia barua Waziri wa Mawasiliano nikiorodhesha Kata na Vijiji vya Wilaya ya Ngara ambavyo havina mawasiliano mazuri ya simu, ukizingatia Ngara inapakana na nchi mbili za Burundi na Rwanda tunahitaji kuwa na uhakika wa mawasiliano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, narudia tena, ni lini Wizara hii itatekeleza ahadi yake ya kuhakikisha kwamba kuna mawasiliano ya uhakika katika Wilaya zinazopakana na nchi za jirani? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO SAYANSI NA TEKINOLOJIA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza ni muhimu kuweka sahihi kwamba, Wizara yetu sisi haitengewi bajeti na Bunge hili ya kujenga minara. Tunachofanya sisi tunafanya mambo matatu, kwanza ni kuweka chachu na motisha kwa makampuni binafsi kujenga minara katika maeneo ambayo sisi tumeyaainisha kwamba yana matatizo ya mawasiliano. Pili kutafuta njia za ubunifu za kutafuta fedha kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote na kutoa ruzuku ya fedha kwa makampuni binafsi kujenga minara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi kama Bunge hili lingetutengea bajeti kama linavyotenga *REA* na kwingineko, kazi ya minara nchini ingekuwa imeshakwisha muda mrefu. Kwa hiyo, tunayo changamoto na sisi ya kuwashawishi watoa huduma binafsi kupeleka mawasiliano, lakini hilo haliondoi wajibu wetu wa kuhakikisha kwamba mawasiliano yanapatikana nchini kote na kwa haraka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nayakumbuka maeneo ambayo tulimuahidi Mheshimiwa Ntukamazina ikiwemo Keza na kwingineko na niliona orodha ya Kampuni za *Tigo* na *Vodacom* kupeleka mawasiliano kwenye baadhi ya maeneo ya huko. Kulikuwa na uchelewashaji wa ujenzi wa minara kutokana na ukweli kwamba kazi hii inafanyika sasa hivi katika maeneo mengi na kihistoria Wakandarasi wa Ujenzi wa Minara wamekuwa ni wachache tofauti na wa barabara na maji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri aliitisha mkutano Wizarani wa Makampuni ya Simu na Wakandarasi kuhakikisha kwamba ujenzi unaharakishwa ili tutimize ahadi yetu kwamba Waheshimiwa Wabunge mtakapokwenda kuomba kura tena, basi suala la mawasiliano lisiwe sehemu ya hoja.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu wa maswali umekwisha na maswali yamekwisha. Sasa nitatangaza wageni waliopo Bungeni asubuhi hii.

Wageni sita wa Mheshimiwa *Engineer* Gerson H. Lwenge, Naibu Waziri wa Ujenzi, wakiongozwa na Mchungaji Seith Mlelwa, Mkurugenzi wa Elimu, Dayosisi ya Kusini Njombe. Karibuni Dodoma. *(Makofi)*

Mgeni wa Mheshimiwa Godbless Lema ambaye ni Bi Neema Lema, mke wake. Karibu sana Bungeni. *(Makofi)*

Wageni wa Mheshimiwa Yahaya Kassim Issa ambaye ni ndugu Fatma Abdallah, Ndugu Haeshi Abdallah na Ndugu Asha Mohamed. Karibuni Bungeni Dodoma.

Maafisa 15 kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ambao ni Watendaji Waandamizi sita wakiongozwa na Ndugu Mbaraka Abdulwakil ambaye ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Mambo ya Ndani. Ahsanteni. *(Makofi)*

Watendaji Waandamizi wanane kutoka Idara ya Uhamiaji wakiongozwa na Ndugu Sylvester Ambokile, ambaye ni Kamishna Mkuu wa Uhamiaji, Ndugu Johari Sululu ambaye ni Kamishna wa Uhamiaji, Zanzibar na Afisa Uhamiaji Mkoa wa Dodoma, Ndugu Ali Ameir. Karibuni sana Dodoma.

Wageni kumi na mbili wa Mheshimiwa Mahamoud Hassani Mgimwa, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, ambao ni Wachungaji sita na Wainjilisti sita kutoka Jimbo la Mufindi Kaskazini. Karibuni Dodoma.

Wageni sita wa Mheshimiwa George Simbachawene, Waziri wa Nishati na Madini kutoka Jimboni kwake wakiongozwa na Ndugu Sangoma Kapesa. Karibuni sana Dodoma.

Wageni sita wa Mheshimiwa Joshua Nassari, ambao ni Wakuu wa shule zote za Sekondari za Kanisa la KKT Dayosisi ya Meru wakiongozwa na Mwalimu Tareto Nassari. Karibuni sana Dodoma.

Matangazo ya kazi; Mheshimiwa Dunstan Kitandula Makamu Mwenyekiti, Kamati ya Bunge ya Uchumi Viwanda na Biashara, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo kuwa leo tarehe 19, saa saba mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati katika Ukumbi wa Pius Msekwa.

Mheshimiwa Zaynab Matitu Vullu, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge Hesabu za Serikali, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati hiyo ya Hesabu za Serikali *(PAC)* kuwa leo tarehe 19 saa saba mchana kutakuwa na Kikao cha Kamati Ukumbi Namba 227, Ghorofa ya Pili, Jengo la Utawala.

Mheshimiwa Dkt. Festus Limbu, Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Bajeti, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati ya Bunge Bajeti kuwa leo tarehe 19 saa saba na robo mchana, kutakuwa na Kikao cha Kamati hiyo na Kikao hicho kitafanyika katika Ukumbi wa Msekwa B.

Tangazo, Alhaji Mohamed Missanga, anaomba kuwatangazia Waheshimiwa Wabunge Waislam kuwa kutakuwa na Kikao Maalum leo tarehe 19 saa saba mchana baada ya kuahirisha Kikao cha Bunge katika Ukumbi wa Msekwa.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Masuala ya Ukimwi, anaomba kuwatangazia Wajumbe wa Kamati kuwa, leo tarehe 19 saa saba mchana kutakuwa na kikao cha Kamati hiyo Ukumbi wa Msekwa C. Katibu!

## MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI

### Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Silaha na Risasi wa Mwaka 2014 (*The Firearms and Ammunition Control Bill, 2014)*

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba Muswada wa Sheria ya kupendekeza kutungwa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi sasa usomwe Mara ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa wingi wa rehema na kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki Mkutano huu wa 19 wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha kwa masikitiko makubwa napenda kuungana na wewe Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, kutoa pole nyingi na za dhati kwa familia ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge Mwenzetu, Marehemu *Captain* John Damiani Komba kwa kifo cha ghafla kilichotokea tarehe 28 Februari, Jijini Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania kama ilivyo nchi nyingine duniani inakabiliwa na tatizo la uzagaaji wa silaha haramu ambazo wakati mwingine zimekuwa zikitumika katika mapigano ya wenyewe kwa wenyewe, ugaidi, uwindaji haramu na kufanya vitendo mbalimbali vya kihalifu. Kwa kutambua tatizo hilo Jumuiya za Kimataifa, Jumuiya za Kikanda zimechukua hatua mbalimbali za kukabiliana na tatizo la kuzagaa kwa silaha katika nchi wanachama kwa kupitisha maazimio na itifaki mbalimbali kama ifuatavyo:-

(1) Azimio la Umoja wa Mataifa la Kudhibiti Kuzagaa kwa Silaha Ndogondogo na Nyepesi katika Nchi Wanachama la tarehe 20 Julai, 2001.

(2) Itifaki ya Kimataifa Kuhusu Kuzagaa kwa Silaha Ndogondogo na Nyepesi katika Nchi Wanachama la 31 Mei, 2001.

(3) Azimio la Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kudhibiti Silaha Ndogondogo na Nyepesi la 9 Machi, 2001.

(4) Itifaki za Nchi za Kusini mwa Afrika kuhusu Kudhibiti Silaha Ndogondogo na Nyepesi ya tarehe 14 Agosti, 2001.

(5) Azimio la Nairobi kuhusu Kudhibiti Silaha Ndogondogo na Nyepesi katika Nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika la Tarehe 15 Machi, 2000.

(6) Itifaki ya Nairobi kuhusu kudhibiti Silaha Ndogondogo na Nyepesi katika Nchi za Maziwa Makuu na Pembe ya Afrika ya Tarehe 21 Aprili, 2004.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha katika Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki kuna mpango madhubuti wa kukabiliana na uzagaaji wa silaha haramu. Ili kukabiliana na tatizo hili nchi wanachama zimekubaliana kuwa na mfumo wa sheria baada ya kusaini na kuridhia Maazimio na Itifaki kwa kutunga sheria ili kudhibiti umiliki wa matumizi ya silaha zinazomilikishwa kwa wananchi ili zisizunguke mikononi mwa wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Tanzania sheria ya sasa ya kuruhusu raia kumiliki silaha, *The Arms and Ammunition Act,* namba 2, ya 1991, ina upungufu mkubwa hivyo imeonekana na vyema itunge sheria mpya kwa kuzingatia maudhui yaliyoainishwa katika Itifaki ambazo nchi yetu imesaini na kuridhia badala ya kuifanyia marekebisho. Aidha, sheria hii inalenga kukabiliana na changamoto za uhalifu unaotendeka kwa kutumia mbinu mpya ambao unatendeka kwa kuvuka mipaka ya nchi moja hadi nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua zinazochukuliwa katika kutekeleza Itifaki na maazimio hayo. Nchi yetu imechukua hatua mbalimbali za utekelezaji wa Itifaki na Maazimio ya Kimataifa na Kikanda ambayo yamesainiwa kuhusu udhibiti wa silaha ndogo ndogo na nyepesi kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya *operation* 21 za pamoja za Kikanda.

(ii) Kuwaelimisha watu kusalimisha silaha kwa hiari na kupata mafanikio yafuatayo:-

(i) Jumla ya silaha 5,337 na risasi 4,821 zilisalimishwa na kuteketezwa kati ya mwaka 2000 na mwaka 2007 katika Mikoa ya Kigoma na Kagera. Silaha hizo ziliingizwa nchini na Wakimbizi waliokimbia mapigano katika nchi jirani.

(ii) Silaha 439 na risasi 37 zilisalimishwa kutokana na *Operation* Salimisha Silaha iliyofanyika mwaka 2012.

(iii) Kuteketeza silaha zilizosalimishwa kama ifuatavyo:-

- Agosti 2003 katika Maazimisho ya Siku ya Polisi, Silaha 1,000 ziliteketezwa Uwanja wa Taifa Dar es Salaam.

- Septemba 21, mwaka 2003 katika Semina ya Asasi za Serikali kuhusu uratibu wa Silaha iliyofanyika Jijini Mwanza, silaha 921 ziliharibiwa.

- Februari 27 mwaka 2004 wakati wa Semina ya Mashirika Yasiyo ya Kiserikali Jijini Mbeya, silaha 1,847 ziriharibiwa.

- Silaha 1000 ziriharibiwa katika Viwanja vya Jangwani Jijini Dar es Salaam 9 Julai, 2004 kwenye maazimisho ya *UN Arms Day*.

- 25 Agosti, 2004 kwenye Maazimisho ya Siku ya Polisi huko Zanzibar silaha 1,000 ziliharibiwa.

- Novemba 21 mwaka 2006 Mjini Kigoma kwenye Mradi wa Usalimishaji Silaha kwa Hiari uliofadhiliwa na *UNDP*, silaha 2,772 ziliharibiwa.

- Mei 25, 2009 Silaha zilizokuwa zikimilikiwa na Jeshi la Magereza zipatazo 2,765 ziliharibiwa Jijini Dar es Salaam.

- Juni 24, 2009 silaha 2,895 za Idara ya Wanyamapori ziliteketezwa Jijini Dar es Salaam.

- Machi 20, 2010 Silaha 1550 kutoka *TANAPA* na Mamlaka ya Ngorongoro ziliteketezwa Jijini Arusha.

- Mei 25, 2010 katika Maazimisho ya Siku ya Amani ya Afrika Duniani, Silaha 2,565 ziliteketezwa huko Bukoba, Kagera.

- Tarehe 27 Julai mwaka 2010 silaha 5,655 ziliteketezwa katika Uwanja wa Jamhuri Morogoro.

- Agosti Saba 2010, Silaha 1,217 ziliteketezwa Jijini Mwanza na;

- Februari 16, mwaka 2015, silaha 3,193 ziliteketezwa katika hafla ya kufunga Mradi wa *East* Afrika *GIZ Small Arms and Light Weapons Project*.

(iv) Kuweka alama ya silaha za Serikali, taasisi na watu binafsi. Hadi sasa silaha za taasisi za Serikali zimewekwa alama kwa asilimia 85 ambapo zoezi hili limefanyika mikoa karibu yote ya Tanzania. Aidha, silaha 31,050 za watu binafsi zimekwishawekewa alama. Taasisi ambazo silaha zake zimekwishawekewa alama ni pamoja na Jeshi la Polisi, Jeshi la Magereza, Idara ya Wanyamapori, *TANAPA*, Ngorongoro *NCAA*, Halmashauri za Wilaya, Taasisi za Fedha na Benki, Makampuni yanayomiliki migodi na makampuni yanayotoa huduma za ulinzi binafsi.

(v) Kuweka kumbukumbu za wamiliki wa silaha katika Kanzidata, kuelimisha jamii madhara ya kumiliki silaha haramu kupitia vipindi katika vyombo vya habari, maonyesho na vipeperushi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sababu za kupendekeza kutungwa kwa sheria mpya. Wizara inawasilisha mapendekezo ya kutungwa kwa sheria mpya kutokana na upungufu mwingi uliopo katika sheria ya sasa miongoni mwao kama ifuatavyo:-

(1) Kutokuanishwa umri wa kuanzia na ukomo wa kumiliki silaha;

(2) Kutokuwepo kwa mafunzo mahususi kwa wamiliki wa silaha;

(3) Kuwepo kwa mamlaka mbili zinazotoa leseni za kumiliki silaha yaani Jeshi la Polisi na Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa hutoa leseni za kumiliki Magobole;

(4) Kuziba mianya ya kuingiza silaha bandia;

(5) Kutoainishwa vyema silaha zinazoweza kumilikiwa na raia;

(6) Kutobainishwa kwa utaratibu wa kuweka alama kwenye silaha kisheria hasa kwa kuzingatia kuwa nchi yetu imeridhia na kusaini Mikataba ya Kimataifa na Kikanda ambayo inazitaka Nchi Wanachama kuziwekea alama silaha ndogondogo na nyepesi; na

(7) Kutokuwa na kifungu kinachosimamia makampuni binafsi yanayomiliki silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchakato wa kutunga sheria mpya. Mchakato wa kuandaa Muswada huu uliwashirikisha wadau mbalimbali na waliunga mkono kutungwa kwa Sheria mpya ya Kusimamia na Kudhibiti Umiliki wa Silaha za Kiraia. Aidha, vikao mbalimbali vimefanyika kuanzia mwaka 2003 na kushirikisha wadau ikiwemo Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, vyombo vya habari na asasi za kiraia na zisizo za Kiserikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa ujumla wadau walikubali itungwe sheria mpya badala ya kuifanyia marekebisho sheria ya sasa kwa sababu mbili kuu. Moja, maeneo yanayotakiwa kurekebishwa ni mengi mno na mbili kuhakikisha sheria mpya inaweka vifungu vinavyoendana na Itifaki na Maazimio ambayo nchi yetu imesaini na kuyaridhia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, madhumuni na sababu. Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Silaha na Risasi, Sura 223, kwa lengo la kutunga upya sheria nyingine kwa ajili ya

kusimamia na kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha za kiraia na risasi. Vile vile sheria inatungwa kwa madhumuni ya kudhibiti umiliki wa silaha na risasi nchini ambazo zinamilikiwa na makampuni yanayotoa ulinzi binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mgawanyo na mpangilio wa Muswada. Muswada huu umegawanyika katika sehemu tisa kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza, inapendekeza masharti ya utangulizi ambayo yanajumuisha jina la sheria na tafsiri ya maneno mbalimbali yanayotumika ndani ya Muswada huu.

Sehemu ya Pili, inahusu mashatri ya kiutawala ambapo Inspekta Jenerali wa Polisi anakuwa ndiye Mratibu wa Kitaifa katika masuala ya utekelezaji wa sheria hii. Inspekta Jenerali wa Polisi kwa kushirikiana na mamlaka husika Tanzania Zanzibar atamteua Katibu wa Kamati kutoka miongoni mwa Maafisa Waandamizi wa Jeshi la Polisi. Sehemu hii pia inapendekeza kuwa Mratibu wa Kitaifa ndiye atakayekuwa kitovu cha mawasiliano nchini. Aidha, sehemu hii inatoa masharti ya uteuzi wa Msajili wa silaha na risasi, kazi zake, masharti ya kuanzisha Kamati ya Usimamizi na Uteketezaji wa Silaha.

Sehemu ya Tatu, inapendekeza masharti ya leseni ya kumiliki silaha na risasi. Katika sehemu hii inaelezwa kwamba, mtu yeyote hatapewa kibali cha kumiliki silaha au risasi isipokuwa kama amepata kibali au ruhusa kutoka kwa Msajili. Sifa za umilikaji wa leseni inamtaka mwombaji kufanya majaribio na mafunzo ya uwezo katika asasi za Serikali zilizothibitishwa. Aidha, sehemu hii inaeleza kwamba Kamishna wa Polisi wa Zanzibar atakuwa Msajili chini ya sheria hii.

Sehemu ya Nne, inahusu masharti ya utoaji vibali vya uuzaji, utengenezaji na uhunzi wa silaha. Katika sehemu hii imeelezwa kwamba Msajili atatoa kibali cha uuzaji baada ya kushauriana na kuthibitishwa na Bodi ya Ushauri na Udhibiti wa Silaha. Aidha, Muswada unatoa masharti ya kuzuia utengenezaji wa silaha na risasi. Hivyo, hakuna mtu atakayeruhusiwa kutengeneza au kuunda silaha au risasi bila kutimiza vigezo na masharti yatakayotolewa na Bodi.

Muswada pia unaainisha kuwa kibali cha uhunzi wa silaha na kibali cha udalali ni lazima vithibitishwe na Bodi ya Ushauri ya Udhibiti wa Silaha. Sehemu hii pia, inaeleza kuwa, pale mmiliki wa silaha anapofariki dunia, au silaha ikiokotwa na ikiwa mwenye silaha hafahamiki au hakupatikana, silaha hiyo itawasilishwa Kituo cha Polisi kwa namna itakavyoelezwa na Msajili.

Sehemu ya Tano, inapendekeza masharti ya uingizaji wa silaha na risasi ndani ya nchi, uuzaji silaha nje ya nchi, usafirishaji na upitishaji wa silaha na risasi. Inapendekezwa kwamba silaha au risasi hazitasafirishwa bila ya kuwa na kibali cha kuagiza au kuingiza nchini, kusafirisha nje au kupitisha silaha ndani ya nchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita, inapendekeza kuhusu upekuzi na uzuiaji wa silaha au risasi ambapo wakati wa kutekeleza majukumu yake ya kazi, Afisa yeyote Muidhinishwa anaweza wakati wowote kumsimamisha mtu yeyote, chombo, gari, ndege au kuingia eneo lolote na kufanya upekuzi.

Sehemu ya Saba, inahusu masharti ya uteketezaji wa silaha na risasi.

Sehemu ya Nane, inaeleza masharti mbalimbali. Sehemu hii inatoa masharti kuhusu Masijala ya Silaha ambayo Makao yake Makuu yatakuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi na Masijala Ndogo itakuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Zanzibar. Inaendelea kuelezwa

kwamba Masjala Kuu itakuwa chini ya uangalizi wa Inspekta Jenerali wa Polisi au Afisa mwingine atakayechaguliwa na Waziri. Aidha, adhabu na makosa mbalimbali yameainishwa chini ya sehemu hii. Aidha, utunzaji salama wa silaha na risasi pia umeainishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa imeweka masharti ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Serikali za Mitaa kwa kurekebisha kifungu cha 7(1).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutungwa na kuanza kutumika kwa Sheria hii ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi kutakuwa na matokeo chanya kama ifuatavyo:-

(1) Kuimarika kwa ushirikiano na Asasi Zisizo za Kiserikali zinazojishughulisha na udhibiti wa uzagaaji wa silaha;

(2) Kuwatambua wamiliki wa silaha na idadi ya silaha wanazomiliki;

(3) Kuanzisha utaratibu wa utoaji wa mafunzo ya matumizi ya silaha kwa raia;

(4) Kuwepo kwa udhibiti wa uingizaji na uuzaji wa silaha bandia *(toy pistols);*

(5) Kuanzishwa kwa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa silaha;

(6) Kuwepo kwa umri wa kuanzia na ukomo wa kumiliki silaha; na

(7) Kutambuliwa kwa wamiliki wa silaha zinazotengenezwa kienyeji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kwanza nianze kuwashukuru Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Ulizi na Usalama kwa kutuelekeza na kushiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Muswada huu. Pili, wadau katika eneo hili walitusaidia na walikuja na mawazo ambayo mengi yalitusaidia katika kuandaa na kukamilisha.

Mwisho, siyo kwa umuhimu, ni Ofisi ya *AG* na watu wake ambao wameshiriki kikamilifu na kutuelekeza kisheria katika kuandaa Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, endapo Bunge lako Tukufu litapitisha Muswada huu kuwa sheria na Rais kuridhia, sheria hii inapendekezwa ianze kutumika tarehe 1 Julai, 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. SAADA MKUYA SALUM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mwenyekiti Kamati ya Ulinzi na Usalama au mwakilishi wake, Mheshimiwa Chiligati!

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SILAHA NA RISASI WA MWAKA 2014 (THE FIREARMS AND AMMUNITION CONTROL ACT, 2014) KAMA YALIVYOSOMWA BUNGENI**

**MHE. CAPT. (MST) JOHN Z. CHILIGATI- (K.n.y. MHE. ANNA M. ABDALLAH - MWENYEKITI WA KAMATI YA BUNGE YA ULINZI NA USALAMA):** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama na kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, kifungu 86(5), Toleo la 2013, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi, 2014 *(The Firearms and Ammunition Control Act, 2014)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa Kamati inampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Mathias Chikawe, Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Pereira Ame Silima, pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Ndugu Mbarak Abduwakil na Naibu Katibu Mkuu Ndugu Mwamin Malemi. Vile vile Wakuu wa Idara na wataalam wa silaha kutoka Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano walioutoa kwa Kamati yetu katika kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati pia inawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na wale ambao walituma michango yao kwa maandishi, maoni na ushauri wao umesaidia Kamati yetu katika kuboresha Muswada huu. Kamati kwa namna ya pekee inapenda kutoa shukrani kwa wadau wafuatao:-

*Tanzania Security Industry Association, Tanzania Hunting Operators,* Tanzania *Professional Hunters Association, Tanganyika Arms Limited, Wizara ya Ulinzi na JKT na Legal and Human Rights Centre* kwa kutoa maoni na ushauri uliosaidia kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Madhumuni ya Muswada; Kamati ilielezwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Silaha na Risasi (*The Arms and Ammunition Act),* Sura ya 223) kwa lengo la kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha na risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati ilielezwa kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuziba upungufu uliopo katika sheria ya sasa hasa katika maeneo ya kutoonesha ukomo wa umri wa kumiliki silaha, kutoainishwa vema silaha zinazoweza kumilikiwa na raia *(small arms and light weapons),* kuziba mianya ya kuingiza silaha bandia *(toy guns),* kuwepo kwa Mamlaka mbili zinazotoa leseni za kumiliki silaha yaani Jeshi la Polisi na Serikali za Mitaa, kutokuwepo kwa mafunzo mahususi kwa wamiliki wa silaha, kutokuwepo kwa kifungu kinachosimamia makampuni binafsi yanayomiliki silaha, kutobainishwa kwa utaratibu wa kuweka alama ya utambuzi kwenye silaha, hasa kwa kuzingatia kuwa nchi yetu imeridhia na kusaini Mikataba ya Kimataifa na ya Kikanda ambayo inazitaka nchi wanachama kuziwekea alama ya utambuzi silaha ndogo ndogo na nyepesi.

Vilevile Muswada huu unalenga kuzingatia masuala muhimu ambayo mtoa hoja amekwishayafafanua wakati akiwasilisha hoja yake hivi punde.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchambuzi wa Muswada; tarehe 16 Januari, mwaka huu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kuchambua maudhui ya Muswada. Baada ya kupokea maelezo ya Waziri, Kamati ilialika wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, ili kupata maoni yao kuhusu Muswada huu.

Hata hivyo, wadau waliieleza Kamati kuwa hawakushirikishwa kabla na wakati wa utungwaji wa Muswada huu. Hivyo Kamati iliamua kuahirisha kuendelea kujadili Muswada huu na kuielekeza Wizara kwenda kufanya mazungumzo na wadau, kama njia ya kuwashirikisha katika mchakato wa kutunga Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilikutana tena na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 5 Machi, mwaka huu, ambapo aliieleza Kamati kuwa Wizara ilifanya Kikao na wadau wa silaha na kukubaliana juu ya maudhui ya Muswada huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo ya Waziri, Kamati iliuchambua Muswada huu ikizingatia pia maoni ya wadau mbalimbali yaliyohusu mapendekezo ya kuboresha Muswada. Uchambuzi wa Kamati kuhusu maoni ya wadau pamoja na kupitia kifungu kwa kifungu, kuliiwezesha Kamati kutoa mapendekezo ambayo yanaonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Maoni na Ushauri wa Kamati; Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Tisa ambazo Kamati imezichambua Kifungu kwa Kifungu. Baada ya mashauriano baina ya Kamati, Serikali na wadau kuhusu vifungu mbalimbali ambavyo vilionekana kuwa na mkanganyiko, utata ama kutoeleweka vizuri, Serikali imeweza kuzingatia kwa kiasi kikubwa maoni yaliyotolewa na Kamati kuhusu maboresho ya vifungu husika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu sehemu mbalimbali za Muswada:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Kwanza; Sehemu hii ina ibara tatu zinazobainisha masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la sheria, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya sheria. Kwamba Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa silaha zote isipokuwa silaha kubwa za Kijeshi. Vile vile Waziri baada ya kushauriana na mamlaka husika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anaweza kwa tangazo litakalochapishwa katika Gazeti la Serikali kusamehe aina ya silaha au risasi kutoka katika matumizi ya Sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati baada ya kupitia ibara hizi imeona kwamba sehemu hii inajitosheleza na ilikubaliana na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu maboresho ya sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Pili, sehemu hii ina ibara ya (4) hadi ya (9), inabainisha masharti ya kiutawala na kwamba Inspekta Jenerali wa Polisi atakuwa ndiye Mratibu wa Kitaifa katika masuala ya utekelezaji wa sheria hii na pia atakuwa Afisa Mahusiano kati ya Jamhuri ya Muungano na Mataifa mengine kuhusiana na masuala yote ya utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa kuhusiana na udhibiti wa silaha na risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vifungu vya (5) na (6) vya Muswada vinahusu Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha. Ibara ya (6) inataja Wajumbe wanaounda Kamati hii. Katika eneo hili, kulitolewa hoja mbalimbali na wadau kuhusu aina na idadi ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha. Hoja kubwa ya wadau ilikuwa kwamba Kamati hii imewatenga wadau na kujumuisha wajumbe kutoka Idara za Serikali tu. Serikali imeikubali hoja hii kwa kuongeza wajumbe kutoka sekta binafsi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati imeridhika na marekebisho yaliyopendezwa na Serikali ya kuongeza idadi ya Wajumbe wa Kamati hii ili iwe na uwakilishi mpana wa wajumbe kutoka sekta binafsi badala ya kuifanya Kamati hii kuwa ya Kiserikali zaidi.

Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, kiongezwe kifungu kitakachoweka sharti la kwamba, mjumbe yeyote atakayeteuliwa kwenye Kamati hii ni lazima awe raia wa Tanzania na kisomeke kama ifuatavyo:-

*"Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika Ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati endapo ni raia wa Jamhuri ya Muungano"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Ibara ya (9) ya Muswada inaeleza uanzishwaji wa Masijala Kuu ya Silaha. Kamati inaunga mkono pendekezo hili kwa kuwa itakuwa rahisi pindi silaha ikikamatwa mmiliki aweze kutambuliwa mara moja. Vile vile kutokana na wimbi la uhalifu na kuzagaa kwa silaha haramu, wanachama wa Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki wana mpango madhubuti wa kukabiliana na tatizo hili la kuzagaa kwa silaha haramu. Hivyo, ili kukabiliana na tatizo hili nchi wanachama zimekubaliana kuwa na mfumo wa kisheria wa kutunga sheria ili kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha zinazomilikishwa kwa wananchi ili zisiangukie mikononi mwa wahalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tatu, sehemu hii yenye Ibara ya 10 hadi ya 31 inahusu masharti ya kupata leseni au kibali cha kumiliki silaha na risasi. Sehemu hii imebainisha kuwa mtu hatamiliki silaha isipokuwa kama amepata mafunzo ya kutumia silaha na pia kama amepata leseni au kibali cha kumiliki silaha chini ya Sheria hii. Sifa na masharti ya kumiliki silaha pia zimeorodheshwa katika sehemu hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeona kuwa hatua hii ni nzuri kwa kuwa itasaidia katika kupunguza tatizo la umiliki holela wa silaha na uhalifu na silaha zilizozagaa mitaani kwa kuwa itawezesha watu wenye vibali ndiyo wamiliki silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 11 kinaweka masharti ya mtu kupewa leseni ya kumiliki silaha likiwemo sharti la umri, kwamba umri wa mtu kupewa leseni ya kumiliki silaha ni kuanzia miaka 25. Aidha, Ibara ya 26 inaweka masharti ya mtu kuzuiwa kumiliki silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 19 kinatoa masharti kuwa silaha zote ndogo na silaha nyepesi zitawekwa alama ya utambuzi wa Kitaifa. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu kwa masharti haya kuwepo na kwamba zoezi hili litiliwe mkazo baada ya Sheria hii kupitishwa ili silaha zote nchini ziwe zimewekwa alama kama inavyoelekezwa katika Sheria hii. Hivyo, litakuwa kosa kubwa la jinai kwa kumiliki silaha bila ya kuisajili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 20 kinahusu kumiliki silaha kinyume na sheria. Kifungu cha 20(2) kinatoa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja kwa mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la kumiliki silaha kinyume cha sheria.

Kamati ina maoni kwamba kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu wa kutumia silaha, adhabu hii isiwe na mbadala wa faini, bali iwe ni kifungo tu cha miaka mitano kwa mtu aliyetiwa hatiani, ili kukomesha vitendo hivi. Hivyo, Kamati inapendekeza kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kisomeke kama ifuatavyo:-

*"Mtu aliyekiuka kifungu hiki anatenda kosa na iwapo atatiwa hatiani atawajibika kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26 kinabainisha watu wasio na sifa za kumiliki silaha. Kamati inapendekeza kwamba, mtu asiyetimiza umri wa miaka 25 iwe ni moja ya mambo yatakayomzuia mtu huyo kupata leseni ya kumiliki silaha. Hivyo, kiongezwe kifungu (g) na kisomeke kama ifuatavyo:-

"*Mtu mwenye umri chini ya miaka 25*"

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nne. Sehemu hii ina ibara ya 32 hadi ibara ya 44. Ibara hizi zinahusu leseni na vibali vya wahunzi, masharti ya utoaji vibali vya uuzaji na utengenezaji wa silaha. Sehemu hii inaeleza kuwa Msajili hatatoa kibali cha uuzaji wa silaha na risasi isipokuwa kama ameshauriana na kupata ridhaa ya bodi ya ushauri ya udhibiti wa silaha. Vile vile mtu hataruhusiwa kutengeneza au kuunda silaha au risasi bila kutimiza vigezo na masharti yaliyotolewa na Bodi chini ya sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati imeridhika na maudhui ya vifungu hivi katika sehemu hii kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tano. Sehemu hii ina ibara ya 45 hadi ibara ya 52. Ibara hizi zinakataza uingizaji na upitishaji nchini wa silaha au risasi bila kuwa na kibali. Vile vile sehemu hii inapendekeza masharti ya uingizaji wa silaha na risasi ndani ya nchi, uuzaji silaha nje ya nchi na upitishaji wa silaha na risasi nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu hii ni muhimu kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uingizaji wa silaha haramu nchini hasa kutoka nchi jirani zenye migogoro, hivyo hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la uingizaji holela wa silaha nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Sita. Sehemu hii ina ibara 53 hadi 54 na inahusu upekuzi wa vyombo vya usafiri ambapo Muswada umeelekeza kuwa Afisa yeyote Aliyeidhinishwa *(an Authorized Office)* wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi, anaweza wakati wowote, yakiwepo mazingira ya kutia shaka, kumsimamisha mtu yeyote au chombo chochote cha usafirishaji au kuingia kwenye eneo lolote na kufanya upekuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, baadhi ya wadau walitoa maoni kwamba madaraka haya ya upekuzi, Mwenyekiti naomba *Hansard paragraph* hii waifanyie masahihisho.

Hoja ya wadau ilikuwa kwamba madaraka haya ni makubwa sana na yanaweza yakatumiwa vibaya, lakini maoni ya Kamati ni kwamba, madaraka haya ni muhimu yawepo ili kupambana na tatizo hili la uingiaji holela wa silaha na risasi. Naomba *Hansard* ichukue haya niliyoyasema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Saba. Sehemu hii ina ibara 55 hadi 57, na inahusu kuhifadhi silaha au risasi pale mmiliki wa silaha anapofariki au kampuni yenye kumiliki silaha inapofilisika. Vile vile inahusu utaifishaji wa silaha zinazohusiana na makosa na utaifishaji wa silaha au risasi zisizokuwa na mmiliki. Kamati inasisitiza kwamba, silaha hizi pindi zitakapotaifishwa ziteketezwe mara moja kama sheria inavyoelekeza ili zisiangukie mikononi mwa watu wasio waaminifu na kuzirudisha mitaani ili ziendelee kufanya uhalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Nane. Sehemu hii ina ibara za 58 hadi 72 zinazohusu ofisi ya Masjala Kuu ya Silaha kuwa iwe Makao Makuu ya Polisi Dar es Salaam na iwepo Ofisi Ndogo ya Masjala itakayokuwa kule Zanzibar. Masjala Kuu itakuwa chini ya usimamizi wa Mkuu wa Jeshi la Polisi *(IGP)* na kwamba Kamishna wa Polisi, Zanzibar atakuwa Msimamizi Msaidizi wa Masjala Ndogo ya Zanzibar. Aidha, vifungu hivi vinaweka masharti ya utoaji wa taarifa ya

upotevu wa silaha, kutoa msamaha kwa mtu atakayejisalimisha kama atapatikana anamiliki silaha au risasi kinyume cha sheria.

Kamati imeridhika na maudhui ya vifungu hivi katika sehemu hii. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba kifungu cha 62(2) kifanyiwe marekebisho ya adhabu ya kifungo cha mtu anayepatikana na hatia. Kifungo kiongezwe kiwe cha mwaka mmoja badala ya miezi miwili iliyopendekezwa kwenye Muswada ili kifungo kiendane na faini inayopendekezwa ambayo ni shilingi milioni tano au zaidi. Hivyo basi, kifungu kisomeke kama ifuatavyo;

*"Any person who contravenes subsection one commits an offence and is reliable for on conviction to a fine not less than five million Shillings or to imprisonment for a term not exceeding one year or both."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Sehemu ya Tisa. sehemu hii ina ibara ya 73 na 74 na inahusu masharti ya kufanya marekebisho katika Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa kwa kurekebisha kifungu cha 7(1). Kamati inaunga mkono mapendekezo ya ibara hii kwa kuwa mamlaka ya usajili wa silaha sasa itakuwa moja tu hapa nchini baada ya sheria hii kuondoa madaraka ya Halmashauri za Wilaya kusajili na kutoza ushuru bunduki aina ya magobore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao Bunge lako Tukufu likiupitisha kuwa sheria utasaidia kupunguza tatizo la kuzagaa kwa silaha haramu mitaani. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Kudumu ya Ulinzi na Usalama imeuchambua Muswada huu kwa kina na kuuboresha na kwamba jedwali la marekebisho lililo mbele ya Bunge lako ni matokeo ya uchambuzi wa Kamati na wadau waliohusika kuujadili Muswada huu. Kwa hiyo, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu liujadili na kuuboresha zaidi Muswada huu na hatimaye upitishwe kuwa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati, napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mheshimiwa Mathias Chikawe na Mheshimiwa Pereira Silima kwa namna walivyoshirikiana vizuri na Kamati yangu katika kuuboresha Muswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru wataalam wa silaha kutoka Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao ulioiwezesha Kamati kuchambua Muswada huu hadi hatua hii tulipofikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vile vile napenda kwa mara nyingine kuwashukuru wadau kwa kutoa maoni yaliyosaidia kuboresha Muswada huu. Aidha, kipekee nawashukuru wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara na ushauri uliofanikisha kuwasilishwa kwa maoni haya mbele ya Bunge lako Tukufu. Wajumbe wameorodheshwa pale kwa kuokoa muda sitawasoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashilillah, Mkurugenzi wa Kamati, Ndugu Charles Mloka, Wakurugenzi Wasaidizi wa Kamati Ndugu Ruhilabake, Ndugu Ng'wavi na Ndugu Athumani Hussein, Makatibu wa Kamati Ndugu Nesta Kawamala na Ndugu Onesmo Laulau na ndugu na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi maoni haya kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inaunga mkono Muswada huu na naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MAONI YA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SILAHA NA RISASI WA MWAKA 2014 (THE FIREARMS AND AMMUNITION CONTROL ACT, 2014) KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI**

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kutoa maoni na ushauri wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi wa Mwaka 2014 ( The Firearms and Ammunition Control Act, 2014).

**Mheshimiwa Spika,** kwanza kabisa Kamati inampongeza Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mheshimiwa Mathias M. Chikawe, (Mb), Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi Mhe. Pereira Ame Silima, (Mb); pamoja na Katibu Mkuu Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi Ndg. Mbarak M. Abduwakil na Naibu Katibu Mkuu Ndg. Mwamin J. Malemi, Wakuu wa Idara na wataalamu wa silaha kutoka Jeshi la Polisi pamoja na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ushirikiano kwa Kamati uliowezesha kuboresha muswada huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia inawashukuru wadau wote waliofika mbele ya Kamati na wale ambao walituma michango yao kwa maadishi, maoni na ushauri wao umesaidia Kamati katika kuboresha Muswada huu. Kamati kwa namna ya pekee inapenda kutoa shukrani kwa wadau wafuatao:- Tanzania Security Industry Association, Tanzania Hunting Operators, Tanzania Professional Hunters Association, Tanganyika Arms Ltd, Wizara ya Ulinzi na JKT, na Legal and Human Rights Centre kwa kutoa maoni na ushauri uliosaidia kuboresha Muswada huu.

## 2. 0 MADHUMUNI YA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilielezwa na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi kuwa Muswada huu unakusudia kufuta Sheria ya Silaha na Risasi (The Arms and Ammunition Act, Sura ya 223) kwa lengo la kutunga Sheria mpya kwa ajili ya kusimamia na kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha na risasi.

Aidha, Kamati ilielezwa kuwa madhumuni ya Muswada huu ni kuziba upungufu uliopo katika sheria ya sasa hasa katika maeneo ya:- kutoonyeshwa kikomo cha umri wa kumiliki silaha, kutoainishwa vema silaha zinazoweza kumilikiwa na raia( small arms and light weapons), kuziba mianya ya kuingiza silaha bandia(toy guns),kuwepo kwa Mamlaka mbili zinazotoa leseni za kumiliki silaha yaani Jeshi la Polisi na Serikali za Mitaa, kutokuwepo kwa mafunzo mahususi kwa wamiliki wa silaha, kutokuwepo kwa kifungu kinachosimamia makampuni binafsi yanayomiliki silaha, kutobainishwa kwa utaratibu wa kuweka alama ya utambuzi kwenye silaha, hasa kwa kuzingatia kuwa nchi yetu imeridhia na kusaini Mikataba ya Kimataifa na ya kikanda ambayo inazitaka nchi wanachama kuziwekea alama ya utambuzi silaha ndogo ndogo na nyepesi. Vilevile Muswada huu unalenga kuzingatia masuala muhimu ambayo mtoa hoja amekwisha yafafanua wakati akiwasilisha hoja yake mapema leo hii.

## 3.0 UCHAMBUZI WA MUSWADA

**Mheshimiwa Spika,** Tarehe 16 Januari, 2015 Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi aliwasilisha Muswada huu mbele ya Kamati kwa mara ya kwanza kwa ajili ya kuchambua maudhui ya Muswada. Baada ya kupokea maelezo ya Waziri, Kamati ilialika wadau kwa mujibu wa Kanuni ya 84(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la

2013 ili kupata maoni yao kuhusu Muswada huu. Hata hivyo, wadau waliieleza Kamati kuwa hawakushirishwa kabla na wakati wa utungwaji wa Muswada huu. Hivyo Kamati iliamua kuahirisha kuendelea kujadili Muswada huu na kuielekeza Wizara kwenda kufanya mazungumzo na wadau, kama njia ya kuwashirikisha katika mchakato wa kutunga Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilikutana na Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi tarehe 5 Machi, 2015 ambapo aliileza Kamati kuwa Wizara ilifanya Kikao na wadau wa silaha na kukubaliana juu ya maudhui ya Muswada huo. Baada ya maelezo hayo ya Waziri, Kamati iliuchambua Muswada huu ikizingatia pia maoni ya wadau mbalimbali yaliyohusu mapendekezo ya kuboresha Muswada. Uchambuzi wa Kamati kuhusu maoni ya wadau pamoja na kupitia kifungu kwa kifungu, kuliiwezesha Kamati kutoa marekebisho ambayo yanaonekana kwenye Jedwali la marekebisho ya Serikali.

## 4.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI KUHUSU MUSWADA WA SHERIA YA USIMAMIZI NA UDHIBITI WA SILAHA NA RISASI

**Mheshimiwa Spika,** Muswada huu umegawanyika katika sehemu Tisa ambazo Kamati imezichambua Kifungu kwa Kifungu. Baada ya mashauriano baina ya Kamati, Serikali na wadau kuhusu vifungu mbalimbali ambavyo vilionekana kuwa na mkanganyiko, utata ama kutoeleweka vizuri, Serikali imeweza kuzingatia kwa kiasi kikubwa maoni yaliyotolewa na Kamati kuhusu maboresho ya vifungu husika.
**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni yafuatayo kuhusu sehemu mbalimbali ya Muswada huu kama ifuatavyo:-

### 4.1 Sehemu ya Kwanza

**Mheshimiwa Spika,** sehemu ya kwanza ina ibara 3 zinazobainisha masharti ya utangulizi yanayojumuisha jina la sheria, matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno mbalimbali yaliyotumika ndani ya sheria. Kwamba Sheria hii itatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa silaha zote isipokuwa silaha kubwa za Kijeshi. Vilevile Waziri baada ya kushauriana na mamlaka husika ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar anaweza kwa tangazo litakalochapishwa katika *Gazeti la Serikali* kusamehe aina ya silaha au risasi kutoka katika matumizi ya Sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati baada ya kupitia ibara hizi imeona kwamba sehemu hii inajitosheleza na ilikubaliana na ufafanuzi uliotolewa na Serikali kuhusu maboresho ya sehemu hii.

### 4.2 Sehemu ya Pili

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara ya 4 hadi ya 9 , inabainisha masharti ya kiutawala na kwamba Inspekta Jenerali wa Polisi atakuwa ndiye Mratibu wa Kitaifa katika masuala ya utekelezaji wa sheria hii, na pia atakuwa Afisa mahusiano kati ya Jamhuri ya Muungano na Mataifa mengine kuhusiana na masuala yote ya utekelezaji wa mpango kazi wa Taifa kuhusiana na udhibiti wa silaha na risasi.
**Mheshimiwa Spika,** vifungu vya 5 na 6 vya Muswada vinahusu Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha. Ibara ya 6 inataja Wajumbe wanaounda Kamati hii. katika eneo hili, kulitolewa hoja mbalimbali na wadau kuhusu aina na idadi ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha. Hoja kubwa ya wadau ilikuwa kwamba Kamati hii imewatenga wadau na kujumuisha wajumbe kutoka

Idara ya Serikali. Serikali imeikubali hoja hii kwa kuongeza wajumbe kutoka sekta binafsi.

Aidha, Kamati imeridhika na marekebisho yaliyopendezwa na Serikali ya kuongeza idadi ya Wajumbe wa Kamati ili iwe na uwakilishi mpana wa wajumbe kutoka sekta binafsi badala ya kuifanya Kamati hii kuwa ya kiserikali zaidi. Hata hivyo, Kamati inashauri kuwa kiongezwe kifungu kitakachoweka sharti la kwamba mtu yeyote atakayeteuliwa kwenye Kamati hii awe ni raia wa Tanzania na kisomeke:-

***"5( 3) Bila ya kuathiri masharti yaliyomo katika Ibara hii, mtu yeyote atakuwa na sifa za kuteuliwa kuwa Mjumbe wa Kamati endapo ni raia wa Jamhuri ya Muungano"***

**Mheshimiwa Spika,** katika Ibara ya 9 ya Muswada inaeleza uanzishwaji wa Masijala Kuu ya Silaha. Kamati inaunga mkono pendekezo hili kwa kuwa itakuwa rahisi pindi silaha ikikamatwa mmiliki aweze kutambuliwa mara moja. Vilevile Kutokana na wimbi la uhalifu na kuzagaa kwa silaha haramu, wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wana mpango madhubuti wa kukabiliana na tatizo hili la kuzagaa kwa silaha haramu. Hivyo, ili kukabiliana na tatizo hili nchi wanachama zimekubaliana kuwa na mfumo wa kisheria wa kutunga sheria ili kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha zinazomilikishwa kwa wananchi ili zisiangukie mikononi mwa wahalifu.

### 4.3 Sehemu ya Tatu

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii yenye Ibara ya 10 hadi ya 31 inahusu masharti ya kupata leseni au kibali cha kumiliki silaha na risasi. Sehemu hii imebainisha kuwa mtu hatamiliki silaha isipokuwa kama amepata mafunzo ya kutumia silaha na pia kama amepata leseni au kibali cha kumiliki silaha chini ya Sheria hii. Sifa na masharti ya kumiliki silaha pia zimeainishwa katika sehemu hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona kuwa hatua hii ni nzuri kwa kuwa itasaidia katika kupunguza tatizo la umiliki holela wa silaha na uhalifu na silaha zilizozagaa mitaani kwa kuwa itawezesha watu wenye vibali ndio wamiliki silaha. Kifungu cha 11 kinaweka masharti ya mtu kupewa leseni ya kumiliki silaha likiwemo sharti la umri, kwamba umri wa mtu kupewa leseni ya kumiliki silaha ni kuanzia miaka 25. Aidha, Ibara ya 26 inaweka masharti ya mtu kuzuiwa kumiliki silaha.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 19 kinatoa masharti kuwa silaha zote ndogo na silaha nyepesi zitawekwa alama ya utambuzi wa kitaifa. Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu kwa masharti haya kuwepo na kwamba zoezi hili litiliwe mkazo baada ya Sheria hii kupitishwa ili silaha zote nchini ziweze kuwekwa alama kama inavyoelekezwa katika Sheria hii.Hivyo litakuwa kosa kubwa la jinai kwa kumiliki silaha bila ya kuisajili.

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 20 kinahusu kumiliki silaha kinyume na sheria. Kifungu cha 20(2) kinatoa adhabu ya kulipa faini isiyozidi shilingi milioni kumi au kutumikia kifungo cha miaka mitano au vyote kwa pamoja kwa mtu anayetiwa hatiani kwa kosa la kumiliki silaha kinyume na sheria. Kamati ina maoni kwamba kwa kuwa kumekuwa na ongezeko kubwa la uhalifu wa kutumia silaha, adhabu hii isiwe na mbadala wa faini, bali iwe ni kifungo tu cha miaka mitano kwa mtu

anayetiwa hatiani, ili kukomesha vitendo hivi. Hivyo kamati inapendekeza kifungu hiki kifanyiwe marekebisho na kisomeke:-

***"20(2) Mtu aliyekiuka kifungu hiki anatenda kosa na iwapo atatiwa hatiani atawajibika kutumikia kifungo kwa kipindi kisichopungua miaka mitano."***

**Mheshimiwa Spika,** kifungu cha 26 kinabainisha watu wasio na sifa ya kumiliki silaha.Kamati inapendekeza kwamba mtu hasiyetimiza umri wa miaka 25 iwe ni moja ya mambo yanayomzuia mtu huyo kupata leseni ya kumiliki silaha. Hivyo, kiongezwe kifungu (g) na kisomeke:-

***"26 (1) (g) Mtu mwenye umri chini ya miaka 25"***

### 4.4 Sehemu ya Nne

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara ya 32 hadi 44, Ibara hizi zinahusu leseni na vibali vya wahunzi, masharti ya utoaji vibali vya uuzaji na utengenezaji wa silaha.Sehemu hii inaeleza kuwa Msajili hatatoa kibali cha uuzaji isipokuwa kama ameshauriana na kupata ridhaa ya Bodi ya Ushauri na Udhibiti wa Silaha. Vilevile mtu hataruhusiwa kutengeneza au kuunda silaha au risasi bila kutimiza vigezo na masharti yatakayotolewa na Bodi ya sheria hii.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeridhika na maudhui ya vifungu katika sehemu hii kama yalivyowasilishwa.

### 4.5 Sehemu ya Tano

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara ya 45 hadi 52, vifungu hivi vinakataza uingizaji au upitishaji nchini wa silaha au risasi bila ya kuwa na kibali. Vilevile sehemu hii inapendekeza masharti ya uingizaji wa silaha na risasi ndani ya nchi, uuzaji silaha nje ya nchi na upitishaji wa silaha na risasi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ni muhimu kwa kuwa kumekuwa na tatizo la uingizaji wa silaha haramu nchini hasa kutoka nchi jirani zenye migogoro, hivyo hatua hii itasaidia kupunguza tatizo la uingizaji holela wa silaha nchini.

### 4.6 Sehemu ya Sita

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara za 53 hadi 54 na inahusu upekuzi wa vyombo vya usafiri ambapo Muswada unaelekeza kuwa afisa yeyote aliyeidhinishwa (an authorized Officer) wakati akitekeleza majukumu yake ya kazi anaweza wakati wowote yakiwepo mazingira ya kutia shaka kumsimamisha mtu yeyote au chombo chochote cha usafirishaji au kuingia eneo lolote na kufanya upekuzi.

Aidha, baadhi ya wadau walitoa maoni kwamba madaraka haya ya upekuzi yawe ya Jeshi la Polisi tu, na siyo yatumiwe pia na maafisa uhamiaji. Lakini Kamati inakubaliana na Serikali kwamba wakati umefika kwa maafisa uhamiaji wanapokuwa kwenye doria wawe na madaraka ya upekuzi ili kuongeza ufanisi katika mapambano dhidi ya uhamiaji haramu na uingizaji silaha nchini kinyume cha sheria.

### 4.7 Sehemu ya Saba

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara za 55 hadi 57 na zinahusu kuhifadhi silaha au risasi pale mmiliki wa silaha anapofariki, au kampuni yenye kumiliki silaha ikifilisika, utaifishaji wa silaha zinazohusiana na kosa, na utaifishaji wa silaha au risari zisizo kuwa na mmiliki. Kamati inasisitiza kwamba silaha hizi pindi zinapotaifishwa ziteketezwe mara moja kama sheria inavyoelekeza ili zisiangukie mikononi mwa watu wasio waaminifu na kuzirudisha mitaani kufanyia uhalifu.

### 4.8 Sehemu ya Nane

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina ibara za 58 hadi 72 zinazohusu Ofisi ya Masijala Kuu ya Silaha kuwa makao makuu ya Polisi Dar es salaam na Ofisi ndogo ya Masijala itakuwa Zanzibar. Masijala kuu itakuwa chini ya usimamizi wa mkuu wa Jeshi la Polisi( IGP) na kwamba Kamishna wa Polisi Zanzibar atakuwa msimamizi msaidizi wa masijala ndogo ya Zanzibar. Aidha, vifungu hivi vinaweka masharti ya utoaji wa taarifa ya upotevu wa silaha, kutoa msamaha kwa mtu atakayejisalimisha kama atapatikana anamiliki silaha au risasi kinyume cha sheria.

Kamati imeridhika na maudhui ya vifungu katika sehemu hii. Hata hivyo Kamati inashauri kuwa kifungu cha 62(2) kifanyiwe marekebisho ya adhabu ya kifungo kwa mtu anayepatikana na hatia, iongezwe iwe mwaka mmoja badala ya miezi miwili iliyopendekezwa kwenye Muswada ili kifungo kiendane na faini inayopendekezwa ambayo ni shilingi milioni tano au zaidi. Hivyo basi kifungu kisomeke:-

*"62(2) Any person who contravenes subsection (1)commits an offence and is liable on conviction to a fine not less than five million Shillings or to imprisonment for a term not **exceeding one year** or to both"*

### 4.9 Sehemu ya Tisa

**Mheshimiwa Spika,** sehemu hii ina Ibara ya 73 na 74 inahusu masharti ya kufanya marekebisho katika Sheria ya fedha ya Serikali za Mitaa kwa kurekebisha kifungu cha 7(1). Kamati inaunga mkono mapendekezo ya Ibara hii kwa kuwa mamlaka ya usajili wa silaha itakuwa moja tu hapa nchini baada ya sheria hii kuondoa madaraka ya halmashauri za Wilaya kusajili na kutoza ushuru bunduki aina ya magoboli.

## 5.0 HITIMISHO

**6.1** **Mheshimiwa Spika,** Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao Bunge lako tukufu likiupitisha kuwa sheria utasaidia kupunguza tatizo la kuzagaa kwa silaha haramu mitaani. Aidha, napenda kulihakikishia Bunge lako kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama imeuchambua Muswada huu kwa kina na kuuboresha; na kwamba Jedwali la marekebisho lililo mbele ya Bunge lako tukufu ni matokeo ya uchambuzi wa Kamati, na wadau waliohusika kuujadili Muswada huu. Kwahiyo, Kamati inaliomba Bunge lako tukufu liujadili na kuuboresha zaidi Muswada huu na hatimaye upitishwe kuwa sheria.

### 6.2 Shukrani

**Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati napenda kutoa shukrani za dhati kwa Mhe. Mathias M.Chikawe, Mb na Mhe. Pereira A.Silima, Mb kwa namna walivyoshirikiana vizuri na Kamati yangu katika kuuboresha Muswada huu. Aidha, napenda kuwashukuru wataalamu wa silaha kutoka Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa maoni na ushauri wao uliowezesha Kamati kuchambua Muswada hadi hatua hii.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile napenda kwa mara nyingine kuwashukuru wadau kwa kutoa maoni yaliyosaidia kuboresha Muswada huu. Aidha kipekee nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa maoni, busara na ushauri uliofanikisha kuwasilishwa kwa maoni haya mbele ya Bunge lako tukufu. Naomba niwatambue Wajumbe hao wa Kamati kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Anna M. Abdallah, Mb - Mwenyekiti
2. Mhe. Dr. Mohamed S. Khatibu, Mb - M/Mwenyekiti
3. Mhe. Brig. Jen (Mst) Hassan Ngwilizi, Mb - Mjumbe
4. Mhe. Kapt. (Mst) John Z. Chiligati, Mb - Mjumbe
5. Mhe. Mariam Mfaki, Mb - Mjumbe
6. Mhe. Dkt. Agustine L. Mrema, Mb - Mjumbe
7. Mhe. Cynthia Hilda Ngoye, Mb - Mjumbe
8. Mhe. Dr. Donald M. Malole, Mb - Mjumbe
9. Mhe. Eng. Stella Manyanya, Mb - Mjumbe
10. Mhe. Vita R. Kawawa, Mb - Mjumbe
11. Mhe. Musa H. Musa, Mb - Mjumbe
12. Mhe. Rachel R. Mashishanga, Mb - Mjumbe
13. Mhe. Hamad Ali Hamadi, Mb - Mjumbe
14. Mhe. Masoud Abdallah Salim, Mb - Mjumbe
15. Mhe. Vincent Nyerere, Mb - Mjumbe

**Mheshimiwa Spika,** napenda pia kuchukua fursa hii kumshukuru Katibu wa Bunge Dkt. Thomas Kashililah, Mkurugenzi wa Kamati Ndg. Charles Mloka, Wakurugenzi wasaidizi wa Kamati Ndg. Theonest Ruhilabake, Ndg. Angumbwike Ngw'avi na Ndg. Athuman Hussein, makatibu Kamati Ndg. Nesta Kawamala na Ndg. Onesmo Laulau na watumishi wote wa Bunge kwa kuisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake kwa kuratibu vyema kazi za Kamati hadi maoni haya kuletwa mbele ya Bunge lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,** Naunga mkono Muswada na naomba kuwasilisha.

**Anna M. Abdallah, (Mb)**
**MWENYEKITI**
**Kamati ya Ulinzi na Usalama**
**19 Machi, 2015**

**MWENYEKITI:** Sasa namwita Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani Bungeni ambaye ni Waziri Kivuli wa Wizara hii, Mheshimiwa Godbless Lema!

**MHE. GODBLES D. LEMA (MSEMAJI MKUU WA KAMBI YA UPINZANI BUNGENI):** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha Bungeni maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi, 2014 *(The Firearms and Ammunition Control Act, 2014)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, namshukuru sana Mwenyezi Mungu, familia yangu na viongozi wangu wa Chama na wanachi wa Jimbo langu. Nawashukuru pia maadui zangu kwa dhati kwani uadui wao, hila zao na mbinu zao chafu dhidi yangu zimeendelea kuimarisha imani yangu na tumaini langu siku hadi siku katika vita hii muhimu tunayoipigania ya kulikomba Taifa hili. *(Makofi)*

Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi unaletwa katika Bunge lako Tukufu wakati ambapo nchi katika mtaziko mkubwa ambapo matukio ya ujambazi wa kutumia silaha yamekithiri, mauaji ya raia kwa kutumia silaha za moto yameongezeka, matukio yenye sura ya ugaidi ya utekaji na utesaji yameshuhudiwa hapa nchini, matukio ya uvamizi na uporaji wa silaha katika Vituo vya Polisi yanashamiri na uhamiaji haramu umekuwa ukiongezeka pia kwa kasi hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli usiopingika kwamba matukio yote haya yametokea huku kukiwa na Sheria ya Usimamizi wa Silaha na Risasi ambayo itafutwa na Muswada huu kama utapitishwa na Bunge lako. Hii ni dhahiri kwamba, tatizo kubwa la nchi hii si sheria na matumizi yake bali ni uongozi uliokosa fikra chanya na utu katika kutawala. Ndiyo maana leo Serikali inafikiri kupambana na janga la mauaji ya *albino* ni kuwatenga *albino* na jamii kutoka kwenye makazi yao ya kawaida wakati tatizo la msingi ni imani potofu iliyojengeka miongoni mwa jamii. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba huwezi kuipinga imani kwa kutumia silaha isipokuwa kwa habari njema na imani inayojali utu kuwafikia watu wote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na nia njema ya Serikali ya kuleta Muswada huu Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kwamba kama Serikali itajali utu, usawa, haki na demokrasia ya kweli, pengine kusingekuwa na hofu ya matumizi mabaya ya silaha miongoni mwa wananchi na hivyo kusingekuwa na haja ya kuleta sheria ya kudhibiti silaha na kuweka masharti magumu kwa wananchi kumiliki silaha hasa kipindi hiki ambapo kumekuwa na matukio mengi ya kigaidi, ya uvamizi, utekaji na utesaji ambapo kimsingi wananchi wanahitaji ulinzi wa Serikali na ulinzi binafsi kuliko wakati mwingine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa linaelekea kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ifikapo oktoba mwaka huu wa 2015. Matumizi ya sheria ya kulinda amani nchini ni muhimu sana wakati huu lakini mambo muhimu na ya msingi yakipuuzwa amani inaweza kutoweka licha ya sheria ngumu za udhibiti ikiwemo udhibiti wa silaha kuwepo. Masuala hayo ni kama ifuatavyo:-

Moja, kucheza na haki ya wananchi kujiandikisha kuwa mpiga kura. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza kwamba, mzaha katika jambo hili hautavumilika. Aidha, ijulikane kwamba wananchi watakapotambua kuwa hawawezi kuwapata viongozi wao wanaowataka kupitia sanduku la kura basi wanaweza kutafuta haki yao kwa njia nyingine, hali ambayo inaweza kuliingiza Taifa katika machafuko kwani haki haiombwi ila inadaiwa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa wito kwa wananchi wote kujitokeza kwa wingi kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapiga kura ili waweze kuamua nani atakuwa kiongozi wao kwenye uchaguzi mkuu unaokuja.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inamkumbusha kila mwananchi atambue kwamba kura yako ni maisha yako, nenda kajiandikishe sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pili, kufanya mzaha na uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaonya Serikali kutokufanya mzaha na jambo hili kwani inaweza kuiingiza nchi katika machafuko makubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wa nchi hii wamekuwa wakifanya mizaha kuhusu maisha ya wananchi kwa mambo mengi yakiwemo ufisadi uliokithiri. Kwa mfano, Mheshimiwa Spika aliwahi kumuomba Mheshimiwa Andrew Chenge kutoa mwongozo au kutengeneza maazimio ya Bunge kuhusu watuhumiwa wa wizi wa fedha za *Escrow* wakati yeye mwenye alikuwa ni mutuhumiwa. Huu ni mzaha mkubwa ambao tafsiri yake inaonesha kwamba watawala wanawaona Watanzania kuwa ni wajinga. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaonya kuwa mizaha kama hii ikiletwa kwenye suala la uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi, Taifa hili linaweza likasambaratika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Tume Huru ya Uchaguzi si kwa sababu inataka kushinda uchaguzi bali ni kwa sababu inataka kujenga na kulinda imani ya mpiga kura ili kulinda amani ya nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, matumizi ya kisiasa ya Jeshi la Polisi. Kwa vile imethibitika pasipo shaka yoyote kwamba Polisi mkatili na mkorofi dhidi ya upinzani anapandishwa cheo, ni dhahiri kwamba kitendo hiki kimejenga msingi *(presidency)* wa Polisi kuwaonea, kwadhalilisha na kuwafedhehesha viongozi wa upinzani kwa matarajio kwamba watapongezwa na kupandishwa vyeo na Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani imepiga kelele sana juu ya suala hili la matumizi mabaya ya Jeshi la Polisi kulinda maslahi ya kisiasa ya watawala kwa miaka yote. Viongozi, wanaharakati na wananchi wanaounga mkono mageuzi wamepita kwenye bonde la uvuli wa mauti kwa muda mrefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatukuonewa kwa sababu sisi ni wanyonge ila ni kwa sababu tumeendelea kuwa wavumilivu. Nina mashaka kama uvumilivu huo utaendelea kuwepo kama uonevu na ukandamizaji utaendelea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwenyezi Mungu pamoja na upole wake, ukarimu wake, upendo wake na rehema zake kwa watu wote lakini bado ametenda jehanamu kwa watenda dhambi ambao amewaumba yeye mwenyewe. Tusisubiri wananchi wacho ke kuvumilia bali hekima ya Mungu ituongoze ili kuepusha taifa hili na majanga ya uvunjifu wa amani pindi watu watakapokosa uvumilivu wa mateso. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ulinzi wa raia na mali zao; kukosekana kwa ulinzi na usalama wa raia na mali zao kunaweza kuliingiza Taifa katika machafuko. Matukio ya kuuawa kwa watu wenye ulemavu wa ngozi *(albino)*, mauaji ya vikongwe na wanawake kutokana na imani za kishirikina yamekithiri sana katika nchi yetu licha ya kuwa na vyombo vya ulinzi na usalama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali hii imefanya wananchi kukosa imani na Serikali kuwa bado yanaendelea licha ya kampeni nyingi kutoka kwa wanaharakati mbalimbali kupinga mauaji ya albino. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatahadharisha Serikali kutokudharau kundi la *albino* kuwa ni dogo na kutolipatia ulinzi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huu, sasa naomba nijielekeze kwenye Muswada wa sheria uliopo mbele yetu unaohusu usimamizi na udhibiti wa silaha na risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matukio yote niliyoyataja hivi punde ni matukio ambayo kwa kiasi kikubwa yamedhoofisha hali ya usalama hapa nchini, hivyo, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba muswada huu umekuja wakati muafaka kwa kuwa matukio yaliyotajwa hapo juu ambayo yamekuwa yakiongezeka hapa nchini ni matukio ambayo utekelezaji wake unahitaji silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa matukio hayo ni ya kihalifu ni dhahiri kwamba, hata silaha zinazotumika hazina uhalali, hivyo, sheria bora itakayoweka udhibiti na usimamizi wa matumizi ya silaha hapa nchini inaweza kufanikiwa kupunguza matukio ya uhalifu ikiwa itatungwa kwa nia njema ya kulinda usalama wa raia wote na si kwa lengo la kukandamiza kundi fulani la watu ili kukidhi matakwa ya kisiasa ya kundi la watu wachache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya ujumla; kabla sijaanza kuchambua vifungu vya Muswada huu naomba nitoe maoni ya jumla ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utekelezaji bora wa Muswada huu pindi utakapokuwa sheria kama ifuatavyo:-

Moja, Serikali iimarishe ulinzi wa raia na viongozi sambamba na matumizi ya Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi. Itakuwa haina maana sana kuweka Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi kama wananchi na viongozi watakuwa hawana ulinzi dhidi ya watu wanaotumia silaha kwa malengo ya kihalifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa ninapowasilisha maoni haya ya Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hawana ulinzi wa Serikali. Ni ajabu kwamba Mbunge ambaye kimsingi kazi zake zinamfanya awe na maadui ambao ni wahalifu na mafisadi anakuwa hana ulinzi wowote wa Serikali. Kwa mfano, maisha ya Mheshimiwa David Kafulila aliyeibua sakata la wizi wa *Escrow* na kusababisha Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Mawaziri kufukuzwa yako hatarini kwa kuwa hana ulinzi wowote, lakini Wakuu wa Wilaya ambao kazi zao ni kupokea Mwenge, kusoma taarifa za UKIMWI na njaa Wilayani na kupokea wageni wa Kitaifa wana ulinzi majumbani mwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge mtakumbuka tukio la kuvamiwa na kuchomewa nyumba kwa wabunge wenzetu. Wabunge hawa wangekuwa wamepatiwa ulinzi wa Polisi wenye silaha yamkini uvamizi ule ungeweza kuepukika.

Kwa mantiki hii Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka Serikali kuanzia sasa kutoa ulinzi kwenye nyumba za Wabunge na viongozi wengine wanaostahili huduma hiyo kama ambavyo Serikali ya Kenya imefanya kwa Wabunge na viongozi wake. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutokufanya ubaguzi wa kiulinzi kwa viongozi katika mihimili mitatu ya dola, yaani Serikali, Bunge pamoja na Mahakama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, Wabunge wote na viongozi wote wenye hadhi ya kidiplomasia *(diplomats)* wawe na sifa za moja kwa moja *(direct entitlement)* za kumiliki silaha kwa ajili ya kujilinda mara tu wanapopata hadhi ya kidiplomasia. Utaratibu wa kuwatambulisha kwa Msajili wa Silaha ili kupatiwa leseni ya umiliki wa silaha ufanyike na taasisi wanazozitumikia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo hapa ni kuepusha mlolongo mrefu wa kuwajadili viongozi walioaminiwa na wananchi walio wengi kama Rais na Wabunge au viongozi walioaminiwa kwa kiwango cha juu na Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kujadiliwa na ngazi za chini za uongozi katika vitongoji na mitaa kama ambavyo sheria ya sasa inavyoelekeza.

Kitendo cha kuruhusu viongozi wakuu walioaminika kujadiliwa na ngazi za chini kama wana sifa ama hawana sifa za kumiliki silaha ni udhalilishaji wa itifaki *(humiliation of protocol)*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, ulinzi na usalama ni pamoja na kutambua hadhi ya itifaki. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kutambua hadhi ya viongozi wakuu wa Vyama vya Siasa ambao si Wabunge lakini Vyama vyao vina uwakilishi Bungeni na kuwapa hadhi ya kidiplomasia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiingii akilini kuona kiongozi wa Kitaifa kama Profesa Ibrahim Lipumba ambaye Chama chake kina Wabunge wengi Bungeni, kinaunda Serikali ya Umoja wa Kitaifa huko Zanzibar anakuwa hana hadhi ya kidiplomasia. Kwa upande mwingine inashangaza kuona kiongozi wa Kitaifa kama Dkt. Willbroad Slaa ambaye Cama anachokiongoza kinaunda Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni anakuwa hana hadhi ya kidiplomasia wakati Wabunge walioko chini yake wana hadhi hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, viongozi wakuu wa vyama vya siasa wenye uwakilishi mkubwa Bungeni ni viongozi wa Serikali watarajiwa hivyo kupuuza itifaki na ulinzi wao ni kuiweka nchi katika mtaziko na mashaka. Hili si jambo ambalo mnaweza kuliunga mkono kwa sasa, lakini ni jambo muhimu kulielewa kwa sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na mapendekezo ya vifungu mahsusi, Mamlaka ya Msajili wa Silaha. Mamlaka na majukumu ya Msajili wa Silaha yametolewa chini ya kifungu cha 8(2) cha Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha, lakini kifungu hicho hakijatoa mwongozo au mipaka ya utekelezaji wa majukumu ya Msajili wa Silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo yake ni kwamba katika maeneo mbalimbali ya sheria hii Msajili amepewa mwanya mkubwa wa kuamua anavyotaka *(discretion)*. Kwa mfano, kifungu cha 17(1) na (2) kinampa Msajili wa Silaha mamlaka ya kutoa kibali cha kumiliki silaha kwa mtu yeyote kwa kipindi ambacho ataamua yeye mwenyewe na kuweka masharti ya kibali hicho yeye mwenyewe. Aidha, Msajili anaweza katika muda wowote kufuta kibali cha umiliki wa silaha.

Matokeo yake ni kwamba katika maeneo mbalimbali ya sheria hii, Msajili amepewa mwanya mkubwa wa kuamua anavyotaka *(discretion)*, kwa mfano, kifungu cha 17 (1) na (2) kimpa Msajili wa Silaha mamlaka ya kutoka kibali cha kumiliki silaha kwa mtu yeyote kwa kipindi ambacho ataamua yeye mwenyewe na kuweka masharti ya kibali hicho yeye mwenyewe. Aidha, Msajili anaweza katika muda wowote kufuta kibali cha umiliki wa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani ina mtazamo kwamba ni bora zaidi masharti ya utoaji wa kibali cha muda masharti ya muda au kipindi ambacho kibali hicho kitakoma na masharti ya kufuta kibali yakawekwa na sheria na siyo kutegemea utashi wa Msajili wa Silaha. Kwa kufanya hivyo, mianya ya rushwa na upendeleo na uonevu wa aina yoyote katika utekelezaji wa majukumu ya Msajili wa Silaha inaweza kuzibwa na kukwepeka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 26(1) cha Muswada huu ipo orodha ya mambo au tabia zinazoweza kumkosesha mtu sifa ya kumiliki silaha. Miongoni mwa tabia hizo ni pamoja na ukorofi. Kwa kuwa tafsiri ya neno "ukorofi" ni *subjective* na kwa kuwa kila mtu anaweza kutafsiri ukorofi kwa namna yake, hivyo Msajili wa Silaha anaweza kuwa na tafsiri yake ya ukorofi kutokana na hisia zake na kumnyima mtu leseni ya kumiliki silaha kwa kisingizio kwamba mtu huyo ni mkorofi.

Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba neno "ukorofi" litafsiriwe na sheria hii ili kuondoa mkanganyiko wa tafsiri pindi sheria itakapoanza kutekelezwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26(2) cha Muswada huu kinaeleza kwamba, endapo Msajili wa Silaha ataridhika kwamba kuna sababu za msingi za kuamini kwamba mtu ana sifa ya kumiliki silaha atatoa *notice* ya maandishi ya kumtaka mtu huyo kufika mbele yake katika muda na sehemu iliyotajwa katika *notice* hiyo, ili kuonyesha ni kwa sababu gani asitangazwe kuwa hana sifa ya kumiliki silaha?

Aidha, ikiwa mtu alipewa *notice* hiyo atashindwa kuhudhuria katika muda na sehemu iliyotajwa katika *notice*, Msajili wa Silaha atamtangaza mtu huyo kuwa hana sifa ya kumiliki silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaona kwamba kifungu hiki kina upungufu mkubwa na upungufu huo ni pamoja na muda wa kufika mbele ya Msajili kutowekwa sheria badala yake kuachwa katika utashi *(discretion)* wa Msajili wa Silaha.

Kwa sharti la kufika mbele ya Msajili wa Silaha mwenyewe kujieleza kama mtu ana sifa ya kumiliki silaha iwapo kuna mashaka juu yake, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri kwamba muda wa kufika mbele ya Msajili uwekwe mbele ya sheria ili kuziba mwanya na uonevu unaoweza kutumika kwa kuweka muda mfupi ili mtuhumiwa ashindwe kufika katika muda huo na kutangazwa kuwa hana sifa ya kumiliki silaha. *(Makofi)*

Aidha, sharti la kufika mbele ya Msajili mwenyewe liondolewe na badala yake sheria iweke Wasajili wasaidizi katika Mikoa ili kupunguza adha na gharama za kusafiri kumfuata Msajili wa Silaha mmoja ambaye kwa vyovyote vile ofisi yake itakuwa ni Dar es Salaam.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26(3) kinasema kwamba cheti cha kuonyesha uwezo, leseni na kibali kilichotolewa kwa mtu aliyetangazwa kuwa hana sifa ya kumiliki silaha, vitapoteza uhalali wake kuanzia tarehe ya kutangazwa huko. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji, ni kwa nini Serikali itoe cheti cha kuonyesha uwezo, leseni na kibali kwa mtu ambaye hana sifa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivi kwa sababu ikiwa Serikali itakuwa makini tangu mwanzo mtu anapoomba leseni au kibali cha kumiliki silaha, basi uwezekano wa mtu huyo aliyekidhi vigezo tangu mwanzo vya kumiliki silaha kupoteza sifa na kutangazwa kuwa hana sifa utakuwa ni mdogo sana, vinginevyo awe ameugua kichaa cha ghafla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 26(4) kinasema pia kwamba mtu aliyetangazwa kuwa hana sifa ya kumiliki silaha, basi ataisalimisha katika Kituo cha Polisi haraka iwezekanavyo, cheti cha kuonyesha uwezo, leseni na vibali vilivyotolewa kwake, silaha pamoja na risasi zilizo katika umiliki wake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona kwamba huu unaweza kuwa ni uporaji wa hila wa silaha za wananchi kwa kutumia sheria kwa kuwa Muswada huu haujatamka ni hatua gani zitafuata baada ya mtu aliyetangazwa kuwa ana sifa za kumiliki silaha atakaposalimisha silaha yake na nyaraka za umiliki katika Kituo cha Polisi. Sheria hii ikiachwa kama ilivyo, inaweza kutumika kwa kulipiza visasi ama kutekeleza maelekezo yenye nia mbaya.

Utoaji wa silaha na risasi kutoka katika ghala la Umma ama Kituo cha Polisi. Kifungu cha 29 (1) cha Muswada huu kinaeleza kwamba silaha ama risasi zilizohifadhiwa katika ghala la

Umma, Kituo cha Polisi ama sehemu nyingine yoyote iliyoelezwa na Msajili hazitatolewa humo isipokuwa kwa kibali kilichosainiwa na Msajili.

Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa kuwe na ugatuzi wa madaraka ili kibali cha kuondoa silaha katika ghala la Umma au sehemu nyingine yoyote kiweze kusainiwa na Wakuu wa Polisi wa Mkoa hasa pale inapotokea madhara mfano ujambazi, uasi na wanyama hatari.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kifungu cha 33 cha Muswada huu kinampa Waziri mamlaka makubwa ya kutunga kanuni zitakazoweka masharti ya utoaji wa kibali cha muuzaji wa silaha, masharti kuhusiana na eneo la biashara la muuzaji, masharti ya kutolewa upya kwa kibali cha muuzaji na masharti ya kusitishwa, kufutwa kwa muda kwa kibali cha muuzaji wa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza masharti hayo yatajwe na sheria ili kuziba mwanya wa Waziri kutumia madaraka yake vibaya kwa kuweka masharti kandamizi ama ya upendeleo kwa baadhi ya makundi ya wauzaji wa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upekuzi na ukamataji wa silaha. Kifungu cha 54 cha Muswada huu kinasema kwamba hakuna mashitaka ama hatua zozote za kisheria zitachukuliwa dhidi ya Msajili ama mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa anayetekeleza majukumu yoyote chini ya sheria hii kwa lolote atakalolitenda kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna utendaji bora usiokuwa na mipaka. Kifungu hiki kinaweza kutumika vibaya kwa kuwa kinatoa mwanya mkubwa kwa Msajili ama Afisa yeyote aliyeidhinishwa kupekua au kukamata silaha au kufanya jambo lolote hata kama ni ovu kwa kisingizio cha nia njema.

Hivyo Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba sheria hii imtake Msajili ama Afisa aliyeidhinishwa kuzingatia kanuni na taratibu za upekuzi na ukamataji kwani kumiliki silaha kihalali siyo kosa la jinai, hivyo upekuzi na ukamataji uzingatie taratibu za kisheria hasa kwa wale wanaomiliki silaha kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapendekezo na marekebisho ya baadhi ya vifungu yataletwa katika jedwali la marekebisho wakati wa Kamati ya Bunge Zima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, imekuwa ni desturi kwa Serikali zilizopo madarakani kuleta Miswada ya Sheria kwa ajili ya kulinda maslahi yake yenyewe bila kujali maslahi mapana ya wananchi na Taifa kwa ujumla.

Aidha, imekuwa ni desturi sheria nyingi kupitishwa haraka haraka bila kupata maoni ya wadau wengi jambo ambalo husababisha sheria nyingi kupingwa hata kabla hazijaanza kutumika. Mfano halisi ni Muswada huu kutoshirikisha wadau ipasavyo. Wadau wengi walilalamika mbele ya Kamati ya Ulinzi na Usalama kwamba hawakushirikishwa kabisa katika mchakato wa kuandaa Muswada huu.

Kambi Rasmi ya Upinzani inaihoji Serikali: Je, ni kwa nini inapuuza wadau katika sheria muhimu kama hii? Je, Serikali haioni kuna athari kubwa kiulinzi na kiusalama kwa kutowashirikisha wadau wakubwa wa silaha na risasi kama vile Makampuni ya ulinzi binafsi na wafanyabiashara wakubwa wa silaha hapa nchini?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inasisitiza tena kwamba amani na utulivu wa nchi hii hautategemea tu uwepo wa Sheria ya Udhibiti na Usimamizi wa

silaha na risasi, bali uongozi unaozingatia misingi ya utawala bora, haki, usawa, ukweli na ustawi wa jamii nzima kwa ujumla.

Aidha, ugumu wa maisha unaosababishwa na umasikini uliokithiri kutokana na mfumuko wa bei, elimu duni, maradhi, ukosefu wa ajira, ukosefu wa maji safi na salama na kadhalika ni viashiria vikubwa vya uvunjifu wa amani kuliko silaha na risasi ambazo Serikali inafanya bidii kubwa kutungia sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni bado inaitaka Serikali kukumbuka na kuzingatia barabara masuala manne muhimu iliyotahadharisha yasichezewe na kufanyiwa mzaha kwani yanaweza kuliingiza Taifa hili katika machafuko. Masuala hayo ni kuchezea haki ya wananchi kujiandikisha kuwa mpiga kura, kufanya mzaha na uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi, matumizi ya kisiasa ya Jeshi la Polisi na ulinzi wa raia na mali zao hususan watu wenye ulemavu wa ngozi, yaani Albino.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaingia kwenye mjadala na tunaanza na mchangiaji wetu wa kwanza ambaye ni Mheshimiwa Dkt. Anthony Mbassa, kama hayupo aanze Mheshimiwa Masoud na Mheshimiwa Mussa H. Mussa ajiandae.

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu na nikupongeze kwa kunipa nafasi ya kuchangia Muswada huu kama mchangiaji wa kwanza.

Pia naomba ni-*declare interest* kwamba mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwangu ni kuboresha tu baadhi ya mambo ya hapa na pale ili kuweka vizuri Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo na madhumuni ya Muswada unaeleza wazi kwamba ni kusimamia na kudhibiti umiliki na matumizi ya silaha na risasi. Katika kudhibiti na kusimamia umiliki huu wa silaha na risasi imeonekana kwamba kuna matatizo makubwa ambayo yanakwaza nchi yetu na baadhi ya Watanzania wamekuwa wakilalamika muda mrefu kwamba watu ambao wanapoteza maisha, bado umakini wa Serikali haujakaa vizuri na zaidi kwa wenzetu waliopo mipakani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna malalamiko makubwa kwamba wahamiaji haramu na wakimbizi wanatumia silaha katika maeneo ya mipakani na kuwajeruhi baadhi ya wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, haya yanapotokea ni kwamba Serikali mara nyingi tumekuwa tukiishauri na tukiiambia kwamba ni vema wakati huu Watendaji wetu wa Vijiji vyote waliopo mipakani wachukue hatua nzuri na ili na wao wenyewe waepukane na kupewa tuhuma. Lakini kwa sababu wananchi wenyewe wana uelewa mpana na wanaelewa kwamba wahamiaji haramu wanatoka nchi za jirani, wanakuja katika maeneo yale, wanapata baraka zote za Watendaji wa Vijiji. Anakuja mtu kuchunga au kufuga, anakuja mtu kufanya biashara anakaa pale muda mrefu, anaoa na kila kitu na baadaye yanayotokea ndiyo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa Serikali ni lazima iliangalie suala hili kwamba ni kwa kiasi gani itaandaa mazingira na mkakati maalum wa kudhibiti wahamiaji haramu kutoka nchi jirani na hasa wakimbizi. Hili lilikuwa ni jambo langu la kwanza kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uboreshaji wa maeneo hayo kuna matumizi ya silaha hasa wakati Polisi wanatakiwa kutumia hizo silaha zenyewe na hasa wakati wa maandamano. *Post General Order* (*PGO)*, imeweka bayana, imeeleza waziwazi, wakati mtuhumiwa au mtu yeyote ambaye tayari yuko katika mikono ya Polisi, sasa kitu ambacho kinasikitisha, wakati wa kutumia silaha hizi ndani ya Jeshi lenyewe la Polisi, wawe makini kupita kiasi. Unakuta mtu amekamatwa yuko ndani ya mikono ya Polisi, lakini siyo muda mrefu unakuta tayari anavuja damu. Sasa hili nalo ni jambo ambalo limekuwa likilalamikiwa muda mrefu sana na ni jambo ambalo halipendezi na halikubaliki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii tunaelekea kwenye uchaguzi, halafu malalamiko haya yanakuja kila wakati, halafu unasikia Polisi wa ngazi za chini wanasema hii ni amri kutoka juu. Amri kutoka juu huko *IGP's* inaweza kuwa wanamzushia tu, Makamishna nao wanasema hawahusiki, Makamanda wa Mikoa wanasema hawahusiki. Sasa amri kutoka juu ni kutoka sehemu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaelekea katika uchaguzi. Huu ni mwaka uchaguzi, hivyo nawaomba sana Polisi wa ngazi za chini wasiwe tayari kutumiwa na baadhi ya viongozi wa kisiasa. Hili ni jambo moja kubwa sana ambalo linakera, linaumiza na kwa kweli huko tunakoelekea tuwe makini kupita kiasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usajili. Nakubali kabisa kwamba kwa upande wa Tanzania Bara *IGP* atakuwa yeye ndio anayewajibika zaidi na kwa upande wa Zanzibar Kamishna wa Polisi Zanzibar naye ndio atakuwa anawajibika kusajili silaha zote. Ushauri wangu tu ni kwamba katika hali hii pale ambapo itatokea tatizo lolote na hasa kwa upande wa Zanzibar ambapo wanasema sheria hii inatumika Tanzania Bara na Zanzibar, lakini kuna vifungu vya sheria hapa vinasema waziwazi kwamba umiliki wa silaha kwa upande wa Zanzibar sheria bado inabana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa basi kwa kuwa sheria hii inatumika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano, lakini upande mmoja wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hauruhusu kumiliki silaha. Sasa sipingani na hilo kwa upande wa Zanzibar, lakini ni aina gani ya watu waliopo Zanzibar hawapaswi kumiliki silaha? Je, ni watu wote hata wakiwa Wabunge? Ni watu wa aina zote, hata Mawaziri waliopo Zanzibar hawapaswi kumiliki silaha?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashauri kwamba watu ambao wana *status* ambazo nimezitaja; Mawaziri na hata Wabunge waliopo Zanzibar kwa jinsi heshima zao zilivyo, naona hili liangaliwe upya angalau tu kwamba twende sambamba na taratibu zilivyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni umri wa kumiliki silaha. Kamati ilieleza vizuri kwamba umri wa kumiliki silaha ni miaka 25 na katika hili, huu umri mimi sipingani na hilo, lakini kuna haja ya kuangalia tena kwamba hoja kubwa inaonekana kwamba umri wa miaka 21 bado inaonekana vijana kwa kiasi kikubwa zaidi hawajatulia. Lakini kuna watu wengine wana umri wa miaka 40 wanatumia silaha vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna watu wengine wana miaka 40, 50 au hata 60 lakini tumekuta baadhi ya matukio yaliyopita, tena wengine viongozi, anampiga mtu risasi na anapoteza maisha. Ana umri wa miaka 60 na ni kiongozi wa juu. Yametokea miaka iliyopita, si tunayo mifano hiyo! Mheshimiwa Waziri wa Fedha tulia. Hiyo ndiyo hali halisi ilivyo na hili halikubaliki. *(Kicheko/Makofi)*

Kwa hiyo, hili nalo ni lazima tukae vizuri na tujipime. Mbali ya hoja ya umri lakini ionekane wazi kwamba elimu inahitajika zaidi katika suala zima la kuweza kumiliki silaha na risasi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kiwango cha faini. Yule ambaye silaha yake haikusajiliwa, faini yake imeelezwa kwenye sheria, ni Shilingi milioni 10 na kifungo cha miaka miwili na katika hali ya kawaida ikaonekana kwamba kama atakutwa ni tajiri na ana uwezo wa kulipa faini kwa muda wowote, anaweza kutumia silaha vibaya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubali kabisa kwamba faini iondolewe iende kwenye kifungo tu moja kwa moja cha muda wa miaka mitano ili angalau tuone kwamba matatizo haya yanaendelea kukomeshwa. Nitamshangaa sana Mheshimiwa Mbunge atakayesimama hapa na kusema kwamba bado faini iwepo, wakati watu wanaendelea kuuawa kila siku katika maeneo mbalimbali, Waheshimiwa Wabunge tunalalamikiwa; Mbunge akisema hapana na faini iwepo, nitamtafsiri vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la mwisho, katika hili naomba nisisitize lile la mwisho ambalo lina nguvu za ziada. Pia kuna tabia hivi sasa na kwangu ni ushauri mkubwa tu kwa baadhi ya wananchi wanaotusikiliza; kuna askari mmoja hivi karibuni hapa Dodoma naye vilevile alipoteza maisha. Askari alikwenda kutatua mgogoro, lakini bahati mbaya akajikuta naye vilevile anapata tatizo na akapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, hili nalo liangaliwe jinsi *PGO* anavyoelekeza; ni wakati gani Askari katika kutatua migogoro kwenye maeneo anakwenda peke yake mmoja au wanakwenda wawili. Hili nalo ni jambo jema la kuliangalia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 58 inasema: Ofisi ya Masjala Kuu ya Silaha itakuwa Makao Makuu ya Jeshi la Polisi Dar es Salaam na Ofisi ya Masjala Ndogo itakuwa Zanzibar. Sasa mngebaini kwamba itakuwepo Dar es Salaam kwa sababu ndipo ilipo Makao Makuu, kwani tunatarajia Dar es Salaam, maisha yatakuwa ndiyo Makao Makuu? Kumbe tayari mmeshaweka dhana kwamba Makao Makuu ya Nchi yapo Dar es Salaam! Makao Makuu ya Polisi, maisha yatakuwa pale Dar es Salaam? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ile dhana kwamba Makao Makuu ya nchi itakuwa Dodoma, kumbe hayapo katika vichwa vyenu! Ndiyo mantiki inayokuja hapa! Kumbe hamna kabisa hili! Makao Makuu kumbe hayawezi kuondoka! Nafikiri sheria ingesema kwamba Makao Makuu ya nchi popote ambapo itakuwa ndiyo Makao Makuu ya Masjala. Lakini mnaposema itakuwa Dar es Salaam tu, wakati huu sawa, lakini ingewekwa katika hali kama hiyo, *blank* kidogo angalau kwamba popote Makao Makuu ya Nchi. Kumbe hamna nia njema ya kuhamia hapa Dodoma! Kumbe ndiyo dhana ilivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, tupo pamoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante, Mheshimiwa Mussa H. Mussa, ajiandae Mheshimiwa Mipata.

**MHE. MUSSA HASSAN MUSSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ambayo ipo mbele yetu. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uwezo wa kusimama katika hafla hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba utangulizi wangu niwapongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara kwa kuwasilisha Muswada huu kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya pongezi hizo, naomba nijielekeze katika mambo matatu. Kwanza, niseme kwa nafsi yangu. Mimi ni mtu wa Pwani, natoka upande wa pili wa Jamhuri ya Muungano Zanzibar. Sasa Kiswahili changu kidogo, nikiri msanii aliyesema kwamba

Kiswahili chabishana cha Pwani siyo cha Bara; unaitwa Abdallah wengine watasema Abdara. Kwa hiyo, wakati natamka hapa, naweza nikasema gobore kwa kwetu na upande mwingine ikawa gobole lakini mwisho wa habari itafahamika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napata mashaka na wale ambao wanajaribu kupata hofu kwenye Muswada ambao umewasilishwa hapa. Mashaka yangu yanakuja wapi? Sisi tunasema kwamba ukimwona Askari yupo kwenye zikri au Maulidi, kuna tatizo. Halikadhalika raia mwema akimkimbia Askari Polisi, basi naye vilevile ana tatizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar, sheria inatamka wazi kwamba sheria itatumika kwa pande mbili; upande wa Bara na upande wa Zanzibar, lakini Zanzibar hali tuliyokuwanayo sasa, nafikiri ni vyema mpaka pale Baraza la Wawakilishi nalo litakapowasilisha sheria hii barazani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Zanzibar kuna lugha moja mbaya sana. Kuna lugha au *term* inayosema, "potelea mbali." Mzanzibari anaposema potelea mbali, msikilizaji awe makini sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba nitoe mifano ambayo imetokea pale Zanzibar. Tarehe 26 na 27 Januari, 2001 kulitokea tendo ambalo haliwezi kusahaulika. Upande mmoja wanalalamika wanasema limeweka watu vizuka, walemavu na wengine walipoteza maisha. Lakini ukiuliza na ukidadisi hoja hii imetoka wapi, utaambiwa ni suala la matokeo ya uchaguzi. Hivi uchaguzi umefanyika mwezi wa Kumi, tukio hili limetokea mwaka 2001 Januari, uhusiano huu uko wapi?

Mheshimiwa Spika, lakini ni nini hasa kimetokea? Watu wanasema wanapinga utendaji au matokeo halali au uendeshaji wa shughuli nzima ya uchaguzi. Halina ukweli! Suala la uhalisia hapa, kuna wigo ambao hauna faida ndani yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, unapozungumza *history* ya Ujerumani haikamiliki kama hujazungumzia tarehe 26 na 27 Januari. Sasa sijui wigo huo unahusishwa vipi na wigo ambao unajitokeza hapa.

Juzi tu tarehe 26 na 27 Januari kulitokea matokeo hapa na imetajwa kwenye Bunge hili kwamba watu wanalalamika. Lakini hii ni *history* ya Hitler wakati walipokuwa wanakataa kutweza nguvu na kufanya mapenzi ya jinsia moja kule Ujerumani. Sasa inahusishwa na Tanzania kwa misingi ipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri Muswada huu ni vyema tukaukazia na tukaupitisha kwa nia moja kwa sababu unahakikisha na kudumisha usalama katika nchi yetu. Suala la silaha na risasi siyo la mchezo; na kila Mtanzania mwenye nia njema, basi ni budi aunge mkono na ashiriki kupitisha Muswada huu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hilo halitoshi, kuna wiki mbili tu nyuma, hili linanipelekea kwanza niwapongeze Watendaji na Maofisa wa Polisi kule Zanzibar. Kunakuwa na uchunguzi na ufuatiliaji wa kina na matukio makubwa ya kuhatarisha amani bado hayajatokea. Lakini iwapo sheria hii inatamka wazi katika Kifungu cha (2) kwamba, itatumika Bara na Zanzibar, basi tuwe na hadhari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kuna Skuli moja inaitwa Faraja ipo Jimboni kwangu, eneo maarufu linaitwa Kwamtipura, ndani ya Jimbo la Amani kulirushwa mabomu. Mabomu hayo yalikuwa mawili, kwa bahati nzuri hayakuleta madhara. Lakini wahusika ni nani? Ni watoto wadogo na kwa sababu za kiuchunguzi tu, sina haja ya kwenda *deep*, lakini wametengeneza mabomu

kienyeji kwa kutumia *hapic* hii ya kusafishia nyumbani. Kitu ambacho kilishindwa kutumika pale na kilichosababisha labda isiwe hasara kubwa, wameshindwa kuweka *segments*, *either* vipande vya vyuma, misumari au vitu vingine.

Sasa hiki siyo kitu cha mchezo hata kidogo kusema kwamba kwa sababu tu sheria inasema Msajili Mkuu atakuwa *IGP* na kwa Zanzibar atakuwa Kamishina wa Polisi, tukasema haya Zanzibar nayo iingie kwenye msweka msweka huu wa kutumia sheria hii. Bado wakati haujafika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hebu tutazame *history*. Ni muda mfupi tu, Viongozi wa Siasa wamekamatwa na silaha pale Zazibar. Utaratibu na sheria iliyopo Zanzibar sasa hivi, mwananchi na mtu yeyote anayetaka kuingia pale Zanzibar, anapaswa kusalimisha silaha yake *either* bandarini au *airport*. Watu wanasema Zanzibar ni njema, atakae na aje, wewe unaingia na silaha kule unakwenda kufanya nini? Kuna ulinzi wa kutosha, ni nchi ya amani, ni kisiwa cha amani, unakwenda na silaha unatafuta nini?

Mhehimiwa Mwenyekiti, lakini ukirudi nyuma, ukisema kwamba nchi ina ulinzi wa kutosha, kuna amani, wewe unakwenda kwenye uchaguzi, unashindwa kwenye uchaguzi, unaandamana; unataka kuvamia Kituo cha Polisi, unachukua silaha, uelekee wapi? Inakuja Sheria hapa ili tupitishe sheria mpya ambapo matokeo ya uchaguzi yanaweza yakahojiwa, hata ya Urais, wewe unakataa una-*walkout*, Muswada huu nao unaukataa, sasa tunaelekea wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, nafikiri huu ni wakati muafaka wa sheria hii na ninaomba kila mmoja wetu, Mtanzania mwenye nia njema na amani ya nchi hii tuunge mkono kuupitisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaha na risasi ni vitu ambavyo vina mawanda mapana katika tafsiri. Mimi naikumbuka moja, Mark Mallone aliweka gari tu, kulikuwa na mbolea na *element* fulani, ikalipuka na ghorofa 27 zikaanguka na mauaji yakawa ni makubwa sana. Sasa kipengele cha kusema kwamba kuwe kuna kibali kwa watengenezaji wa silaha nacho tukiangalie vizuri. Mimi nafikiri ni vema silaha hizi ziwe na kikomo kama inavyokuwa inatamka sheria na kusiwe na mwanya mwingine wowote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, nirejee tena kuwapongeza Viongozi wa Wizara na Watendaji kwa namna ambavyo wanaimarisha ulinzi katika nchi yetu; na bado, pamoja na kwamba kuna matatizo madogo madogo, lakini nchi yetu bado ni salama. Tushirikiane kupitisha Muswada huu ili tuendelee kudumisha amani na utulivu huu katika nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ilizungumzwa hapa, lakini kitu ambacho kinasikitisha sana ni kwamba, chochote kinachozungumzwa kuhusu matumizi mabaya ya silaha kinahusishwa na siasa na kwa Zanzibar zaidi ni watu wa dini. Lakini tutazame silaha kwa maana ya risasi, watu wa namna hii wanapoikosa, wanatumia *acid* na kuhilikisha na kuumiza viongozi.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Namwita Mheshimiwa Mipata, ajiandae Mheshimiwa Ngonyani na atafuatiwa na Mheshimiwa Maselle.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa nafasi. Nami ninayo machache ya kuchangia katika Muswada uliopo mbele yetu, Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu ni muhimu na ninaanza kwa kuunga mkono kwa sababu zifuatazo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza niipongeze Serikali kwa hatua mbalimbali ambazo imekuwa ikichukua katika kuhakikisha kwamba silaha zinapungua na hazizagai hovyo. Mheshimiwa Naibu Waziri ametuelezea hatua na matukio mbalimbali yaliyokwishapita ya kupunguza silaha ambazo zinazagaa hovyo katika maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ambayo yanakuwa na matukio mengi ya uhalifu hasa yale ya mipakani, nizungumzie katika mwambao wa Ziwa Tanganyika, yanatokana na mahusiano ya karibu yaliyopo na nchi za jirani ambao pengine wenzetu hawana sera nzuri kama sisi tulizonazo hizi za kuhakikisha kwamba silaha zinaangukia katika mikono salama na uangalizi wa Polisi na vyombo vingine unakuwa karibu kuangalia kwamba silaha zinakuwa kwa watu wanaohusika na hatua mbalimbali kama hizi zinachukuliwa ili kuhakikisha kwamba silaha haziendi katika mikono ambayo siyo salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu sisi tunaokaa mwambao wa Ziwa Tanganyika, tunaona adha na usumbufu mkubwa na matukio mabaya yanayotokea ya uvamizi, watu wanaacha shughuli zao kutokana na hofu kwa sababu tu hawana uhakika wa juu ya matumizi ya silaha zinazokuwa zinapatikana katika maeneo haya. Kwa hiyo, binafsi naipongeza Serikali kuleta ajenda hii muhimu kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipengele ambacho naunga mkono ni juu ya adhabu. Ili kuhakikisha silaha hazizagai hovyo, naunga mkono adhabu iliyopendekezwa katika kifungu cha 20 (2) kwa mtu ambaye atakuwa anakutwa na silaha bila kuzingatia sheria. Sheria hii imependekeza na Kamati hasa imekazia juu ya kutoa adhabu ya kifungo na isiwe na mbadala. Hii itasaidia sana katika jamii yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nami naomba Bunge likubali kwamba tunapoangalia juu ya usalama wa wananchi wetu, ili waweze kuendeleza shughuli zao za kiuchumi, walale, wakiamka wajue wako salama, ni lazima tufanye juhudi za kila siku kupunguza silaha zinazozagaa hovyo. Moja kati ya hatua muhimu sana ni adhabu inayoweza kutolewa kwa mtu ambaye atapatikana akiwa na silaha bila utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana juu ya adhabu inayotolewa isiwe na mbadala iwe ni miaka mitano jela akipatikana na kosa la namna hiyo. Ni muhimu sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nije kwenye utengenezaji wa silaha. Wapo wahunzi ambao wanaonesha vipaji vyao katika utengenezaji wa silaha katika maeneo mbalimbali nchini. Mimi pia niungane na mchangiaji aliyetangulia kwamba, kwa hapa tulipofikia siyo vizuri sana kuendelea ku-*encourage* utengenezaji wa silaha ambao pia udhibiti wake utakuwa mgumu sana. Kwa hiyo, nashauri kwamba mamlaka zitakazokuwa na uwezo wa udhibiti wa silaha ndizo pekee ziwe na mamlaka ya kuruhusu ni nani na namna silaha zinavyoweza kupatikana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa upatikanaji wa silaha uliopo sasa hivi, nao nina mashaka nao kidogo. Utakuta maduka yanayouza silaha yako mengi, ingawa kunaweza kuwa na control, lakini nilifikiri silaha siyo bidhaa ambayo tunatakiwa tuipate kila mahali. Iringa unakuta maduka mawili, Dar es Salaam unakuta maduka. Tungekuwa na *control* moja na tena

kwa utaratibu maalum. Siyo busara sana na siyo wakati muafaka kuhakikisha kwamba silaha tunazifanya kama biashara sasa, hapana! Pawepo na udhibiti mkubwa zaidi wa watu kupata silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfumo wa kuchunguza watu wenye silaha bila kufuata mfumo, ni lazima ufuatiliwe vizuri na kwa makini zaidi.

Nakumbuka kuna wakati fulani Serikali yetu iliweka utaratibu ambao ulitumia watu wa kawaida, wanaokaa kwenye maeneo kutoa utambuzi juu ya nani anadhani anamiliki silaha bila kufuata utaratibu? Lile jambo lilisaidia sana na wakati mwingine kutoa matamko yanayowezesha watu wanaomiliki silaha, kuyatoa bila adhabu kwa kipindi fulani, yameweza wakati mwingine kutusaidia kupunguza silaha ambazo zinaweza zikaleta athari baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado naiomba Serikali na Wizara inayohusika, itumie mifumo ya kawaida ya kutoa wito kwa wananchi ili kupunguza uhalifu unaoweza kujitokeza kuhusu suala la kuzagaa kwa silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo ya mwambao mwa Ziwa Tanganyika ni maeneo ambayo kuna wageni wengi ambao wanatokana na ujirani wa nchi ambazo tumepakana nazo. Kwa sababu maeneo ya mpaka ni vigumu kudhibiti uhamiaji, kuna wasiwasi mkubwa kwamba katika maeneo haya kunakuwa na silaha vilevile. Matukio hayo utayakuta katika vipindi ambavyo uhalifu unatokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiweka mfumo ambao utawezesha wenyeji wanaokaa katika maeneo hayo kuwa na utaratibu wa kawaida wa namna ya kutoa habari, itatusaidia kuwezesha watu ambao wanamiliki silaha bila utaratibu wakagundulika na ikatusaidia kupunguza matukio ambayo yanatokea katika maeneo hayo ya uvunjifu wa amani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, naunga mkono juu ya adhabu ambayo inapendekezwa iwe kali zaidi kuliko kutoa faini. Kutoa faini, haiwezi kutusaidia katika hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Sasa namwita Mheshimiwa Ngonyani, ajiandae Mheshimiwa Maselle na naona Mheshimiwa Mbassa amerudi, baada ya Maselle atakuwa Mheshimiwa Mbassa.

**MHE. STEPHEN H. NGONYANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nianze kwa kushukuru Serikali kwa mpango huu mzima wa matumizi ya silaha kwamba ni kitu kizuri na wamekileta kwa wakati muafaka.

Vilevile nisiache kuwashukuru Jeshi la Wananchi wa Tanzania pamoja na Polisi Mkoa wa Tanga kwa kazi ambayo waliifanya hivi karibuni kwa kupambana na majambazi ambao walikuwa wameiba silaha, wakaingia kwenye mapango kule Amboni. Pamoja na kwamba Askari mmoja alifariki kwa kutetea wananchi wa Mkoa wa Tanga, lakini vile vile tunawashukuru sana Polisi na Jeshi la Wananchi, walifanya kazi ya ziada sana. Mungu awabariki sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la kumiliki silaha. Naishukuru Serikali kwamba imeleta mpango mzuri sana, lakini kuna matatizo madogo madogo ambayo ni lazima yarekebishwe. Kwanza zile silaha ambazo zilikuwa zimepatikana siku za nyuma, zingeanza kusajiliwa upya. Kwa sababu kuna watoto wengine ni wadogo mno nao wanajiita ni watoto wa viongozi. Wanakuja kwenye mikutano, anatoka kijana anaonyesha silaha au anawaonesha

kwamba yeye ana silaha. Ukimwangalia umri wake, haulingani na jinsi tulivyoletewa hapa. Sasa inafika mahali unajiuliza, huyu umri huu na hana biashara yoyote, silaha ameipata wapi? Jibu ni kwamba unakosa cha kufanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukizingatia, Mbunge kuwa na silaha ni haki yake, na ni haki alindwe. Lakini utakuja kushangaa hata wauza machungwa wengine eti wamepata silaha.

Sasa hii kwa kweli hata kama tunasema tunaleta Muswada ambao utasaidia, lakini vilevile wangeanza tena upya usajili wa hizi silaha. Kila aliyekuwa na silaha aieleze Serikali kwamba aliipata namna gani kwa sababu itatusaidia hata wengine kupita mahali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, juzi katika Jimbo langu, watu wamemvamia na kumuua mfanyabiashara. Wamempiga risasi, wamemuu kule Mkumbara! Matokeo yake, Polisi wametumia kila mbinu kuwatafuta na bahati nzuri wengine wamepatikana, wanahojiwa na wengine wakiwa katika hali ya usalama ni vizuri wakiwa wanachunguza hali kama hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, adhabu ambayo tumeiona hapa ni ndogo sana. Mimi naiona ni ndogo sana! Kama kweli tunataka kukomesha, kusiwepo faini; iwe ni adhabu ya hata kifungo cha maisha. Kwa sababu mnapomkuta mtu na silaha, maana yake ni muuaji; na muuaji mara nyingi anayongwa.

Sasa mtu akutwe na silaha, ameitoa nchi jirani, anakuja kutufanyia uuaji na anaua watu wengi, leo mnapandisha tu kiwango, eti cha miaka miwili jela. Jela ya nini wakati mtu amekuja kuua watu? Kama yeye alikuwa anataka kumiliki silaha kihalali, kulikuwa na haja gani silaha hiyo isisajiliwe kama nyingine?

Mheshimiwa Mwenyekiti, naamini kabisa kwamba tutakapoyafanya haya Serikali yetu itakuwa imefanya kitu kikubwa sana. Nami bahati nzuri kwa mtazamo huu naunga mkono sana, ila ninachoomba ni kwamba shughuli hizi zianze mara moja. Huo mwezi wa Saba mnaotuambia ni mbali sana. Mimi nataka Muswada huu ukipita, kesho tu apelekewe Mheshimiwa Rais, kwa sababu mkisema unaanza kutumika tarehe 1 Julai, kote huko unangoja nini, wakati matukio makubwa ya ujambazi yanaendelea; na huko tunakokwenda ni wakati wa uchaguzi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati wa uchaguzi hata mtu asiyekuwa na silaha atataka kuonesha tu silaha ili watu wasumbuliwe na kutishwa. Lakini tukiupitisha huu Muswada na Mheshimiwa Rais akiusaini, nasi tutakuwa miongoni mwa watu ambao tutawapeni taarifa, ni maandalizi gani watu wanayotaka kufanya? Tusiseme tu vyama, vyama! Hakuna cha vyama hapa! Hapa kila mtu anataka nafasi yake, anataka kwenda kupambana na kupambana kwake kuna mambo mawili. Sisi Waheshimiwa Wabunge hatulindwi, tunajilinda wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeishi Kenya; Mbunge mmoja wa Kenya ana Askari wawili wanaomsaidia kumlinda kwa kila hali. Leo hii Mbunge wa Tanzania ukivuka mpaka silaha unaacha mpakani, sasa tuna usalama gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii Mbunge unatoka hapa unakwenda Zanzibar ambapo ni nchi moja hii, unafika mahali unaacha silaha. Unaiacha ya nini? Kama kweli mlituamini mkatuona sisi ndio wenye Serikali, ni kwanini tuwe na sehemu katika nchi hii ambazo ukifika unaonekana kwamba sio bora?

Mimi nafikiri cha msingi, hii sheria iboreshwe vizuri ili Mbunge wa Zanzibar akija na silaha yake, aje; Mbunge wa Tanzania akiingia Zanzibar, aingie nayo kwa sababu ndiyo ulinzi wetu.

Kufuatana na mazingira yaliyopo sasa hivi, siyo rahisi Kiongozi au Mbunge yeyote kutokuwa na silaha, maana zinatusaidia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bahati nzuri katika maeneo yetu, Polisi wengi wanatusaidia sana kutulinda, wakimwona Mbunge amekaa mahali, hasa mimi kwenye Jimbo langu. Askari yeyote akisikia kwamba Maji Marefu yuko mahali, wanakuja, wanazingira ile sehemu wanakaa karibu, wanaona nafanya nini mpaka naondoka. Hata kwenye Mikutano yangu wananilinda. Je, hao wengine ambao hawalindwi na Askari usalama wao unakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hii sheria irekebishwe vizuri ili iwe mfano kwa kila mtu. Kama ni… nilitaka niongee Kingoni kidogo, lakini nimeona hapa ni Bunge ni lazima tuongee Kiswahili. Kama ni kipengele ambacho kinatakiwa kila mwananchi akijue, basi naomba kifanyiwe haraka na isingoje mwezi wa saba. Haya mambo tukipitisha leo, Mheshimiwa Waziri peleka kwa Mheshimiwa Rais ili hii kazi ifanyike mara moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, sina maneno ila naunga mkono hoja hii kwamba mimi ni miongoni mwa watu wanaounga mkono. Ahsante sana.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Maselle na baadae Mheshimiwa Mbassa.

**MHE. AUGUSTINO M. MASELE:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami mchana wa leo niweze kutoa mchango wangu katika huu Muswada muhimu ulioletwa na Serikali kwa wakati muafaka, Muswada wa Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kabla ya kuchangia naomba nimnukuu Mwanafalsafa mmoja ambaye aliwahi kuishi huko kwenye karne ya nne. Yeye alisema hivi kwa Kiingereza, *"let him who wants peace prepare for war."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, maneno haya ni ya msingi kwamba mtu yeyote yule ambaye anapenda amani ni vema akajiandaa kwa vita. Kwa maana hiyo, naipongeza Serikali yetu kwasababu imeliona jambo hili na kuileta sheria hii wakati muafaka. Kwasababu vipo viashiria ambavyo vimeonyesha dhahiri kwamba katika baadhi ya Serikali ambazo zimeshindwa kuwa na udhibiti wa silaha na risasi, zimejikuta zikiandaa mazingira ya kuwepo na machafuko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali zinapokuwa haziwezi kudhibiti silaha zimesababisha nchi nyingine kuingia kwenye vita. Mfano, ni rahisi tu tumeona Libya iliposambaratika, Boko Haramu na wenyewe wakawa wamezaliwa kwasababu silaha zilizagaa na kuingia katika nchi za wenzetu huko Afrika ya Magharibi, hawana amani tena.

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme wazi kwamba Serikali yetu imechukua uamuzi sahihi na sisi tunapaswa kuiunga mkono na mimi niseme dhahiri kwamba naunga mkono hoja ya Mheshimiwa Waziri. Muswada huu ukishapita ufanywe kuwa ni Sheria mara moja kwasababu Watanzania tunapenda amani na tungependa nchi yetu iendelee kuwa ni kisiwa cha amani ili Mataifa mengine waweze kukimbilia hapa na kupata suluhisho la matatizo yao kama ilivyo jadi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Muswada huu unakuja kubadili Sheria iliyokuwepo hapo mwanzo na kuziba mapengo ambayo kimsingi ni kweli yalikuwepo. Kwa mfano, usajili wa hizi silaha, nami naunga mkono kwamba sasa uwe mikononi mwa Jeshi la Polisi badala ya kuruhusu Halmashauri kuwa zinafanya kazi na zenyewe kufanya kazi ya umilikishaji wa silaha hasa magobore.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini naunga mkono? Ni kwasababu masuala ya ya ulinzi ni taaluma, sasa unapotoa mamlaka kama haya kwa raia wenyewe waendelee kumikishana silaha, maana yake ni kwamba usalama unakuwa uko mashakani. Kwa maana hiyo, naiunga mkono Serikali iendelee na mkakati wake huo.

Aidha, naunga mkono suala la umri kwamba vijana ni kundi kubwa na kwa nchi yetu ni dhahiri kwamba tukiruhusu, kundi hili ndiyo linaweza kujikuta lina silaha zaidi kuliko makundi mengine. Kwa maana hiyo, nashukuru tu kwamba Serikali imeanza kuona kwamba jambo hili liwekewe angalau *limitation* kwamba mtu aanze kumiliki silaha akiwa na umri wa miaka 25. Hongera sana Serikali.

Aidha, niseme tu kwamba adhabu imewekwa ili iweze kudhibiti na iwe tishio au kichocheo cha kumzuia mtu kupata hamu ya kutenda kosa na kwa maana hiyo, uwepo wa adhabu ya miaka mitano kwa mtu yeyote ambaye atapatikana na kosa la kumiliki silaha kinyume na Sheria, ni jambo muafaka na kwamba kusiwe na hiyo *alternative* au *option* ya kwamba mtu anaweza akapata adhabu ya kulipa faini. Hiyo *option* ya faini name nashauri isiwepo. Ni kwamba mtu akipatokana na kosa la kumiliki silaha bila utaratibu, basi aadhibiwe kwa kifungo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nisiwe na maneno mengi ya kuongea hapa kwasababu naona tu dhahiri kwamba mambo mengi ambayo yamewekwa ndani ya Sheria hii au Muswada huu ni mambo ambayo yana msingi mkubwa, labda la kumalizia tu ni kuhusiana na hawa wabunifu ambao ni Watanzania wenzetu.

Naomba tu Serikali na yenyewe ingeandaa mazingira ya kuwaangalia hawa Watanzania wanaoweza kuwa na hizo sifa za kuwa wabunifu, basi waandaliwe mazingira waweze kukuza vipaji vyao na hatimaye ikiwezekana na sisi tupate Watanzania ambao wanaweza kuleta mambo mapya hapa duniani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukiendelea kuwabana na kuwazuia wasiwe na upenyo wa kudhihirisha vipawa vyao, tunaweza tusiwe tunatenda haki.

Najua kuwa kazi yoyote ambayo mwanadamu anaweza kuifanya, ikiwekwa katika utaratibu mzuri, inaweza kuleta mchango katika maendeleo ya nchi yetu, maana hawa watu wanaweza kudhihirisha vipawa vyao vya Wanasayansi. Kwani hawa wanasayansi wengine wa huko duniani walianzaje? Walianza kwa ubunifu kama huu, wakatengenezewa mazingira mazuri, ambao waligundua hizi silaha za *automatic machine gun* walikuwa ni watu wa kawaida.

Kwa hiyo, nasi Watanzania tunaweza kuandaa utaratibu wa namna ya kuwatengenezea mazingira Watanzania hao waweze kuonyesha vipawa vyao ili mradi tu Serikali iweze kuwaandalia udhibiti mzuri na sheria iweze kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Dkt. Mbassa, halafu wajiandae Mheshimiwa Moza, Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili name nichangie katika Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi ambao uko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze kwa kutoa pole kwa Mama Anna Mloe ambaye alidhurika kutokana na matumizi mabaya ya silaha huko Tunduma ilhali wananchi walikuwa katika utaratibu wa kawaida kuona waweze kufanya nini ili kunusuru afya zao kwa nia njema kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni jambo ambalo linasikitisha. Katika hali ya kawaida vyombo ambavyo vinapashwa kusimamia sheria hii, vinapaswa kusimamia silaha hizi, vinakubali matukio kama haya yanatokea na Mama huyu sasa hivi yuko hospitali, hali yake ni mbaya, lakini tunamwombea Mungu amsaidie japo mtoto ameshapoteza maisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala zima la umiliki wa silaha limekuwa na matatizo mengi sana katika jamii yetu japo linachukua hatua ndefu sana katika kupata au kumiliki silaha kihalali, tunaoishi huko mpakani, silaha hizi zimekuwa zikizagaa na tukiamini kabisa kuwa kuna suala zima la usimamizi na uingizaji wa silaha ambalo linapashwa lifanyiwe utaratibu wa Kisheria na liafuatwe, lakini lakini silaha zinapita na matokeo yake zinazagaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili linatia shaka sana kwasababu kama watu wameshajua ni wapi silaha zinapotokea, kwa nini kusiwe na mbinu chanya za kuweza kudhibiti silaha hizo zisizidi kupita? Lakini kila uchao suala hili limekuwa ni wimbo ambao hauna mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili limetokea kuwa na matatizo hasa huko vijijini, leo hii kuna kesi lukuki Mahakamani au Polisi hasa za watu wanaosingiziwa kumiliki silaha ilhali hawana silaha, na watu wanasoteshwa rumande, wengine wananyimwa dhamana kwamba huyu anamiliki silaha haramu, lakini mwisho wa siku inakuja kubainika kwamba hawa waliosingiziwa hawana hata manati.

**MBUNGE FULANI:** Eeh!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, inasikitisha sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasoteshwa ilhali wale watu waliotoa hizo taarifa hawafuatiliwi kwamba ni kwa nini wamepeleka taarifa ambazo ni potofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba pamoja na mambo yote, iwepo sheria au kanuni ya kuwataka wale wanaotoa taarifa hizi ambazo ni potofu kwa ajili ya kuwaumiza wenzao nao wafuatiliwe na kuchukuliwa hatua.

Vinginevyo imekuwa ni suala la kusingiziana kila uchao ilimradi tu chuki ndogo ndogo zikitokea, fulani anamiliki silaha. Askari kweli wanaenda kumkamata mtu yule. Mtu yule amekuwa mahali hapo miaka nenda rudi kijijini, hana sifa yoyote ya ujambazi wala kumiliki silaha, lakini anatiwa mikononi mwa Polisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tusikubaliane kwamba hawa ni raia wema wametoa taarifa, bali nao tuwafuatilie ili kusudi nao wapate adhabu inayostahili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na suala zima la hili Jeshi la Mgambo au hawa Migambo. Kuna baadhi ya sehemu hawa wanapewa silaha na wanazunguka vijijini. Sasa sijui Sheria inasemaje kuhusiana na watu hawa wanaopewa silaha ilhali wengine hata mafunzo ya Mgambo hawakufuzu inavyostahili. Wanapita vijijini wanatishia wananchi, kila uchao wananchi wakiona basi ni mbio kwasababu wameshaogopa kwasababu wana silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tufuate utaratibu, hawa watu wanapotumwa kwenda vijijini: Je, Sheria inawaruhusu kwenda na silaha pasipokuwa na Askari alaiyepata mafunzo na kuhitimu vizuri? Ndiyo hapo tunapowatambua kama Jeshi la Akiba, lakini wanapokwenda na silaha kule vijijini, wanaleta *image* gani kwa wananchi? Wakirudisha zile silaha wakirudi, mambo yanakuwa ni ya vitisho, wananchi wanaishi kwa hofu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala hili halikubaliki. Vyombo vyetu vya ulinzi tafadhali lizingatie maadili ya kazi ambazo wamepewa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna suala zima la utaratibu unaotumika kuwataka wananchi warejeshe silaha. Silaha hizi zimekuwa zikirejeshwa kwenye Vituo vya Polisi na silaha zinaporejeshwa kwenye Vituo vya Polisi kuna utaratibu wa kuziandika na kuona kwamba zimerejeshwa. Lakini bado mambo haya yanapofanyika, watu hao hao wanazidi kufuatwa vijijini kule kwamba wewe una miliki silaha na taarifa tunazo, ilhali silaha ile ameshairudisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa tunapashwa tupate ufafanuzi, watu hawa ambao wanatii sheria bila shuruti, wakifanya jambo hilo, iweje tena wazidi kusumbuliwa? Kwa nini wazidi kusumbliwa? Mtu akishafanya hivyo, inaonekana basi yeye ameshakuwa na tiketi ya moja kwa moja, yeye ni mmiliki wa silaha wa kudumu na kila likitokea tu wanamfuata. Wananchi wetu walivyo *innocent* inabidi wawe wapole, wanasumbuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba tafadhali, tunapopitisha sheria hii haya masuala yaangaliwe. Mtu anapotumia uhuru wake, akiambiwa una silaha karejesha kweli, basi heshima yake iwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la mwisho, ni jinsi gani suala la mipakani bado halijapewa uzito unaostahili. Ni juzi tu huko Kagera zimeokotwa silaha katika pori la Kimisi na Burigi kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Mkoa wa Kagera na vile vile Mkoa wa Geita. Kwa habari zilizopatikana, inaoneka walikamata hata sare za Jeshi la nchi jirani. Sasa suala la kujiuliza, kama hawa watu waliweza kuwafuatilia na kuna doria za kila mara, iweje hizi kambi ziendelee kuwepo kwenye Mikoa yetu? Hawa watu kama wamepatikana au waliopatikana, iweje intelijensia isichukue mkono wake kujua kwamba hawa watu walitokea maeneo gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli mipaka yetu haijawa makini kiasi cha kuweza kuzuia watu kuingia na silaha haramu? Jeshi la Polisi, Kamati za Ulinzi na Usalama, masuala haya ni muhimu sana kuyafuatilia. Leo hii Wakuu wetu wa Wilaya ndio Wenyeviti wa Kamati za Ulinzi na Usalama, na mle majeshi haya yanahusika, kwa nini hawa watu wasifanye kazi ya ziada ya kutafuta taarifa mbadala kutoka kwa raia wema, au kufuatilia au kuagiza majeshi haya kuhakikisha unakuwepo Ulinzi wa kutosha maeneo yote ambayo yanasadikiwa; Au ambayo basi inakisiwa kwamba watu hawa ndio wanapenyeza?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuwa hivi hivi. Kama hali hii inaendelea, ina maana usalama wa nchi yetu haupo. Ina maana usalama wa raia haupo! Ndiyo maana leo hii unasikia silaha zinakamatwa Dar es Salaam sijui zimetokea wapi, Mara, Geita, sijui zimetokea wapi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba sasa ufike muda muafaka Kamati hizi sasa ziweze kufanya kazi yake inavyostahili, vyombo hivi vifanye kazi inavyostahili ili kusudi tuweze kuondokana na suala zima la uzagaaji wa silaha pamoja na risasi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru, ahsante.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Moza, halafu wajiandae Mheshimiwa Kidawa na Mheshimiwa Vita.

**MHE. MOZA A. SAIDY:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi hii nami niweze kuchangia Muswada huu uliopo mbele yetu japo kwa kifupi sana tu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, usimamizi wa udhibiti wa umiliki na matumizi ya silaha na risasi, kwa hali ya sasa hivi haupo katika mkondo wake wa uhalali halisi. Hapo nyuma kulikuwepo na umiliki wa silaha na watu walikuwa wakitumia silaha, lakini siyo kama utaratibu uliopo sasa hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuishauri Serikali irudishe mpango ule wa mgeni wa aina yeyote anayeingia katika Kijiji, Kitongoji, katika Mitaa yetu anayeingia ndani ya nyumba ya mtu kama ndugu, jirani au rafiki kumtembelea, basi angalau apewe taarifa Mwenyekiti wa Kijiji na aweze kuandikishwa kwenye daftari maalumu na kukaguliwa ana nini alichokujanacho?

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii itasaidia wingu kubwa la mauaji yanayotokea hasa ya Albino. Kwasababu sasa hivi unasikia mtu ameuawa. Muda huu huu Askari wanatoka kumtafuta bila mafaniko ya aina yoyote. Lakini kukiwepo na vitu kama hivi, nafikiri utaratibu kama huu angalau utapunguza vitendo kama hivi na wahalifu wanaweza kupataka mapema mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwepo na uingizaji wa silaha kiholela kwa muda mwingi sana, tumekuwa tukilalamikia hata hapa Bungeni. Hii yote inaletwa na wageni. Nilikuwa nataka kujua, katika mipaka yetu kuna udhibiti gani au jopo kubwa la kuweza kuongeza ulinzi katika maeneo yale, kuzuia uingizwaji wa silaha. Ingawa huko nchi za jirani kweli wana mapigano, na ndani ya mapigano yao wengine wanakimbia, wanaogopa wasiumizwe, lakini wanaingia na silaha katika nchi yetu. Katika nchi yetu, vitu kama hivi vimekutwa sehemu nyingi mno na hadi katikati ya Mikoa yetu vimeanza kuingia, vipo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mauaji yamekuwa yakitokea kiholela kwa muda mrefu, Vituo vya Polisi vinavamiwa, wananchi wanavamiwa, wanaporwa na Serikali bado inafumbia macho hali kama hii. Lakini nimekuwa nikishauri utaratibu ambao Serikakli ingeongeza sasa ulinzi na mbinu zaidi au wakapewa uwezo mkubwa Askari wetu hawa wakaongezewa mbinu maalumu za kuweza kudhibiti vitu kama hivi na vyombo kama hivi vya uingizwaji wa silaha. Ni hatari kubwa katika nchi yetu, kwani nchi yetu ndiyo kimbilio la watu. Leo hii tunaangalia nchi yetu sasa ndiyo imeanza kuwa na hofu kubwa sana. Sitaweza kutoa mifano mingi ambayo imeweza kujitokeza hapa katikati na mbele ya sura zetu hapa hapa nchini mwetu Wilayani kwetu na Mikoani kwetu, inatia aibu sana. Hebu sasa tuwe na msimamo mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri sana Serikali itoe kipaumbele kwa Serikali za Mitaa. Wanaopewa taarifa hizo angalau Jeshi la Polisi au Jeshi la aina yoyote, anapopewa na raia taarifa kwamba kuna mtu anaingiza silaha au kuna mtu ana chombo hicho, basi naomba wawe wanahifadhi, wawe wanatunza hata siri. Hili ndilo jambo ambalo limejitokeza katika nchi yetu kusababisha watu kuogopa kusema ambapo akisema anaambiwa kwamba yeye ameambiwa na Askari fulani, ameambiwa na mtu fulani kwamba kuna silaha ipo hapa, yule mtu anakwenda kudhuriwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii inafikia hatua tunaongea mambo kama haya. Naomba suala kama hili, ukiwa mtu wa ulinzi na usalama, basi kuwa na siri ya ulinzi na usalama na uweze kuitumikia nchi yako na kuweza kuilinda kwa hali na mali na kutunza siri za nchi yako na kudhibiti mipaka na mali za nchi yetu sisi wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa sikitiko kubwa sana kuona Askari wetu ambao wanauawa na majambazi wakiwa bado ni wadogo mno! Hivi Askari mpaka anavamiwa, mpaka anapigwa, anauawa na watu wanaangalia, ni jambo la kusikitisha mno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado niendelee kusema kwamba udhibiti uwepo na watu waweze kuwa na ushirikiano na Jeshi la Polisi. Hebu sasa Jeshi la Polisi na Jeshi la Ulinzi waongeze mapenzi kwa wananchi na kuwalinda wananchi na wananchi nao watoe sasa mioyo yao ya imani kuwa hili sasa ni Jeshi lao waweze kutumikia kwa uhalali liweze kuwasaidia na wao kuwalinda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa na haya machache tu, Muswada huu uliofika hapa mbele yetu kwa kweli tumeupokea na mimi naunga mkono na sheria iliyokuwa imepitishwa, basi sheria hii iwe halali. Ikiwa ni kifungo sasa iwe ni kifungo kweli. Siyo tena leo awe mtoto wa mkubwa fulani au wa Mheshimiwa Moza hapa, mtoto wake ana silaha halafu amefanya jambo la uhalifu, mnaenda kumtoa kule. Ni marufuku, vitu kama hivi tuvifanye viwe vya uhalali kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja hii iliyofika, basi itimizwe kwa utimilifu na uadilifu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Kidawa, ajiandae Mheshimiwa Kawawa.

**MHE. KIDAWA HAMID SALEH:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana na mimi kunipatia nafasi kuchangia Muswada muhimu sana uliopo mbele yetu. Naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu ambao umelenga kuleta usimamizi madhubuti wa matumizi ya silaha ndani ya nchi yetu ikiwemo uingizaji wa silaha, uhifadhi na mambo mengine yanayohusiana na silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi yetu inapita katika kipindi kigumu sana, sisi tulipokuwa wadogo kule Zanzibar ilikuwa kabisa hatujui mambo ya risasi na wala silaha nyingine. Silaha ambazo tulikuwa tukizijua sisi zikitumika katika mambo ya uhalifu ikiwemo wizi wa majumbani ni mapanga, mashoka na visu na jiwe moja kubwa linaitwa jiwe na Fatuma; linachukuliwa linagonga kah! Mlango unafunguka wezi wanaingia ndani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini katika miaka hii ya karibuni zimekuwa zinaingia silaha nyingi za moto kupitia njia za panya. Silaha hizo zinatumika kwa mambo ya kihalifu mbalimbali ikiwemo wizi, ujambazi na hata mauaji ya watu ambao hawana hatia. Kwa hiyo, naipongeza Serikali kwa kuleta Muswada huu kwa sababu mambo hayo yasipodhibitiwa, yataondoa kabisa yale tunayojivunia ya usalama na amani ndani ya nchi yetu na raia wake. Kwa hiyo, hii ni sheria muhimu sana kupitishwa hapa Bungeni kwa sababu itasaidia kuondoa huo udhaifu ambao umejitokeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuchangia katika huu Muswada, labda hapa ukurasa wa 57 ile ya Kiswahili kumeundwa Kamati ya Usimamizi na Udhibiti wa silaha. Ni jambo jema, naunga mkono kuwepo kwa kipengele hiki, lakini ningeomba yafanyiwe marekebisho mawili matatu kutokana na muundo wake, hasa kwa kuwa sheria hii ina sura ya kitaifa kwa maana ni ya Muungano, itatumika katika pande zote mbili za Muungano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa kuna Wajumbe 15 walioainishwa, lakini kati ya Wajumbe hao, ukitupa macho tu utaona ni Mjumbe mmoja tu kutoka Zanzibar ambaye ni Kamishna wa Polisi Zanzibar. Wajumbe wengine wote wanatokea upande wa pili wa Muungano. Kwa hiyo, nashauri kwa wale Wawakilishi ambao wanawakilisha Wizara ambazo siyo za Muungano ambazo ziko pande zote mbili, basi kuwe na Wawakilishi wawili, mmoja kutoka Zanzibar na mmoja kutoka Tanzania Bara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikitoa mfano, kuna Mwakilishi katika Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa amewekwa mmoja, lakini kule Zanzibar kuna Wizara ya Tawala za Mikoa na Vikosi vya SMZ, nao nadhani wangekuwa na mchango mkubwa katika hii Kamati.

Vilevile kuna Mwakilishi kutoka Wizara inayohusika na Mambo ya Fedha ningeshauri mmoja angetoka upande mwingine na mwingine akatoka Zanzibar. Kuna Mwakilishi kutoka Idara ya Magereza. Magereza siyo jambo la Muungano na kule Zanzibar hakuna Magereza. Kwahiyo, atoke mmoja kule na mmoja huku na kwa mtiririko huo huo mpaka tunafika mwisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hesabu hii kutakuwa sasa na Wajumbe 21. saba watakuwa wanatoka Zanzibar na 14 watakuwa wametoka Tanzania Bara. Kwa hiyo, inaleta ile picha nzuri kabisa ya nchi yetu kuwa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu cha 16(3) kinaruhusu mmiliki wa leseni ya silaha kuweza kuadhimisha silaha ile kwa mtu ambaye tayari amepewa ile hati ya uwezo wa kutumia ile silaha. Kifungu hiki sikubaliani nacho. Yule anayemilikishwa silaha atumie mwenyewe ile silaha na kama kuna haja ya kuazimisha, vianzishwe vitengo maalum vya Serikali, vinavyohusiana na mambo ya Polisi, Askari Wanyamapori na Magereza, viwekwe pale na Vituo vya Polisi vipo mpaka vijijini, wale wapewe dhamana ikionekana kama kuna haja ya mtu kuazima aende pale, siyo mtu tu aende akaazimishe silaha ampe. Nchi yetu tutaiweka rehani, amani ya nchi kwa kukipitisha kifungu hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu asiruhusiwe kumiliki silaha ya moto zaidi ya moja. Ijulikane mtu fulani anamiliki silaha ya aina fulani, basi. Asiruhusiwe kumiliki silaha nyingine, na huyu anayemilikishwa hiyo silaha, anayepewa leseni, kwa kweli achunguzwe kweli kweli tabia zake, mienendo yake, kwa sababu wengine wanakuwa kitu kimo ndani ya moyo hukioni, lakini ukiona ni nani rafiki yake, ma-*group* yake ni yapi? Je, anaweza kweli kudhibiti hasira? Hayo yote yanatakiwa yachunguzwe, vinginevyo silaha zitaangukia mikononi mwa watu waovu wanaozitaka zile silaha kwa nia mbaya. Hili ni jambo la kulidhibiti na kulisimamia kwa hali yeyote ile.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la uhakiki wa silaha lifanyike kila mwaka, anajulikana ni nani amepewa silaha na risasi ngapi.

Kwa hiyo, kila mwaka aende akaripoti nimeshatumia risasi zangu nne kati ya kumi nilizopewa kwa mfano, na hizo nimezitumia kwa matumizi moja, mbili, tatu. Vinginevyo, watakuwa wanatumia wanavyotaka wao, na unajua hatuaminiani kwa sababu waovu wamo humu humu ndani ya nchi. Kusema huyu unamwamini kwa sura yake kumbe yeye mwenyewe ndio mbaya, ana nia mbaya kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasisitiza adhabu iwe ni kifungo tu. Ukisema atoe faini, watu wana mahela chungu nzima na wengine wanapewa hela, kwa hiyo, atalipa tu faini. Lakini apelekwe jela moja kwa moja kwa yule anayemiliki silaha kihalali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namalizia kwa kusisitiza kwamba sheria ni kitu kimoja, usimamizi wa sheria ni kitu kingine. Serikali ya Chama cha Mapinduzi simamieni hii sheria, dhibitini hizo silaha kwa amani na usalama wa nchi yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Kawawa, ajiandae Mheshimiwa Chiligati na Mheshimiwa Augustino Mrema.

**MHE. VITA R. M. AWAWA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipatia fursa hii kuchangia Muswada huu wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi wa mwaka 2014.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nami naunga mkono Serikali kuleta Muswada huu kwa wakati huu. Pia naungana na Kamati ya Ulinzi na Usalama katika maoni yao waliyoyatoa yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inataka silaha lazima isajiliwe. Ni jambo jema, ni lazima isajiliwe na wananchi lazima watambue hili kwamba kuwa na silaha ambayo haijasajiliwa ni kosa la jinai. Kwa hiyo, naunga mkono kabisa eneo hili la silaha kusajiliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia sheria inataka mamlaka iwe moja ya usajili yaani Makao Makuu ya Jeshi la Polisi. Naunga mkono kabisa suala hili na pia Muswada huu unataka silaha zote ziwekewe alama za silaha. Sheria hii inatambua au inatimiza matakwa ya mkataba wa nchi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ambayo inataka kuwepo kwa alama za utambuzi. Pia hatua hii inalenga na itasaidia kuzitambua silaha zinazotumika katika uhalifu ili kujulikana inatoka nchi gani na nani anazi-*possess* zile silaha. Kwa hiyo, naipongeza sana Serikali kwa kuleta sheria na vifungu hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia sheria inataka kuwe na mafunzo kabla mtu hajapewa kibali cha kumiliki silaha. Naunga mkono kabisa hili ila nina ushauri wa ziada, naomba kila baada ya muda, mwaka mmoja au miaka miwili kuwe na utaratibu wa kuwapima wamiliki wa silaha kuwa je, bado wana uwezo wa kumiliki au kuendelea kumiliki silaha ile?

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi binadamu Mwenyezi Mungu ametuumba leo wazima, kesho tunaweza tukachanganyikiwa au anaweza akafanya mambo yoyote mengine. Kwa hiyo, kuwepo na utaratibu wa kila baada ya muda fulani kuwapima wale ambao wamepewa kibali cha kumiliki silaha, bado wana uwezo huo wa kuendelea kumiliki hizo silaha au iwe basi kutokana na akili yao au mambo wanayoyafanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia wenzangu wamezungumzia umri, nashukuru kweli kwa sababu sheria iliyopo sasa hivi ilikuwa imenyamaza kimya, haikusema lolote kuhusu umri, lakini sasa hivi wameweka umri wa mtu mzima au mtu ambaye aliyekomaa kiakili kuanzia miaka 25. Kwa hiyo, nalo nalipongeza sana na ninaliunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu Masjala Kuu ya Silaha. Sheria inataka kuwepo Masjala Kuu ya Silaha itakayotunza *data* ya silaha zote nchini. Masjala hii itakuwepo Makao Makuu ya Jeshi la Polisi, lakini pia kutakuwa na Masjala ndogo Zanzibar ili kuzisajili na kuziangalia silaha zilizoko Zanzibar.

Ushauri wangu ni kwamba Serikali iwezeshe Masjala hii au Idara hii iweze kuwa na vifaa vya kisasa ili waweze kuwa na uwezo wa kutambua haraka silaha inayogundulika popote; huko Namtumbo au Kigoma, kwa wakati huo huo ikionekana silaha ile, ikipelekwa taarifa kwenye Masjala pale Makao Makuu, haraka waweze kutambua silaha hii mwenyewe ni nani na aweze kwenda kuwahiwa na kudhibitiwa, kuliko kuendelea kuwa na mafaili tu na mambo yale ya kizamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaomba sana waweze kusaidiwa, siyo kusaidiwa; kuwezeshwa katika bajeti. Wizara iweke fedha katika bajeti hii baada ya kupitisha sheria kwamba wapatiwe vifaa vya kisasa Idara hii waweze kuwa na vifaa ambavyo wataweza

kutambua haraka wenye silaha hiyo pale taarifa hiyo inapopelekwa na wao waweze kurudisha taarifa ya nani mwenye silaha, yupo eneo gani, haraka iwezekanvyo kutoka kwenye eneo lile walilopata taarifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, yangu yalikuwa ni hayo tu, naunga mkono hoja.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Capt. Chiligati, jiandae Mheshimiwa Mrema na tutamalizia na Mheshimiwa Riziki.

**MHE. CAPT. JOHN Z. CHILIGATI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii nami nichangie Muswada huu uliopo mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote naunga mkono Muswada huu kwa sababu Muswada huu unakuja kwa wakati wake kujibu tatizo kubwa ambalo linaikabili nchi yetu, suala la kuzagaa kwa silaha ndogo ndogo nasuala la uhalifu wa kutumia silaha limeongezeka. Kwa hiyo, Muswada huu unakuja kukabiliana na hili tatizo ndiyo maana na sisi wengine tunauunga mkono na ninaamini Wabunge wote tutaunga mkono.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nimtoe wasiwasi Msemaji wa Kambi ya Upinzani, alikuwa na wasiwasi kwamba Muswada huu umempa madaraka makubwa Msajili atakayekuwa anasajili silaha kwamba huyu anaweza akatumia vibaya madaraka yake akatoa leseni kwa upendeleo, akawanyang'anya wengine leseni kwa kuwaonea tu. Utaratibu utakuwa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, mtu, anaomba kibali cha kumiliki silaha; hatua ya kwanza anajadiliwa na Kamati ya Ulinzi na Usalama katika eneo analokaa. Kama ni Mtaa Mjini au Vijijini, kwa mtazamo huu, Chiligati anaomba kumiliki silaha. Tabia zake zikoje, ndiyo haya mambo ya ulevi, ugomvi, ukorofi au ni mtu wa aina gani, wanakujadili pale. Sasa kama wewe ni mtu wa hovyo hovyo, wewe ni mtu hatari kumiliki silaha, ombi lako linaweza likaishia tu hata kwa Msajili linaweza lisifike.

Kwa hiyo, wakishaona kwamba wewe ni mtu sawasawa, una sifa, sasa ndiyo hatua ya pili unakwenda kupata mafunzo jinsi ya kutumia hiyo silaha. Ukishapata hayo mafunzo na uka-*pass* kwenye majaribio, sasa ndiyo unafika kwa Msajili. Msajili atatazama: Je, wanamsemaje Chiligati kule kwake? Aah, ni mtu mwema huyu. Je, Chiligati ameshapata mafunzo ya kutumia silaha? Amefaulu? Hapo ndipo Msajili anapoingia. Kwa hiyo, suala la Msajili kutoa kwa upendeleo au kumnyima mtu kwa fitina, halipo kwa sababu zipo taratibu mbalimbali mpaka suala lifike kwa Msajili. Kwa hiyo, nilitaka kwanza nitumie nafasi hii kumtoa wasiwasi Msemaji wa Kambi ya Upinzani na Watanzania wengine ambao wanaotusikiliza. Naamini kabisa hizi Kamati zitatenda haki tu, hazitamnyima mtu haki yake kwa sababu yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili, nami niunge mkono suala hili la mafunzo ambayo sasa kabla hujapewa kibali cha kumiliki silaha, utapata mafunzo jinsi ya kutumia hiyo silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, walio wengi wanapata vibali vya kununua silaha, hata kuzitumia hawajui. Watafundishwa jinsi ya kuitumia, watakufundisha jinsi ya kuifanyia *service*. Yaani silaha ni kama gari, kama pikipiki, ni lazima uifanyie *service*, uisafishe, uweke *grease*, ufanyaje*!* Vilevile utafundishwa jinsi ya kuitunza. Watu wengi hawajui jinsi ya kutunza silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, silaha siyo tu kama *pen* unaiweka tu holela, zipo taratibu zake. Wengine wameingia matatani kwa sababu hawajui jinsi ya kutunza silaha, zile silaha

zikachukuliwa hata na watu wengine, watoto, zikafanya uhalifu, unatiwa msukosuko wewe ambaye unamiliki ile silaha. Kwa hiyo, hili suala la mafunzo naliunga mkono kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa wale Wanajeshi wenzangu wastaafu, hii ni fursa kwa sababu huko kwenye kutoa mafunzo itabidi vianzishwe sasa vituo mbalimbali vya kutoa hayo mafunzo kama jinsi ambavyo kuna Shule za Udereva, mtu anakuwa mwekezaji kwenye Chuo cha Udereva, kutakuwa na vyuo vya kufundisha kutumia silaha, kupiga shabaha na vitakuwa vingi katika kila Wilaya, kila Mkoa. Kwa hiyo, ni fursa watu waichangamkie wenye uwezo wa kuanzisha vyuo au vituo vya kutoa mafunzo kama haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tatu nilitaka vilevile nisemee suala la umri. Tulibishana sana na wadau kuhusu umri, kwa sababu baadhi ya wadau walipokuja pale walisema umri uwe miaka 18 kwa sababu ndiyo umri wa kupiga kura. Wengine wakasema hapana, iwe 21, wengine wakasema aah, iwe 30 awe mtu mzima kabisa ameshakomaa, ubishi ukawa mwingi sana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, wale waliokuwa wanasema miaka 18, miaka 20 walikuwa wale ni makampuni ya ulinzi; yakasema sasa sisi tunaajiri vijana wamemaliza *Form Four* hawana kazi tunawaajiri kwenye kampuni zetu za ulinzi. Sasa mnaposema mpaka awe miaka 25 awe miaka mingapi, miaka mingapi, tutafanyaje?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tulitoa ufafanuzi, nataka vilevile nirudie kwamba, kumiliki silaha ni tofauti na ajira ya kutumia silaha. Hii miaka 25 ni ile mtu anataka kuajiri, awe na silaha yake mwenyewe anayo saa 24 nyumbani kwake, hii miaka 25. Lakini yule ambaye ajira yake inahitaji kutumia silaha, yule sio lazima iwe, yule akishafikia umri wa kuajiriwa basi ataajiriwa, lakini yule ile silaha hakai nayo nyumbani kwake saa 24; wakati wa lindo wakati wa kazi atakuwa nayo tena chini ya usimamizi, baada ya kazi anairudisha kule alikoichukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ndio maana baadaye tukaja kwenye hii miaka, tukakubaliana miaka 25. Na nadhani miaka 25 kijana hata kama alikuwa amemaliza Chuo Kikuu, ameshamaliza, ana familia yake ni mtu ambaye anaaminika kumiliki silaha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka niseme hayo tu, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mheshimiwa Mrema, jiandae Mheshimiwa Riziki dakika tano na Mheshimiwa Haji Kombo dakika tano.

**MHE. AUGUSTINE L. MREMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Muswada huu muhimu.

Mimi nakubaliana kabisa na mapendekezo ya Serikali kutokana na kwamba, silaha zimezagaa ndani ya nchi na pia nje ya mipaka yetu; silaha ni nyingi na vikundi vya wahalifu vipo. Kwa hiyo, hili la kusema silaha zisajiliwe naona ni sahihi. Haiwezekani tukawa na silaha zimetapakaa ndani ya nchi, halafu hatujui ni ngapi, hatuzifahamu! Hilo la kwanza, naliunga mkono nasema hapa tumefanya vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili naunga mkono suala la kwamba, silaha ziwekewe alama. Haiwezekani tukapata bunduki hapa na hatujui imetokea Congo, imetokea Zaire au imetokea Rwanda, Burundi, kwa hiyo, zifahamike, ziwekewe alama; naunga mkono hoja hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya tatu ambayo ndio nitaomba hili Bunge lisaidie, ni kuhusu wale watu ambao tayari wanazo silaha sasa hivi; hawakupata mafunzo na inawezekana umri wao wa miaka 25 wameshapita ule umri, sawasawa, lakini watu hawa ni wakorofi katika jamii, wanatumia silaha zile kuwatishia watu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina mfano mzuri hawa watu wenye silaha lakini wana mgogoro na jamii, kwenye Jimbo la Vunjo Meresini, Kitongoji cha Meresini, kuna mgogoro ambao Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi anajua, kwamba, yale mashamba ya mkonge yalivyogawanywa, wanakijiji pale matatizo yao, haki zao hazikuzingatiwa; wamepewa watu wenye uwezo, watu wenye pesa. Hili shamba lilikuwa la mkonge, lilikuwa la Serikali, hawa wagawaji hawakufuata shida za watu wa pale.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa juzi mimi nilikuwa Dar es salaam nakuja Bungeni, ikabidi nirudi Himo, nirudi Vunjo kwa sababu kulikuwa na mgogoro mkubwa kati ya mwekezaji mmoja pale anawekeza kiwanda cha redio, sio kiwanda, kituo cha redio.

Wananchi wanasema haiwezekani eneo hili tuna shule yetu ya *Form Four* tunataka kujenga *Form Five* na *Form Six,* tutajenga wapi? Hatuna viwanja vya kuchezea watoto wetu, hatuna soko, hatuna Mahakama hapa! Inawezekanaje eneo hili mkawapa watu wenye pesa, watu wachache, sisi tutakuwa wakimbizi hapa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, huyo mwekezaji alivyokuja pale kupanga matofali yake anataka kujenga bila huo mgogoro kutatuliwa, kukatokea mgogoro mkubwa sana na wananchi; wanamwambia haiwezekani, Mbunge alikwishafikisha suala letu Bungeni na Waziri wa Ardhi alikwishakubali kwamba, kama ugawaji ule haukuzingatia mahitaji ya wanakijiji wa Meresini, nitakuja.

Sasa, Waziri aliyekuweko wa Ardhi ameondoka kachaguliwa Waziri mwingine. Sasa nikamwambia mimi narudi kule Himo kuna vita kuna mapambano, watu wangu wasije wakauawa! Wakiuawa nani atanipigia kura, na mimi nataka Ubunge wangu niendeleenao? *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ninalotaka kusema hapa, kuna watu tayari, huyo mwekezaji ana silaha, wananchi wamefika pale yeye amefyatua risasi hewani, sijui angani, sijui anawatishia! Sasa katika mazingira kama hayo Serikali inajua pale kuna mgogoro na Waziri ameishasema nitafika; mtu mmoja ana silaha za kuwatisha wale wananchi! Itakuwaje katika mazingira kama hayo?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nilikuwa napendekeza hapa mnisaidie ule mgogoro wa Meresini. Yule mwekezaji aulizwe kwa nini alitumia silaha, risasi zile kwenye kundi la watu? Alitaka kufanya nini? Kwa nini anawatishia hao wananchi? Je, alipewa hiyo silaha kwa ajili hiyo? Kwa madhumuni hayo? Je, Serikali ilikwishampa mafunzo, anajua namna ya kuitumia na ataitumia wakati gani? Au ukishapewa silaha unaweza kutishia nayo watu, unawahangaisha watu?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema Muswada huu wa Kudhibiti Silaha, nimeufurahia sana, lakini ninachosema asipewe mtu silaha aliye na umri wa chini ya miaka 25, sawa. Lakini kuna watu ambao tumekwishawapa silaha kama yule wa Meresini, yule anasumbuaana na wale wanakijiji! Ni mtu mkorofi, ni mtu ambaye hatambui haki za jamii! Itakuwaje? Ataendelea na hiyo silaha mpaka lini? Je, Polisi imechukua hatua? Inawezekanaje mtu akafyatua risasi ya bastola yake, sijui kama ni angani au alikuwa analenga watu fulani!

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, mimi nasema naunga mkono huu Muswada ni mzuri. Na hata mapendekezo kwamba, uanze kutumika mwezi Julai, naona Julai ni mbali, ungeanza sasa hivi, kwa sababu hata sisi kuna watu wanatishia maisha, majambazi kule wanavizia biashara za watu wanaenda kuwatisha wakati mwingine wanawajeruhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ninachoomba nataka majibu; yule mtu aliyefyatua risasi kwenye kundi la watu pale Meresini siku 5 zilizopita! Polisi hawajamkamata! Polisi hawajamhoji! Wale wanakijiji wataishi katika mazingira gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, Waziri wa Ardhi hajaja pale! *Message* yake ninayo kwamba atakwenda! Je, wakati huu ambapo huyo Waziri wa Ardhi hajaenda, ile silaha ambayo yule bwana anatembea nayo kwenye nyumba za watu, kwenye vilabu vya pombe na kuwaonesha kwamba, mkipambana na mimi nitawakomesheni! Kama hilo litapatiwa majibu, mimi nitashukuru sana, lakini namalizia kwamba, naunga mkono hii hoja ni hoja nzuri. Ahsanteni.

**MHE. RIZIKI OMAR JUMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi nichangie machache.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la kwanza ambalo nataka niliseme ni kwamba, huu Muswada au hii Sheria sio mbaya kama itasimamiwa ipasavyo. Lakini naomba niseme kwamba, nianze na kwenye suala la *fine*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la *fine* halifai kabisa katika Muswada huu katika Sheria hii, halifai kabisa! Anayekamatwa kaenda kinyume na Sheria hii basi lazima kifungo kiwe ni adhabu peke yake kuliko suala la *fine*. Kuna matajiri, kuna watu wenye uwezo mkubwa, watakuwa wakifanya mambo mabaya, maasi, wakiumiza watu bila kuchukuliwa hatua yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, ambalo nataka niliseme ni kwamba, naunga mkono kuondolewa kwa suala la matumizi ya silaha hizi bandia. Hazifai, naomba zisiruhusiwe kabisa! Hizi silaha bandia watu wanazitumia vibaya, sikubaliani nazo kabisa katika Muswada huu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la tatu, suala la udhibiti wa silaha. *PGO* ipo muda mrefu! Yaani Sheria ya Udhibiti hii ipo muda mrefu, lakini inaonekana udhibiti hauko sawa! Sijui tunaelekea wapi hata leo tunaleta Muswada huu! Kama usimamizi utakuwa upaswavyo na udhibiti utakuwa wa kweli kweli kwa nia thabiti, basi nina imani kwamba tutaelekea pazuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini je, tujiulize silaha hizi ambazo zinaingia nchini mwetu kinyume na sheria, kinyume na utaratibu, zinapita wapi? Tuna ulinzi wa kutosha, tuna Jeshi la Polisi, tuna Uhamiaji, tuna Jeshi la Wananchi, tuna vitengo vingi tu vya ulinzi, lakini je, silaha hizi zinapita wapi? Na sasa tunaleta sheria hii, je, tutaweza kuondoa yale madhara ambayo yalikuwepo zamani? Askari wetu wanaonekana hawako sawa hawafanyi kazi zao ipasavyo!

Mheshimiwa Mwenyekiti, haiwezekani kuwa silaha hizi zinapita mipakani! Ni sawasawa na dawa za kulevya, siku zote tunapiga kelele dawa za kulevya, lakini tukitizama nchini zinaingia! Zinapita viwanja vya ndege, zinapita baharini, zinapita kila eneo, kila milango zinapita, na bado tunaendelea kulalamika dawa za kulevya! Kwa hiyo, ni sawa na hili suala la silaha haramu zinazoingizwa nchini ambazo zinakuja kuwaangamiza wananchi siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini jambo linguine, hawa askari wetu, hizi silaha ambazo kila siku wanakamata zinaendea wapi? Hawatutangazii wamekamata ngapi, wamechukua hatua gani, nani na nani kachukuliwa hatua! Hatujui kinachoendelea, hatujui zinaishia wapi!

Inawezekana hizi hizi kinyume chake ndio zinazogeuka zikarudi zikaingia mikononi kinyume na utaratibu! Kwa hiyo, naomba sana sheria hii izingatie kwa umakini mkubwa suala hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vituo vya polisi vinatekwa, vinavamiwa ovyo ovyo! Ni kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini moja ambalo linachangia, naomba turekebishe, hivi vituo vyetu vya polisi tunampa askari polisi, pengine yuko peke yake au wako wawili, kituo kiko pengine kimejitenga katika eneo fulani, kibovu, hakina mazingira mazuri! Kwa hiyo, ni rahisi kuingia watu haramu wakawavamia, wakachukua silaha zikaenda kuwahujumu wananchi wetu, zikaenda kufanyia maasi mbalimbali! Kwa hiyo, Muswada huu kama utazingatiwa kweli na utafanyiwa kazi na utasimamiwa ipasavyo, basi unaweza kutuondolea mazito haya ambayo yanawakabili Watanzania ambayo yanaendelea siku hadi siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini lingine; Jeshi la Polisi, Jeshi la Wananchi, imekuwa ni mchezo wa kawaida kwamba, panapofanyika maandamano, wao badala ya kuwa walinzi wa raia, kwa kutumia hizo silaha, lakini maandamano, mikutano, wana uwezo wa kuzuia kwa njia thabiti kabisa, kwa njia halali kabisa! Lakini kinyume chake unakwenda unamkamata raia, tayari umeishamtia mkononi, raia ni kumshika nguo tu ukamburura ukampeleka kunakohusika kwenye chombo cha sheria; lakini mpaka umpige, mpaka umuue, umdhalilishe kiasi ambacho unamletea madhara makubwa katika maisha yake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba sana hata hawa walinzi wetu nao wasitumie silaha vibaya! Watumie silaha kwa mujibu wa sheria na utaratibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru sana. Kwa sababu, mawazo yetu ni madogo sana, mimi nafikiria silaha ndogondogo hizi ziuzwe madukani. Unapouza dukani unazi-*control,* ununuzi wake unakuwa unafahamika nani amenunua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukisema unadhibiti, leo silaha chungu nzima zinaingia bila ya kufahamika! Tutapata mapato, *TRA* watapata mapato kutokana na maduka ya silaha ndogondogo hizi bila matatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mimi mara yangu ya kwanza kusikia bunduki inalia ni mwaka 2001 kwenye maandamano yale ya Chama Cha Wananchi – *CUF,* ndio nasikia bunduki inalia buu! Na niliposikia hivyo nikatoka nikachungulia nikaona kumbe wanaopiga bunduki zile ni Polisi, na wakaua watu wengi!

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadaye tukapata habari kwamba na askari wengine walikuja kutoka Bara, wengine walitoka wapi, kwenye vita hivyo ambavyo Zanzibar mpaka leo kuna sheria raia haruhusiwi kuwa na silaha. Mpaka hivi ninavyozungumza, raia wa Zanzibar hana haki ya kuwa na silaha. Sasa leo anakuja mtu anakwambia tumeuwa hawa kwa sababu walikuwa wanakwenda kwenye vituo vya polisi kwenda kutafuta silaha! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, inanisikitisha sana ndugu zetu wamekufa! Wazanzibari wamekufa, anakuja mtu mmoja mjinga tu anakuja kuzungumza suala hili la 2001, kutia aibu nchi yetu kwamba, tuliuwana!

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa vitendo hivi ilivyo, tunahitaji na sisi tupate silaha sasa mfukoni mwetu, polisi kakuuwa na wewe unampiga! Kwa sababu silaha ya polisi waliotuuwa ni silaha ambayo nimeinunua mimi kwa mchango wangu wa kodi ya nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunakuja kwenye Bunge hili lenye heshima, anakwambia mtu, oo, kwa nini mnasimama mnataka kufanya sijui, aa mnataka kuchukua. Ah jamani, miaka 10, nyie Wazanzibari bado mna *policy* za kijinga kama hizi! *10 years!* Badala ya kukaa mkafikiria tutaishi vipi kwa pamoja! Tutaishi vipi, nyie mnazungumzia mambo ya kipumbavu! Halafu anasema mtu *with confidence,* oh, walitaka kuteka nyara vituo vya polisi! Unateka nyara kituo gani? *Geography* ya Zanzibar nani aliyekuwa haijui? Ee, jamani! *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naomba sana, bado dakika yangu moja, lakini naomba sana turuhusiwe silaha ndogondogo ziuzwe madukani na zitakapouzwa madukani tutapata kodi, tutaendeleza maisha yetu. Tutakapouza madukani tutaweza kuwa-*control* wanaonunua! Sio hii njia ya leo zinayokuja!

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo zinaingia silaha wengine wanaingia nazo anayetaka ananunua! Hazitusaidii, zinatupa matatizo, hata zile hatulipii kodi zinaingia ndani! Leo ukitaka silaha, kama Mbunge wa Zanzibar ana silaha, basi huyo Mbunge anahitajika arejeshe kwa sababu…

**MWENYEKITI:** Ahsante.

**MHE. KOMBO KHAMIS KOMBO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Waheshimiwa Wabunge, wachangiaji wetu wote kwenye orodha hii ya leo tumewamaliza. Jioni, Saa 11:00, Mheshimiwa Spika mwenyewe ndiye atakayekuwa kwenye Kiti na kwa hiyo, Serikali mjiandae majibu na hatua zitakazofuata kwa maelekezo ya Kiti.

Waheshimiwa Wabunge, Frank K. Mbumi, kwa niaba ya Katibu wa Bunge anaomba kuwatangazia Wabunge wa Madhehebu ya *CCT* kwamba, leo tarehe 19 Machi, kutakuwa na ibada mara tu baada ya kuahirisha Bunge, mchana. Haisemi ni wapi! Sasa, labda wiki iliyopita mnajua mlifanyia wapi kwa hiyo, mtajielekeza hukohuko. Sina matangazo mengine! Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11:00.

*(Saa 7.00 Mchana, Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alikalia Kiti*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Waziri, Bunge linaanza saa kumi na moja kamili, kwa hiyo, hiyo ni saa ya kuingia Spika, siyo saa ya kuingia hata watoa hoja.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa nilizonazo ni kwamba kipindi cha asubuhi wote walioomba walipata nafasi. Kwa hiyo, sasa hivi ni moja kwa moja anaingia mtoa hoja kutoa ufafanuzi kwa hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge. Mheshimiwa mtoa hoja, una dakika 60.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kukushukuru wewe na Kamati ya Kudumu ya Bunge chini ya uongozi wa Mwenyekiti Mheshimiwa Anna Abdallah kwa mchango na ushauri ambao umeendelea kutolewa kwa Wizara yangu hadi kufikia hatua hii tunaendelea kujadili Muswada huu wa Sheria ya Udhibiti wa Silaha.

Naomba pia nichukue nafasi hii kumshukuru Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Godbless Lema kwa maelezo ambayo aliyatoa, maangalizo na ushauri mbalimbali kwa nia *(I hope)* safi ya kudumisha amani ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu umechangiwa na Waheshimiwa Wabunge 15 kwa jumla, 13 wamechangia kwa mdomo na wawili wakachangia kwa maandishi. Naomba niwashukuru wajumbe wote hawa na hata wale ambao hawajachangia kwa sababu mchakato bado unaendelea, *I hope* tutapata busara zao kwenye kuikamilisha sheria hii.

Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia kwa maoni, naomba niwaahidi kwamba maoni yao tumeyachukua na kama nitakavyoelezea baadae basi yatakayobakia tutaendelea kuyafanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nianze kujibu hoja mbalimbali zilizojitokeza wakati wa michango au taarifa za Kamati ya Ulinzi na Usalama na baadae Kambi ya Upinzani na hatimaye nitazungumza ikiwa muda utatosha kutoa ufafanuzi wa michango ya wajumbe mmoja mmoja.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwenye taarifa yake, lakini hata kabla ya hapo, imekuwa mchangiaji mkubwa katika kuiboresha sheria hii na naomba niwashukuru sana.

Miongoni mwa michango iliyotoka kwenye taarifa yao ambayo leo nataka niitolee ufafanuzi ni kuhusu kifungu cha 20 kinachohusu adhabu kwa mtu anayepatikana kwa kosa la kumiliki silaha kinyume na sheria. Kamati inapendekeza adhabu ya kifungo cha miaka mitano na isiwe na faini. Pendekezo hili litaonekana baadae kwamba tumelizingatia kikamilifu tutakapopitia jedwali la marekebisho na hiki kipengele kipo kwenye kipengele (n) cha jedwali hilo.

Mheshimiwa Spika, pia walichangia kifungu cha 26(1) na Kamati ikapendekeza kifungu kidogo (g) kwamba mtu ambaye atamilikishwa silaha asiwe chini ya umri wa miaka 25. Pendekezo hili pia ni zuri kama lilivyothibitishwa na baadhi ya Wabunge na tunalichukua moja kwa moja na litaingizwa kwenye sheria kama itakavyoonekana.

Mheshimiwa Spika, kifungu cha 62(2) Kamati ilipendekeza adhabu ya kifungo kisichozidi mwaka mmoja kutoka miezi miwili ambayo ilikuwepo. Naomba niwahakikishie Wajumbe wa Kamati hii pamoja na Bunge lote tukufu kwamba mapendekezo haya yamezingatiwa kwenye jedwali letu la marekebisho kipengele (w).

Jambo lingine ambalo Kamati ilichangia ilikuwa ni kifungu cha 5(3) ambapo walipendekeza kifungu kinachosema Mjumbe wa Kamati awe raia wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania hili ni pendekezo zuri na kwa kweli tumelichukua, tumeliingiza kwenye marekebisho ambayo yatakuja mbele yenu baadae.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie hoja ambazo zimetoka Kambi Rasmi ya Upinzani. Hoja ya kwanza ilikuwa kwamba, mamlaka ya msajili wa silaha kifungu cha 8(2) na kifungu cha 17(1) na (2) kinampa mamlaka ya kutoa na kufuta kibali na hakijatoa mwongozo wa mipaka ya utekelezaji wa kazi hiyo.

Namshukuru Mheshimiwa Chiligati wakati alipopata nafasi ya kuchangia kama Mbunge alitoa ufafanuzi wa hoja hii. Ukweli ni kwamba uchambuzi wa nani apewe kibali au leseni

unaanza kwenye mitaa tunayotoka, kwa hiyo, sio mamlaka makubwa kwa msajili kwa sababu yeye atachukua mapendekezo ambayo tayari yamefanyiwa kazi.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ni watu ambao wanahisiwa hawana sifa ambayo ni kifungu 26(1) cha Muswada kinachohusu orodha ya mambo au tabia zinazoweza kumkosesha mtu kumiliki silaha ikiwemo tabia ya ukorofi. Upinzani Rasmi ulikuwa na shaka na hili na kupendekeza kwamba liwekwe wazi zaidi.

Mheshimiwa Spika, neno ukorofi limeshatafsiriwa kwenye sheria mbalimbali ikiwemo Kanuni ya Adhabu Sura ya 16, Sheria Inayosimamia Amani katika Jamii *(Public Order Management Act)* ambazo zote zinatumika na sheria hii kwa pamoja. Kwa hiyo, kwa ajili ya tafsiri hili halina utata.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kwenye kifungu 26(2) kinachozungumzia muda wa kutoa *notice* kwa mtu aliyepoteza sifa ya kumiliki silaha, muda na mahali vitajwe rasmi kwenye sheria. Ushauri huu umepokelewa na utazingatiwa katika uandishi wa sheria hii.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kifungu cha 26(3) kinachozungumzia mtu kupoteza uwezo, leseni na kibali. Sifa ya kumiliki silaha haina vigezo vingi ambavyo mtu anaweza kuvipoteza vyote wakati mwingine, hivyo ni muhimu mtu kufanyiwa tathmini ya vigezo hivyo mara kwa mara ili kugundua kipi ambacho kinamkwaza na pengine kumshauri afanye nini kabla hajavipoteza vyote.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge, kifungu cha 26(4) kinazungumzia usalimishaji wa silaha na nyaraka zake kituo cha polisi. Kambi Rasmi inahofu kwamba hayo ni matumizi mabaya ya sheria yanayoweza kutumika kunyang'anya haki za raia kumiliki silaha.

Mheshimiwa Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kanuni zitakazotungwa zinatarajia kuweka utaratibu wa kisheria wa kusalimisha silaha na nyaraka zake na pia kukata rufaa kwa mtu ambaye hakuridhika na hatua zilizochukuliwa na msajili wa silaha.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ni kifungu cha 29 kuhusu utoaji na usafirishaji wa silaha na risasi kutoka ghala la umma na kutoa kituo cha polisi. Kambi Rasmi inashauri kuwe na ugatuzi wa madaraka ili kibali kitolewe kwa Wakuu wa Polisi wa Mikoa. Kifungu hiki kinaruhusu usafirishaji wa silaha nyingi na kwa umbali mrefu hasa kutoka Mkoa mmoja hadi mwingine. Aidha ushaUri wa Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani utazingatiwa kwa usafirishaji wa silaha katika eneo moja lililo jirani.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kwenye kifungu cha 33 kinachoruhusu masharti ya wauzaji silaha yatakayotolewa na Waziri. Kambi ya Upinzani inataka masharti hayo yaainishwe kwenye sheria. Ni utaratibu katika utungaji wa sheria kwamba mambo mengi ya kiutendaji huwekwa kwenye kanuni ambazo Waheshimiwa Wabunge wana nafasi pia za kuzitolea maoni.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ya Kambi ya Upinzani inahusu msajili kutochukuliwa hatua kwa utekelezaji wa majukumu yake atakayofanya kwa nia njema. Utekelezaji wa majukumu kwa nia njema ni kigezo cha kisheria kinachopimwa kutokana na matendo ya mtu anayetekeleza wajibu wake. Hivyo basi hakuna sababu ya kuwa na shaka na utekelezaji wa majukumu ya msajili atakayoyafanya kwa nia njema.

Mheshimiwa Spika, mwisho kwa upande wa Kambi ya Upinzani, wanasema Wabunge wawe na haki ya kuomba na kumiliki silaha bila kupitia hatua za kujadiliwa kwenye Kamati za Ulinzi na Usalama. Naomba niseme kwamba maombi ya mtu kumiliki silaha kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama yanasimamiwa na Sheria ya Baraza la Taifa la Usalama. Sheria hiyo inaainisha vigezo na taratibu za kupitisha maombi. Hata hivyo, kwa sababu hili linawezekana pia kutazamwa kiutawala, basi tutaendelea kulijadili tuone vipi tunaweza kulishughulikia.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba nizungumzie hoja moja moja ambazo walichangia Waheshimiwa Wabunge. Hoja ya kwanza ilikuwa kuhusu adhabu ya raia wanaomiliki silaha kinyume na sheria. Wachangiaji wakubwa walikuwa Mheshimiwa Mipata, Mheshimiwa Ngonyani, Mheshimiwa Riziki Omary na Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim. Mapendekezo haya kwa kweli tumeyachukua moja kwa moja na niwahakikishie kwamba wakiipitisha sheria hii watakuta mapendekezo yao yako humo ndani.

Mheshimiwa Spika, hoja ya pili ilikuwa kudhibiti silaha mipakani. Ni kweli kwamba mipaka yetu ni mirefu na iko *porous* na pamoja na mambo mengi yanayofanywa, bado tunaweza tukawa na matatizo ya kuingiza silaha na nchi jirani. Pamoja na hilo, Serikali itajitahidi kuhakikisha kwamba inaweka taratibu za kudhibiti silaha kwa sababu tumeshaona matatizo yake lakini pia niwaombe wananchi wa mipakani wazidishe uzalendo na ushiriki wao ili kupata taarifa za watu wanaopitisha silaha ambazo nina hakika zitatusaidia sana katika kuimarisha juhudi za Serikali za kudhibiti silaha sehemu hizo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwa na suala la vipi Zanzibar wananchi kule hawaruhusiwi kumiliki silaha. Ni kweli kwamba sheria iliyopita na hata hii inaweka vikwazo kwa Zanzibar kumiliki na kutembea nayo. Pamoja na hivyo ni kwamba mambo haya ya kumiliki silaha kwa upande wa Zanzibar yanaonekana Serikali ya kule bado inahitaji uwepo udhibiti huo na kwa vyovyote vile mabadiliko ya sheria hii au utaratibu huu unatakiwa uanzie Zanzibar. Baada ya Zanzibar kama Serikali kusema kwamba imeondoa hiyo hofu, basi sheria zitafanyiwa mabadiliko ili na kule mtu aweze kuingia na silaha bila tatizo.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kuhusu umri wa kumiliki silaha. Imechangiwa na Wabunge Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim, Mheshimiwa Masele na Kapteni Chiligati. Pendekezo hili kama yalivyo mengine tumelichukua na tumeliingiza kwenye kifungu cha 11(1)(a) kwenye sifa za mtu ambaye anatakiwa amiliki silaha.

Mheshimiwa Mussa Haji Kombo alitaka maduka ya silaha yaendelee kuwepo na silaha zinunuliwe *super market.* Nafikiri ni ushauri ambao tutautazama, lakini nakaribia kusema ni ushauri ambao unaweza ukaporomosha jitihada zetu. Kwa hiyo, tukiona mazingira yanaruhusu ushauri ni ushauri tunaweza tukapata mahali tukaufanyia kazi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mipata pia alihoji uwingi wa maduka, kwa hiyo, kwanza kuna ukinzani wa mawazo haya na kwa vyovyote vile sisi tunafikiri kwamba udhibiti wa wauzaji silaha utatusaidia kupunguza uhalifu.

Mheshimiwa Spika, halafu kulikuwa na hoja ya wahunzi. Kuna watu wa vijijini ambao wana utaalamu huu wa kutengeneza silaha wenyewe. Ni jambo la kujisifia, lakini ni lazima nalo tuli-*regulate*. Mheshimiwa Mipata, Agustino Manyanda na Mussa Hassan Mussa walizungumzia habari hii.

Mheshimiwa Spika, kiutaratibu na kimsingi sheria hii haiwazuii watu ambao wana *talents* kama hizo kuweza kuzikuza na pengine tukaweza *one day* zikatusaidia kwamba Tanzania tunatengeneza silaha kinachosemwa hapa ni kujaribu kuyaweka mawazo yao, vipaji vyao

kitaasisi ili tuweze kuvikuza, kuvisimamia, kuviboresha na hatimaye vitusaidie zaidi lakini pia tukijua kwamba nani ana ujuzi gani na uko wapi.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kuhusu wajumbe ya kamati ya usimamizi wa silaha. Hoja hii aliitoa Mheshimiwa Kidawa Salehe na kwa kweli ni ushauri tumegundua ni mzuri na kwa kuanzia tunapendekeza kwamba tuwaongeze wajumbe wawili kutoka Zanzibar ambao watatoka kwenye Wizara ya Tawala za Mikoa na Serikali na Vikosi vya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa usalimishaji wa silaha kwa hiari. Mheshimiwa Mipata alitoa ushauri kwamba hili jambo tulifanye liwe endelevu. Nafikiri hili jambo ni endelevu na tutaendelea kulitumia siku zote ili tuhakikishe kwamba silaha zinatoka kwenye mikono ambayo siyo salama na zinarudi kwenye mikono ambayo iko salama.

Mheshimiwa Mbassa alishauri kwamba, wanaosalimisha silaha kwa hiari wasisumbuliwe, na sisi tunakubaliana naye kwamba ni jambo nzuri na ni sehemu muhimu katika ku-*manage* uzagaaji wa silaha na kwa hiyo, tutahakikisha kwamba, silaha zinazowasilishwa wakati wa *amnesty* tunazichukua kama silaha ambazo zimekuja kwetu kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa ni kuhusu wawekezaji ambao wanatembea na silaha na pengine hawajapatiwa elimu. Hoja ya Mwekezaji ambaye ametishia watu kwa silaha sehemu za Vunjo ambayo ni ya Mheshimiwa Augustino Mrema, naomba nimwambie Mheshimiwa Mrema kwamba hilo ni kosa la jinai na namshauri moja kwa moja asilizungumzie kwenye sheria ambayo tunaitunga, ajue kwamba kuna sheria tayari zinaweza zikamtia hatiani huyu mtu ambaye amefanya hivyo vitisho kwa wananchi. Kwa hiyo, tunachoomba, hizo taarifa zipelekwe kwa taasisi husika ili zifanyiwe kazi mapema kabla sheria hii pengine haijaanza kutumika.

Mheshimiwa Spika, lingine ni masjala ya silaha. Mheshimiwa Vita Kawawa alishauri kwamba tunapoianzisha, basi tuhakikishe kwamba tunaipatia vifaa vya kisasa ili shughuli zake ziwe nzuri na ziwe za haraka na kwa ufanisi mkubwa. Ushauri huu tutauzingatia na hasa wakati wa bajeti. Niwaambie tu Waheshimiwa Wabunge, ikishapita hii sheria, watakapokuja wakati wa bajeti, basi wajue kwamba masjala zinahitaji vifaa vya kisasa, basi wapatiwe hizo fedha ili mapendekezo haya yasiende patupu.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ni silaha bandia. Kuna silaha ambazo tayari zinaonekana zimeishatumika katika uharifu mbalimbali na pia zinatishia kwamba ni silaha za kweli kwa sababu ni za bandia, lakini zinaonekana kama ni silaha hasa.

Tulichokipendekeza kwenye sheria hii ni kuhakikisha kwamba uingizaji na matumizi ya silaha bandia ni kwamba haziruhusiwa, pale zitakapokamatwa basi zitakuwa ni kosa chini ya sheria hii. Haya yalikuwa mawazo ya Mheshimiwa Riziki Omari.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilikuwa kuhusu silaha zinazokamatwa katika matukio mbalimbali zinapelekwa wapi, Mheshimiwa aliuliza. Katika uwasilishaji wangu hapa asubuhi nilitoa orodha ya matukio mbalimbali ya kuteketeza silaha. Mara nyingi au mara zote silaha hizi huwa au zinachomwa moto au zinasagwa sagwa kwenye maeneo ya wazi ili kila mtu aweza kuona; na ushahidi upo wa kufanya hivi katika matukio mbalimbali na sehemu mbalimbali mikoani na Dar es salaam yameishafanyika.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nizungumzie wachangiaji wawili ambao walichangia kwa maandishi. Kwanza, ni Mheshimiwa Haji Juma Sereweji, Mbunge wa Mwanakwereke,

alisema kwamba na akatushauri kwa hisia kwamba kwa mawazo yake silaha kumilikiwa Zanzibar bado haujafika wakati na ni vema tuliangalie jambo hili kwa umakini.

Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema pale mwanzo ni kwamba hili jambo ni nyeti na itabidi tuliangalie mpaka pale tutakaporidhika kwamba Zanzibar yenyewe iko tayari kubadilisha utaratibu ambao upo sasa, basi tunaweza tukapanua wigo. Hakuna sababu ya kuwa wengine wanapata na wengine wakose hilo halipendezi, lakini lazima tutii mamlaka ambazo zipo.

Halafu akasema pia, kwamba wamiliki haramu wa silaha wapewe adhabu ya jela miaka mitano bila faini. Kama nilivyosema pale mwanzo, Wabunge wengi waliunga mkono wazo hili na tukiendelea kuwa pamoja basi itakuwa ni uamuzi wa Bunge letu na itakuwa ni sheria kamili ambayo tumekubaliana tuiweke hivyo.

Mheshimiwa Spika, Mbunge mwingine aliyechangia kwa maandishi alikuwa Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo ambaye alikuwa na hoja tatu: Ya kwanza, Jeshi la Polisi lihakikishe kuwa watu wanaoomba kumiliki silaha wanakidhi vigezo vyote hususan kupata mafunzo ya kijeshi na kuzingatia tabia. Maoni ya Mheshimiwa Chilolo hayako peke yake, kuna mengi ambayo yalikuwa yanaelekea huko na kama nilivyosema pale mwanzoni, ushauri huu ni kwamba tumeuchukua na tayari uko kwenye kifungu cha 11 na 12 cha Muswada huu.

Hoja yake ya pili ilikuwa majambazi kutumia silaha na sare za kijeshi. Katika sheria hii inayopendekezwa kutungwa, *Inspector General* wa Polisi amepewa mamlaka ya kusimamia utendaji kazi makampuni ya ulinzi, ikiwemo silaha na sare zao. Tunaamini tu kwamba Kamishina *General* ataendelea kuifanya kazi hii vizuri na kuhakikisha kwamba nchi inaendelea kuwa salama kwa kusimamia haya ikiwa ni sehemu ya majukumu yake kwa wigo mpana.

Wazo la tatu la Mheshimiwa Diana lilikuwa ni mafunzo ya Askari Kujenga Taifa kutolewa kwa wahitimu kuanza kidato cha nne na kuendelea na pia mafunzo ya askari mgambo kuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, ushauri huu nao tunaupokea hata hivyo, suala la mafunz, na umri ni jambo nje kidogo ya waraka huu mbali na kufikiria kwamba nani apewe silaha na nani asipewe kwa mujibu wa umri wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kwa mara nyingine nikushukuru wewe kunipa nafasi hii na niwashukuru Wabunge wote ambao wamechangia na wale ambao michango yao wanatunong'oneza, wametusaidia sana katika kufanya marekebisho ya kuimarisha sheria hii na nawashukuru tena.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**SPIKA:** Hoja hii imeungwa mkono, hatua zinazofuata, tunaingia Muswada unaofuata kwa sababu *quorum* haitoshi kufanya maamuzi.

**MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI**

***Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa Mwaka 2014***
***(The Immigration [Amendment] Bill, 2014***

*(Kusomwa Mara ya Pili)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji Sura 54 sasa usomwe kwa mara ya pili.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutujalia afya njema na kutuwezesha kushiriki katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa wa Bunge lako Tukufu tukiwa wazima.

Aidha, kwa masikitiko makubwa napenda kuungana na wewe Mheshimiwa Spika, Kamati ya Maendeleo ya Jamii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kutoa pole nyingi za dhati kwa familia, ndugu na jamaa wa aliyekuwa Mbunge mwenzetu Marehemu Kapteni John Damian Komba, kwa kifo cha ghafla kilichotokea tarehe 28 Februari, Jijini Dar es Salaam. Mungu aipokee roho yake na ailaze pema peponi, amin.

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa chini ya Mwenyekiti Mheshimiwa Edward Lowassa na Kamati ya Bunge ya Ulinzi na Usalama chini ya Mheshimiwa Mwenyekiti Anna Abdallah kwa ushirikiano wao mkubwa waliotuonesha katika maandalizi ya Muswada huu muhimu kwa Taifa letu. Pia, napenda kuwashukuru wadau mbalimbali walioshiriki kutoa maoni yao kwa lengo la kuboresha Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unawasilishwa katika Bunge lako Tukufu kwa mara ya pili. Idara ya Uhamiaji ni moja ya vyombo vya ulinzi na usalama inayotekeleza majukumu yake kwa kuongozwa na sheria mbalimbali za nchi ikiwemo Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995, Sura ya 54. Sheria hii inatoa mwongozo katika kusimamia shughuli za uingiaji, ukazi na utokaji nje ya Tanzania kwa raia na wageni. Aidha, sheria hii haina masharti yanayosimamia mamlaka ya kiutawala, uwajibikaji na nidhamu kwa watumishi wa Idara ya Uhamiaji kada ya askari.

Mheshimiwa Spika, kabla ya mwaka 2007, watumishi wa kada hii walikuwa wanasimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 8 ya mwaka 2002 ambapo masuala mbalimbali yanayohusu utumishi wao yalikuwa yameainishwa humo. Mnamo mwaka 2007 watumishi hawa wa kada ya askari waliondolewa katika kusimamiwa na Sheria ya Utumishi wa Umma na hivyo wamekuwa hawana sheria inayowatambua katika kusimamia masuala yao ya kiutumishi.

Mheshimiwa Spika, hali ilivyo sasa, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, ilifanya marekebisho katika muundo wake uliopitishwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 9 Oktoba, 2010. Katika marekebisho hayo muundo wa Idara ya Uhamiaji ulipandishwa hadhi kutoka *Division* ya Uhamiaji na kuwa Idara ya Uhamiaji. Hii ni kutokana na kuongeza na majukumu na shughuli za kiuhamiaji kitaifa, kikanda na kimataifa. Vilevile idara hii imepewa hadhi ya kiuaskari.

Mheshimiwa Spika, baada ya Idara ya Uhamiaji kuondolewa katika sheria ya utumishi wa umma mwaka 2007 na Wizara kufanya marekebisho katika muundo wake, vyeo vya kada za askari vilirekebishwa ili kuandana na vyeo vinavyotumiwa na vyombo vingine vya ulinzi na

usalama vilivyo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi. Kwa msingi huo, utekelezaji wa majukumu na masuala ya usimamizi kwa sasa ni kama ifuatavyo:-

(i) Idara imeendelea kutekeleza majukumu yake bila ya kuwa na sheria ya usimamizi wa kada ya askari kwa kipindi cha miaka saba sasa. Na hiyo kuathiri utendaji kazi, nidhamu na maslahi mbalimbali ya watumishi hawa.

(ii) Idara ya Uhamiaji imeendelea kutambulika kama ofisi ya Mkurugenzi kisheria badala ya Idara ya Uhamiaji na kama muundo wa Wizara na idara ulivyopitishwa na Serikali mwaka 2010.

(iii) Idara imeendelea kupambana na changamoto za kisheria ikiwemo kushindwa kesi Mahakamani kutokana na upungufu uliopo katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutendaji. Mfano, kutotambuliwa kisheria na Mahakama kwa maelezo yaliyochukuliwa na idara kutoka kwa watuhumiwa kuhusu masuala ya uhamiaji na hivyo kusababisha watuhumiwa hao kuachiwa huru kiurahisi na Mahakama.

(iv) Watumishi wa Uhamiaji kada ya askari hupoteza haki zao za utumishi na mamlaka za utumishi kufanya maamuzi ya kiutumishi kwa kutegemea zaidi busara na siyo kwa mujibu wa matakwa ya sheria.

Mheshimiwa Spika, chimbuko la marekebisho na changamoto zilizopo: Chimbuko la marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji pamoja na changamoto zilizopo linatokana na mambo yafuatayo:-

(i) Kutokuwepo kwa sheria inayotambua na kusimamia utumishi wa kada ya askari wa Idara ya Uhamiaji baada ya idara hii kuondolewa katika usimamizi wa Sheria ya Utumishi wa Umma mwaka 2007.

(ii) Idara pamoja na majukumu yake kutoainishwa vizuri katika sheria iliyopo ambapo idara na majukumu hayo yanatambulika rasmi katika muundo wa Wizara na idara.

(iii) Sheria ya Uhamiaji iliyopo kutojitosheleza katika kushughulikia masuala mbalimbali ya kiutendaji.

(iv) Kuongezeka kwa majukumu ya uhamiaji kiulinzi na kiusalama kulikotokana na kujumuishwa kwenye sheria nyingine katika kupambana na makosa mengine kimataifa. Mfano ugaidi, katika Sheria ya Ugaidi, Sura ya 19 na usafirishaji wa haramu wa binadamu katika Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura 432.

(v) Kutojumuishwa katika Sheria ya Tume ya Polisi na Magereza ili utumishi wa Idara ya Uhamiaji kada ya askari usimamiwe na sheria hiyo na kama ilivyo kwa watumishi wengine wa vyombo vya ulinzi na usalama vilivyomo chini ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi.

(vi) Kuweka utangamano wa vyeo na hadhi ya watumishi wa Idara ya Uhamiaji na vyombo vingine vya Ulinzi na Usalama ndani ya Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ili kukidhi mahitaji ya muundo wa Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, mchakato wa marekebisho ya sheria: Baada ya kuona upungufu na changamoto mbalimbali katika utendaji wa kazi za idara, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi ilifanya uchambuzi wa mahitaji yanayotakiwa na kuyawasilisha katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ili kuirekebisha sheria hii. Mahitaji hayo ya marekebisho yalifanyiwa kazi na hatimaye kuridhiwa na Serikali mwezi Oktoba, 2014.

Mheshimiwa Spika, aidha, Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria hii ya Uhamiaji, Sura ya 54 uliwasilishwa Bungeni na Kusomwa kwa Mara ya Kwanza mnamo tarehe 08 Novemba, 2014.

Mheshimiwa Spika, madhumuni na sababu: Muswada huu unapendekeza marekebisho katika Sheria Uhamiaji, Sura ya 54 pamoja na sheria nyingine mbalimbali zinazohusu masuala ya Utumishi wa Idara ya Uhamiaji. Marekebisho yanayopendekezwa yanakusudiwa kuleta muundo mpya wa Utumishi katika Idara ya Uhamiaji pamoja na masuala mengine yanayohusiana na muundo huo.

Mheshimiwa Spika, mgawanyiko wa Muswada huu: Muswada huu umegawanyika katika sehemu tatu kuu:-

Sehemu ya kwanza, sehemu hii inaainisha jina la sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili, sehemu hii inaainisha marekebisho katika Sheria ya Uhamiaji, Sura ya 54 kwa kufuta baadhi ya misamiati kwa adhima ya kuruhusu matumizi ya misamiati na vyeo vipya vinavyoendana na muundo mpya kwa madhumuni hayo.

Sehemu hii pia inapendekeza kufuta msamiati "mkurugenzi", maana ya msamiati "mtoto" na "kirai", "Mwenyekiti wa Mahakama ya Wananchi" na kuweka misamiati na maana mpya zinazoendana na mabadiliko hayo. Hali kadhalika sehemu hii inapendekeza kufuta sehemu yote ya pili na kupendekeza sehemu mpya ya pili na ya tatu zenye vifungu vipya kutokana na…

*(Hapa Alikohoa)*

Kumradhi, kuweka vifungu vipya kutoka kifungu cha 4 hadi cha 22 kwa dhamira ya kuunda Idara ya Utumishi ya Uhamiaji. Kuainisha masharti ya uteuzi wa Kamishina Jenerali na maafisa wa vyeo hivyo…

*(Hapa Alikohoa)*

*Sorry*, samahani Spika! Vitengo vya idara hiyo na masuala mengine yanayohusu uendeshaji na utumishi wa uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Sehemu ya Tatu; Sehemu hii inapendekeza kufanya marekebisho katika sheria mbalimbali, marekebisho haya yanatokana na marekebisho yaliyofanywa chini ya Sheria ya Uhamiaji kwa lengo la kuoanisha marekebisho haya na Sheria hii kama ifuatavyo:-

(a) Kifungu cha 10 kinapendekeza marekebisho katika Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, Sura 432. Marekebisho haya yanalenga kuoainisha vyeo vilivyo katika Sheria hii na kile cha Kamishina Jenerali kama inavyopendekezwa katika Sheria ya Uhamiaji. Hivyo basi napendekeza kufuta maneno ambayo "anayehusika na aliyeshika cheo cha Mkurugenzi wa Uhamiaji" na yanayoainishwa katika kifungu cha 31 na kuweka maneno "ambaye ameshika au anayeshika au aliyeshika cheo cha Kamishina Jenerali".

(b) Kifungu cha 11 kinaainisha marekebisho katika Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi na Magereza, Sura 241. Marekebisho yanayokusudiwa kuingiza Idara ya Uhamiaji katika sheria hii. Kwa kutekeleza hilo sheria hiyo itafahamika na kuitwa Sheria ya Tume ya Utumishi wa Jeshi la Polisi, Uhamiaji na Magereza, Sura 241. Hivyo basi pamoja na mambo mengine, masuala ya mambo ya maslahi, nidhamu, upandishwaji vyeo kwa Maafisa wa Uhamiaji utashughulikiwa katika sheria hii. Sehemu hii pia inaainisha vyeo na misamiati mbalimbali kwa azma ya kufanikisha uingizaji wa muundo wa uhamiaji katika sheria hii.

(c) Kifungu cha 12 kinaainisha marekebisho katika Sheria ya Kupambana na Ugaidi, Sura ya 19. Marekebisho yanayofanywa kwa ajili ya kuleta utengamano wa misamiati inayotumika katika sheria hii na ile itakayotumika katika Sheria ya Uhamiaji kwa kufuta maneno "Kamishina Mkuu wa Uhamiaji" yanayoonekana katika vifungu vya 45 na 46 na kuweka maneno "Kamishina Jenerali wa Uhamiaji".

(d) Kifungu cha 13 kinapendekeza marekebisho katika Sheria ya Wakimbizi, Sura 37. Sehemu hii inapendekeza kufuta maneno "Mkurugenzi wa Uhamiaji" na kuweka maneno "Kamishina Jenerali wa Uhamiji". Lengo la Marekebisho haya kama yale mengine ni kuoanisha marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Uhamiaji na sheria hii.

(e) Kifungu cha 14, kinapendekeza marekebisho katika Sheria ya Uraia wa Tanzania, Sura 357. Dhamira ya marekebisho haya ni kuoanisha masharti ya sheria hii na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Uhamiaji hususan kufuta msamiati wa "Mkurugenzi" na kuweka msamiati wa "Kamishina Jenerali".

Sehemu hii pia inapendekeza kifungu kipya cha 64(a) kwa madhumuni ya kumpa madaraka ya kuthibitisha uraia wa mtu yeyote ambaye ni Mtanzania endapo mazingira yatahitaji au kulazimisha hivyo. Hali kadhalika inampa madaraka Kamishina Jenerali kutegua madaraka yake kwa afisa Muidhinishwa.

(f) Kifungu cha 15 kinaainisha marekebisho katika Sheria ya Pasipoti na Hati za Kusafiria Sura 42. Marekebisho yanayopendekezwa yanakusudia kuleta utengamano baina ya sheria hii na marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, katika kutekeleza hilo, sehemu hii inapendekeza kufuta msamiati "Mkurugenzi" na maana ya msamiati "Idara".

Mheshimiwa Spika, endapo Bunge lako tukufu litapitisha Muswada huu wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji na kuridhiwa, changamoto za kisheria zilizokuwa zinaikumba Idara ya Uhamiaji katika utekelezaji wake wa majukumu zitaondoka.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Sasa nitamuita Mwenyekiti wa Kamati iliyohusika na Muswada huu au mwakilishi wake. Wale ambao wanasema hapa wawe wanasogea, kwa sababu muda tunaopoteza ni mwingi. Wote wanaojua wanasoma wawe wanasogea kwenye *front desks*.

**Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji, *(The Immigration Amendments Bill)* ya mwaka 2014.**

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA):** Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 86(5) ya Kanunu za Kudumu za Bunge, Toleo la Aprili 2013, kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Mataifa Mheshimiwa Edward Ngoyai Lowassa, naomba kuwasilisha maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji *(The Immigration Amendments Bill)* ya mwaka 2014.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuipa Kamati kazi ya kushughulikia Muswada huu kwa mujibu wa Kanuni ya 84(1) ya Kanuni ya Bunge, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 84(2) na Kanuni ya 187(9) kuhusu kuwaalika wadau na kusikiliza maoni yao. Michango ya wadau waliofika mbele ya Kamati na kuwasilisha maoni yao pamoja na wale waliotoa maoni kwa maandishi imekuwa na manufaa makubwa katika mchakato wa utungaji wa sheria inayopendekezwa. Naomba kuwatambua wadau hao kama ifuatavyo:-

Wa kwanza, ni Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu *(Legal and Human Rights Centre)*, wa pili ni *Asylum Access Refugee Solutions Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia maudhui ya Muswada huu, Kamati yangu ilishirikiana na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama katika kuuchambua. Uchambuzi wa Muswada huu ulifanyika kwa ushirikiano mkubwa baina ya Kamati hizi mbili. Tarehe 14 Januari, 2015 katika kikao cha pamoja Kamati hizo zilipokea maelezo ya Serikali kuhusu maudhui ya Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, katika utekelezaji wa dhana ya kuwashirikisha wananchi katika utungwaji wa sheria, Kamati hizi mbili kwa pamoja zilizisikiliza maoni ya wadau waliotajwa hapo juu. Aidha, kazi ya uchambuzi wa maoni, maelezo ya Serikali na maudhui ya Muswada iliendelea kwa kuzingatia mambo mbalimbali ya msingi katika utungaji wa sheria.

Mheshimiwa Spika, Maudhui ya Muswada: Mtoa hoja alipowasilisha Muswada huu kwenye Kamati alieleza kuhusu maudhui ya Muswada huu kwa ujumla. Kamati zote mbili zilipitia Muswada huu ibara kwa ibara. Muswada una ibara 15 zilizopangwa katika sehemu tatu:-

Sehemu ya kwanza inahusu jina la sheria inayopendekezwa.

Sehemu ya pili inahusu marekebisho yanayopendekezwa katika Sheria ya Uhamiaji Sura 54 ya Sheria ya Tanzania, yaani *The Immigration Act Cap, 54.*

Sehemu ya tatu inapendekeza marekebisho katika sheria nyingine sita kutokana na mapendekezo ya kurekebisha sheria ya uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati zilipitia jina refu la Muswada pamoja na ibara zote 15 kwa kuzingatia maelezo ya Serikali na maoni ya wadau waliowasilishwa kwenye kikao na mengine kwa maandishi.

Mheshimiwa Spika, mambo ya msingi yaliyozingatiwa. Katika uchambuzi wa mapendekezo ya kurekebisha Sheria ya Uhamiaji Sura 54, Kamati zilizingatia mambo mbalimbali ya msingi ikiwemo:-

(i) Manufaa ya marekebisho ya sheria yanayopendekezwa.
(ii) Dosari zinazoweza kuwepo kisheria, mfumo na uendeshaji kwa kutorekebisha sheria, kwa namna inavyopendekezwa.
(iii) Mantinki ya mapendekezo yaliyopo katika Muswada huu.
(iv) Namna Muswada wa Sheria unavyoboresha muundo wa uhamiaji.
(v) Uhusiano kwa kimfumo, sheria na uendeshaji unaoimalika na kuboreka kutokana na marekebisho yanayopendekezwa.
(vi) Umuhimu wa kuanisha sheria ya uhamiaji na sheria nyingine zinazohusika na utumishi wa uhamiaji pamoja na udhibiti wa uingiaji wa wageni nchini Tanzania.

Mheshimiwa Spika, katika kuzingatia mambo hayo, Kamati ilianisha mapendekezo ya namna tatu ambayo ni:-

Ya kwanza, ni mapendekezo ya kufuta baadhi ya misamiati au virai yaani *phrases* na kuweka badala yake misamiati mipya na virai vingine.

Ya pili, ni kufuta vifungu vya Sheria ya Uhamiaji Sura 54, katika sehemu ya pili ya sheria na kuweka vifungu vipya katika sehemu ya pili na sehemuu mpya ya tatu kwenye sheria hiyo.

Ya tatu, ni kufanya marekebisho katika sheria nyingine sita.

Mheshimiwa Spika, mapendekezo hayo pamoja na mambo ya msingi yaliyozingatiwa yalisababisha kujitokeza kwa mambo mbalimbali wakati wa uchambuzi wa Muswada na hasa mambo mawili yaliyohusu;

Ya kwanza, ni kuainisha tafsiri ya neno "*child*" yaani mtoto katika Sheria ya Mtoto *(Child Law)* ya Tanzania Bara na Sheria ya Watoto *Children Act* ya Tanzania Zanzibar.

Ya pili, ni kutofautisha dhana mbili katika muundo wa kiaskari. Dhana hizo kwa Kingereza ni "*Gazetted Officer*" na "*Commissioned Officer*" ili kubaini usahihi wa matumizi ya kirai yaani *phrase Commissioned Officer* katika muundo wa Idara ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo: Kwa kuzingatia mambo mbalimbali ya msingi wakati wa kupitia ibara kwa ibara na kutokana na uchambuzi wa majadiriano wa Kamati mbili kwa pamoja yapo maoni na mapendekezo yaliyopelekewa kufanyiwa kazi na Serikali. Maoni hayo yanahusu matumizi ya lugha, uchapishaji na maudhui na maudhui ya vifungu vya sheria inayopendekezwa kama ifuatavyo:-

Maoni kuhusu maudhui: Ibara ya kwanza mpaka ya 16. Katika ibara hizi Kamati iliafikiana na mapendekezo yaliyowasilishwa na Serikali pamoja na maudhui katika vifungu hivi.

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 17: Katika ibara hii kulikuwa na maoni yakuongeza kifungu (5) kinachozuia mtoto kuwekwa rumande kwa muda mrefu wakati akisubiri kurudishwa nchini mwake. Ibara hii inapendekezwa isomeke kama ifuatavyo:-

Ibara ya 17(5) (a*) where a child is detained under subsection 3 it shall be only be ordered as a last resort for the shortest period of time. Subsection (b) The Immigration Officer*

*shall take all possible measures to prevent child migrants from being detained alongside non child migrant.*

Mheshimiwa Spika, Ibara ya 18, 19 na 20. Katika ibara hizi Kamati imeridhika na maudhui pamoja na maelezo yaliyotolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, ibara ya 21, ibara hii inahusu kuachiwa kwa masharti yaani *condition release,* Kamati ina maoni kuwa ni muhimu masharti ya kuachiwa kwa muda yakaainishwa katika sheria. Hivyo basi Kamati inapendekeza kifungu kidogo kinachoainisha masharti hayo kisomeke kama ifuatavyo:-

*(2) A person will be eligible for conditional release if there are no reasonable grounds that he/she (a) is a threat to National Security (b) will endanger public safety or is at risk to public health.*

Mheshimiwa Spika, ibara ya 22. Ibara hii inayohusu kuzuia kuingia nchini yaani *power of refusal of entry* kulikuwa na maoni mbalimbali kutoka kwa wadau waliotaka kifungu hiki kifanyiwe marekebisho kwa kueleza kuwa kifungu kama kilivyo kinatoa madaraka makubwa kwa Idara ya Uhamiaji. Hata hivyo Kamati imeridhika na maudhui ya kifungu hiki kutokana na wajibu na majukumu ya Idara ya Uhamiaji kwa mujibu wa sheria katika shughuli za kuhakikisha usalama kwenye vituo vya mipakani.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Jumla: Kwa ujumla mapendekezo ya kufanya marekebisho ya sheria hii ni ya msingi na yenye tija katika kuweka sawa baadhi ya mambo muhimu kuhusu kuimarisha muundo wa Idara ya Uhamiaji na udhibiti wa uingiliaji wa wageni nchini. Pamoja na hayo, Kamati ina maoni ya jumla kama ifuatavyo:-

Ya kwanza, ili kutekeleza vyema, sheria inayopendekezwa madhumuni yake kuwa na maana katika mfumo wa kisheria kuna umuhimu wa kuhakikisha kuwa unakuwepo uhusiano, ushirikiano na mawasiliano kwa kiwango cha kutosha baina ya idara ya uhamiaji na wadau wengine serikalini.

Ya pili, kwa madhumuni ya utekelezaji bora wa sheria inayozingatia mfumo wa muundo wa kitaasisi na utawala wa idara ya uhamiaji, suala la bajeti na rasilimali nyingine muhimu linahitaji kuzingatiwa ipasavyo.

Ya tatu, kwa kuwa mafunzo ya awali kwa askari wa Idara ya Uhamiaji ni ya msingi na muhimu katika utekelezaji bora wa sheria ya uhamiaji na kwa kuwa kwa sasa Idara ya Uhamiaji haina chuo kwa ajili ya mafunzo awali, tunaishauri Serikali ianzishe chuo cha aina hiyo.

Ya nne, kwa kuwa Sheria ya Uhamiaji inahusu udhibiti wa kuingia kwa wageni nchini; na kwa kuwa ofisi za Balozi za Tanzania katika sehemu mbalimbali Duniani zinashughulikia pamoja na mambo mengine vibali vya watu wa mataifa mbalimbali kuingia nchini, yaani utoaji *Visa*, kuna umuhimu wa Maafisa Uhamiaji kupangwa katika Balozi zetu nje ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Hitimisho: Baada ya maelezo hayo kuhusu maoni ya Kamati naomba tena kukushukuru kwa kunipa nafasi hii adimu ili niwasilishe maoni ya Kamati kuhusu Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Anna Abdallah Mbunge, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama pamoja na Wabunge wote wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Ulinzi na Usalama kwa michango yao mizuri wakati wa kuchambua

Muswada huu kwa kuthamini maoni ya Wajumbe wa kamati hiyo. Naomba kuwatambua majina kama ifuatavyo:-

**SPIKA:** Hatuna muda wa majina.

**MHE. BETTY E. MACHANGU (K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Kama ilivyoainishwa kwenye ukurasa wa 10 wa kitabu cha maoni ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, namshukuru pia Mheshimiwa Mathias Chikawe Mbunge, Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi pamoja na wataalam kutoka Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ufafanuzi wao walioutoa kulingana na mahitaji ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, kipekee nawashukuru Wajumbe wa Kamati ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa kwa michango yao mizuri iliyowezesha kupatikana kwa maoni hayo. Kwa kuwathamini naomba muangalie katika kitabu cha maoni ya Kamati iliyoko ukurasa wa 11 na 12.

Mheshimiwa Spika, vilevile namshukuru Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati Ndugu Othumani Hussein na Makatibu wa Kamati Ndugu Ramadhani Issa, Nesta Kawamala na Onesmo Laulau kwa utaratibu wa kufanikisha maandalizi ya maoni haya.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**SPIKA:** Ahsante, sasa nitamuita Msemaji kutoka Kambi ya Upinzani kuhusu Muswada huu.

**MHE. AMINA MOHAMED MWIDAU (K.n.y MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI):** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Kwa mujibu wa Kanuni ya 86(6) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2013, naomba kuwasilisha mbele yako maoni kwa niaba ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Wizara ya Mambo ya Ndani, Mheshimiwa Godbless Jonathan Lema Mbunge wa Arusha kuhusu Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 2014 *(The Immigration Amendment Act, 2014)*.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa naomba kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa nguvu za kuweza kusimama hapa ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani kuhusu Muswada Huu wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji Sura, 54.

Mheshimiwa Spika, nitakuwa sijatenda haki kama sitawapongeza Viongozi Wakuu wa vyama vilivyounda UKAWA kwa kuhakikisha kwamba wanapambana na propaganda kubwa inayoendelea dhidi ya ushirikiano wetu hasa tunapoelekea Uchaguzi Mkuu. Kwa hali ilivyo kwa sasa inabidi kukaba hadi *penalty* na mwezi Oktoba kitaeleweka tu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile naomba kuchukua nafasi hii kuwashukuru sana wananchi wa Wilaya ya Pangani kwa ushirikiano mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu yangu ya kila siku. Pia naishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu na ushirikiano mkubwa wanaonipatia ninapokuwa katika kutekeleza majukumu yangu.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji ni idara nyeti sana katika Taifa letu lakini kwa masikitiko makubwa sana tumekuwa tukisikia katika vyombo vya habari kwamba, idara hii ndiyo inayoongoza kwa kila aina ya uchafu wa kimaadili.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na taarifa za kila mara kuhusiana na watendaji katika idara hii kujihusisha moja kwa moja katika kusaidia biashara haramu za kusafirisha wahamiaji haramu kutoka nchi za Somalia, Ethiopia na kuwapitisha Tanzania kuelekea nchi za Kusini mwa Tanzania.

Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ya kujiuliza ni kuwa, vipi wahamiaji haramu kutoka Ethiopia wakamatwe katika Mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa au Mbeya, wakati watu hao wanatoka Ethiopia au Eritrea na mpaka wa kuvuka ni kutokea Kenya?

Naomba kunukuu kauli ya Mheshimiwa Waziri Mstaafu wa Wizara hiyo kabla ya kuhamishiwa Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa Mheshimiwa Shamsi Vuai Nahodha, Mbunge, alikaririwa akisema, "Kilimanjaro ni moja kati ya Mikoa minane inayomtia kichefuchefu nchini".

Aidha, Waziri huyo alisema baadhi ya watumishi wamekuwa wakijihusisha na mtandao wa uingizaji wa wahamiaji haramu nchini, pia kutoa vibali bandia kwa wageni.

Mheshimiwa Spika, suala la uhamiaji haramu limeendelea kuwa tatizo sugu linalotia doa utendaji wa Idara hii ya Uhamiaji ndani ya nchi na nje ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, sio hilo tu bali kumekuwepo na taarifa hadi za kutaja majina ya wanaoitwa vigogo wa idara hiyo kumiliki mali ambayo hawawezi kuitolea maelezo. Sambamba na hilo ni utoaji wa hati za kusafiria kwa raia wasiokuwa Watanzania na hati hizo hutumiwa kusafirisha mihadarati.

Mheshimiwa Spika, jambo hili kwa kiasi kikubwa ndiyo chanzo cha kusikia kuwa, Watanzania kadhaa wamefungwa katika Magereza ya nchi za nje kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya ili hali wengi wao sio Watanzaia. Haya yote yanaitia doa kubwa Idara hii ya Uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, Idara ya Uhamiaji nchini iliingia katika kashfa nzito ya kuhusishwa na utoaji wa hati nne za kusafiria kwa mtu mmoja. Hati hizo zilitolewa na Idara ya Uhamiaji kwa nyakati tofauti, zote zikiwa zinatumiwa na mtumiaji huyo, jambo ambalo ni kinyume cha sheria. Aidha, uchunguzi uliofanywa ulibaini kuwa, wafanyabiashara wakubwa wa dawa za kulevya nchini, wamekuwa wakitumia hati za kusafiria zaidi ya moja kama mbinu ya kuwawezesha wasikamatwe. Hoja hapa ni je, marekebisho ya sheria hii ndiyo yatakayopelekea udhibiti wa mianya hii ya rushwa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo kubwa na la kutia aibu ni ajira kutolewa kwa njia ya nasaba. Taarifa ya Utafiti ya Tume Maalum iliyoundwa Kuchunguza Tuhuma za Ufisadi ilibaini uchafu huo wa kupeana ajira na vyeo kwa njia hiyo. Hii inatokana na ukweli kwamba, ni njia ya kulindana au kuunda umoja katika maovu. Umoja huo ndiyo mfumo wa kiutendaji katika Idara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya Kambi Rasmi kutoa masuala hayo ya jumla kuhusiana na utendaji wa Idara hiyo, sasa tunaangalia baadhi ya vifungu kwa Muswada huu.

Kifungu cha 5 cha Muswada, kinachofanyia marekebisho sehemu ya pili ya Sheria, kwa kuvifuta na kuviandika upya vifungu vya 5(1) na 7(1) vya sehemu ya pili vinavyohusu uteuzi.

Kambi Rasmi ya Upinzani, inaona kama nafasi ya *Commissioner General* ni uteuzi wa Rais, basi nafasi za *Deputy Commissioner General* na *Senior Assistant Commissioner*, uteuzi wao usiwe ni kwa Rais, uwe kwa Waziri. Hii ni kwa sababu itasaidia kuondoa mgongano katika utendaji wa kazi kwani hata mamlaka zao za nidhamu ziwe tofauti.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge nadhani wanakumbuka suala la kinidhamu la aliyekuwa Katibu Mkuu Wizara ya Nishati na Madini, Ndugu Jairo. Waziri Mkuu alishindwa kumwajibisha kwa hoja kwamba, mamlaka yake ya uteuzi ni Rais na hivyo mamlaka yake ya nidhamu ni Rais pia. Kwa msingi huo, ni sawa pia kwa nafasi za vifungu vilivyotajwa hapo juu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 7(2) na (3), Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri suala la uteuzi lisiwepo, bali watu wapande vyeo kwa vigezo mbalimbali ambavyo vinatakiwa kuwa wazi ili kuondoa suala la undugu na rushwa katika kupeana vyeo. Jambo hili la uteuzi linaweza kuitumbukiza tena kwa kiwango cha juu Idara hii katika kashfa mpya ya uteuzi wa upendeleo.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 12(1)(s), kinachosema kuwa, kati ya kazi za Afisa Uhamiaji ni pamoja na ku-*conduct patrol and investigation.* Kwa mujibu wa wadau, Kifungu hiki kinatoa nguvu kubwa kwa Afisa wa Uhamiaji kufanya kazi ambayo ilitakiwa kufanywa na Jeshi la Polisi; kwani uchunguzi au upelelezi bila kuwepo na ukomo wake, kunaweza kupelekea udhalilishaji wa wahusika. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona madaraka ya kifungu hiki yawekewe mipaka kwa Afisa Uhamiaji kutekeleza majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17(1), kinachosema kwamba; *An immigration Officer may without warrant arrest any person who has committed or is about to commit an offence under this act or any other written laws.*"

Madaraka haya yanatolewa ya kukamata bila kuwa na kibali cha kukamata kwa kuhisi mtu tu bila ya kuwa na uhakika ni hatari sana.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema, Kifungu hiki kirekebishwe, kwani mamlaka ya kukamata lazima kuwepo na kibali kwani hadi kibali kinatolewa ni dhahiri kwamba, ushahidi wa uhakika unakuwepo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vifungu vya aina hii katika sheria ndivyo vinavyopelekea watu kudhalilishwa utu wao na wengine kunyang'anywa mali zao kama ilivyotokea katika zoezi la Operesheni Kimbunga. Ikumbukwe kwamba, Operesheni hii iliendeshwa bila kuwepo uwepo wa kifungu kama hiki. Sasa je, kikiwepo kwenye sheria madhara yake kwa wananchi yatakuwaje?

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17(3), kinachohusu Afisa Uhamiaji au mwenye cheo cha juu ya *Superintendent*, kuweza kuamuru mtu yeyote kuwekwa kizuizini kabla ya tangazo la kusafirishwa nje ya nchi. Kambi Rasmi ya Upinzani haioni maana halisi ya kuwa na kifungu kama hiki ambacho kinaweza kutumiwa vibaya na kuvunja uhuru na haki za msingi za binadamu. Aidha, kifungu hiki hakielezi ni kwa muda gani kabla ya tangazo la kumhamisha mtuhumiwa atakuwa kizuizini.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 18 (3), kinahusu adhabu kwa yeyote atakayekwenda kinyume na matakwa ya Kifungu cha 18 (2). Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza ni adhabu gani itatolewa kwa Afisa wa Uhamiaji ambaye atamtendea kinyume mtu ambaye hana makosa bali amehisiwa au amedhaniwa tu?

Kambi Rasmi ya Upinzani ina mifano halisi ya wananchi ambao wamenyanyaswa na kudhalilishwa na Maafisa Uhamiaji wakati hawana makosa yoyote, bali Maafisa hao wanakuwa wanatumiwa tu ili kutekeleza mataka ya watu wengine.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu Muswada huu ukaweka kifungu cha adhabu kwa afisa yeyote atakayebainika kutenda kosa hilo.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Inaonekana kabisa Muswada huu mgumu kujadili kwa sababu hakuna cha kujadili, kwa hiyo, tunaedelea. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunao wachangiaji wafuatao:-

Mheshimiwa Leticia Nyerere, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Desderius Mipata na Mheshimiwa Henry Shekifu. Mheshimiwa Leticia Nyerere!

**MHE. LETICIA M. NYERERE:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi na mimi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, suala la Uhamiaji ni suala ambalo liko *very complicated* duniani kote. Nimezifuatilia Sheria zetu za Uhamiaji, ni nzuri kabisa pamoja na marekebisho yake yote, lakini kuna matatizo ambayo siyo ya kuundwa na binadamu, ambayo ni lazima tuyatambue ili tuweze kutatua matatizo yetu ya Uhamiaji. Mfano, haya mambo ya watoto, Askari au *Immigration Officer,* anaweza akashindwa ku-*determine* kwamba, huyu ni mtoto au siyo mtoto. Hilo ni suala ambalo lazima tukubaliane nalo. *Immigration Officer* anapofanya makosa ya kumwita mtoto labda mtu mzima, inawezekana siyo kosa lake.

Mheshimiwa Spika, maana ya kuwa mkimbizi, unaondoka kwa sababu ya dharura ulikotoka, siyo kwamba una muda hata kwa ku-*park* mizigo, kutafuta *documents*, kutafuta *passport*. Haya ni masuala ya dharura ambayo ni lazima tuyaelewe na ndiyo maana tunapozungumza ufanisi wa *Immigration Officer,* ni lazima tutambue yuko katika mazingira gani. Katika mahojiano, unaweza ukakuta mtu hawezi kuongea lugha ambayo *Immigration Officer* anaongea. Kwa hiyo, ni lazima tuwe *realistic* kutambua uzito kwa watendaji wetu, matatizo wanayoyapata.

Matatizo ya uhamiaji hayajitokezi hivi hivi au hayakusudiwi, yanajitokeza kwa sababu ni lazima yatokee, ni kama mtu labda anapata ajali huwa haitabiriki.

Mheshimiwa Spika, nikizungumzia matatizo ya utendaji hapa, sheria tunazo, tunafanya *amendments* kila mara na ni nzuri tu ukiziangalia. Nimezifuatilia sana Sheria za Uhamiaji, nimegundua kuna *amendments* ambazo hazikupaswa kufanyika, kwa sababu zilikuwa nzuri tu, tatizo ni *implementation*, *how do we implement* hizi sheria, ndiyo tatizo kubwa. Kuna makosa, kuna ufanisi, kwa hiyo, tuelewe ili tuweze kufanya kazi kwa haki na kuwatendea wakimbizi haki, siyo tunakaa tunalalamika. Kweli watu wanalalamikia suala la rushwa, lipo, lakini isichukuliwe kwamba, Idara ya Uhamiaji hapa ndiyo imekithiri kwa rushwa, hapana!

Rushwa inazungumzwa duniani kote. Kuna wakati katika Bunge fulani la nchi fulani, *congress man* alisema *our immigration system is rotten.* Kwa hiyo, na sisi tunaweza tukasema hivyo, lakini siyo watu wa kwanza, dunia yote, dunia nzima, ukifanya utafiti kuhusu mambo ya

*immigration*, utakuta dunia nzima inalia na hiyo idara, kwa sababu kuna matatizo ambayo siyo ya kujipangia.

Mheshimiwa Spika, suala la *immigration* pia siyo la Askari wa Uhamiaji peke yake na Serikali, ni la Wananchi wote. Ukienda nchi zingine, utakuta watu wanafuatilia wageni, ukifika leo umelala kwa jirani, tayari wamekufuatilia na kwa sababu ni wazalendo, wanatoa taarifa kwamba kuna mgeni nyumbani kwa fulani. Ndiyo maana wenzetu wengine wana utaratibu wa kuwa-*encourage* wananchi wao kufuatilia mambo haya yakiwemo ya uhamiaji, ni muhimu sana, ni muhimu kusaidiana kwa kazi yoyote. Huwezi kufanikiwa kukamata majambazi kama huwahusishi Wananchi.

Kwa hiyo, naiomba Serikali iweke msisitizo wa hali ya juu katika kuwashirikisha Wananchi, hasa katika suala hili la *immigration* ni suala zito, ni suala gumu, ukizingatia hata nchini kwetu, tuna mipaka ambayo tunapakana na watu ambao wanaongea lugha moja na Watanzania. Kwa hiyo, ni lazima tulichukue na tulipe kipaumbele suala la utekelezaji wa sheria hii.

Kupanga sheria *is one thing, to implement is another thing.* Kwa hiyo, ni wajibu wetu wote ili tuweze kupunguza matatizo haya. Kuna watu kweli wamekuwa wakiingia nchini wanaingia na wanakuwa Watanzania, kwa sababu hakuna ufuatiliaji wa ndani kwa ndani. Endapo tungeweza kufuatilia, hapa kwa jirani amekuja mgeni katokea wapi?

Mimi nimewahi kuingia nyumba ya mtu nikapiga hodi, nikauliza *who is this guy*, nika-*investigate* nikakuta kweli alikuwa siyo wa nchi hiyo, alikuwa ni mgeni ambaye katoka nchi nyingine na hana *documents* za kuishi hiyo nchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, mimi yangu ni hayo tu, nawasihi WAtanzania tuwe wazalendo ili tuweze kuleta ulinzi mkubwa katika masuala ya *immigration*. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa!

**MHE. DKT. ANTONY G. MBASSA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia jioni ya leo katika suala zima lililoko mbele yetu kuhusu suala zima la uhamiaji.

Mheshimiwa Spika, mimi nitaongea suala hili nikichukulia mfano dhahiri wa maeneo ninayotoka ya pembezoni na adha tunayoipata kuhusiana na suala hili.

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa Idara hii imekuwa ikifanya kazi zake aidha kwa umakini, lakini sehemu nyingine imekuwa ikipotoshwa na haipati taarifa zilizo sahihi.

Mheshimiwa Spika, wahamiaji wanaoingia nchini, kimsingi ni wengi kulingana na mipaka yetu kwamba haiwezi kulindwa vizuri wala kutunzwa vizuri. Jukumu la Idara hii ni kuona ni jinsi gani itajipanga iweze kufanya kazi vizuri. Bahati nzuri Idara hii inashiriki katika kazi au kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ambayo katika wilaya inaongozwa na Mkuu wa Wilaya.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza, unakuta watu hawa wanapokuja kukamatwa kwamba ni wakimbizi, tayari wameshakaa muda wa kutosha ndani ya maeneo yetu, kiasi kwamba, wao na wenyeji tofauti haipo.

Sasa swali la kujiuliza; kama Idara hii inafanya kazi yake vizuri na ina mtiririko mzuri kuanzia ngazi ya wilaya au tuanzie mkoa, wilaya mpaka kwenye kitongoji, iweje watu waje

waishi, wajenge, wengine waoane, dakika za mwisho unakuja kuambiwa hawa ni wahamiaji haramu! Kwa kweli inatisha na haiingii akilini.

Mheshimiwa Spika, suala hili tumeliona katika uchaguzi uliopita wa Wajumbe wa Serikali za Mitaa, Uchaguzi za Serikali za Mitaa. Unamkuta mwananchi ameishi zaidi ya miaka 20, kawa kiongozi katika chama fulani, lakini akigeuka kwenda chama fulani, ndiyo hapo pingamizi linatolewa kwamba huyu siyo raia! Sasa unajiuliza; Idara hii ya Uhamiaji ilikuwa wapi? *(Kicheko/Makofi)*

Mheshimiwa Spika, inasikitisha sana, juzi hapa Mheshimiwa Ntukamazina aliongelea kuhusu watu wa Ngara kupata *passport*. Wanachelewesha ifahamike wanatoka wapi, wako wapi, lakini Idara hii si ipo na watu hao si wanafahamika! Baado inakuwa ni tatizo kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, ninapata wasiwasi mkubwa sana, kwa sababu kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya inayoongozwa na Mkuu wa Wilaya, mojawapo ya Wajumbe ni Afisa wa Uhamiaji. Wanapojadili, wanajadili masuala mazima yanayohusiana na usalama ndani ya eneo lao, lakini inasikitisha kwamba watu hawa wanaingia, wapo! Pale wanapokuwa wamepitia katika mazingira ya rushwa, wanaishi vizuri, lakini inapofikia mahala huyu mtu basi akaenda tofauti na wasivyotaka wao, ndiyo anakuwa mhamiaji haramu! Inakujaje?

Mheshimiwa Spika, huko kwetu kuna vibali vinavyotolewa, aidha watu wanatoka kwa muda mfupi tu kutembea na kufanya nini, lakini je Idara hii inajiridhishaje kwamba hawa watu walioomba vibali vya muda mfupi wamerudi ndani ya muda waliopangiwa na kama hawakurudi wanawasaka vipi kuwapata kusudi wawarudishe?

Leo hii kuna watu wanapata vibali sana vya kuja kuishi hapa nchini, je, taratibu zinafuatwa?

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Idara hii ijaribu kuangalia utaratibu wa kufanya kazi ili kuondoa usumbufu mdogo au mkubwa unaojitokeza kwa wananchi wengine ambao kimsingi hawahusiki na wala siyo wahamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, ninaamini kabisa Idara hii ina utaratibu wa kufanya kazi, lakini utaratibu huu unateremkaje mpaka kwenye Serikali zetu za Vijiji ambako ndiko waliko Wajumbe wanaowatambua hawa wageni wanaokuja kwenye vitongoji, kwenye mitaa yetu? Wanafanyaje kazi na hawa watu ili kuweza kubaini mgeni gani kaingia huyu na kama ana vitambulisho vya kuweza kuishi hapa nchini au amekuja kwa mikakati ipi? Suala hili linaachwa tu. Kuna hawa watu wanakuja kwa ajili ya biashara, kuna watu wanakuja kwa ajili ya kilimo, kwa ajili ya ufugaji na wengine kuwatembelea ndugu, jamaa na marafiki. Je, watu hawa kweli wanadhibitiwa na Idara hii ya Uhamiaji?

Mheshimiwa Spika, ipo mifano mingi ambayo imejitokeza huko kwetu, lakini cha ajabu imefika mahala unauliza hupati jibu sahihi. Tunapenda tujue sasa, pamoja na maoni yote yaliyotolewa, kuanzia Kamati husika, Mwenyekiti wa Kamati ametueleza hapa vizuri sana, lakini nishukuru jinsi gani Kambi Rasmi ya Upinzani ilivyoeleza vifungu vingine vizuri, kuhusu uteuzi wa hawa Makamishna, ambao kimsingi najua wakiteremka huku chini wakasimamia majukumu yao vizuri, suala hili la uhamiaji haramu hakika litakwisha.

Mheshimiwa Spika, linaloshangaza zaidi, ni wale watu wanaochukuliwa kwamba ni wahamiaji haramu, baada ya wiki mbili, watu hao unakutana nao mtaani. Hivi huu uhamiaji haramu unakuwa umekwisha au hawa watu wanakuwa wame-*process* vipi vibali vya kuweza kuishi nchini tena? Hili lazima tuliangalie kwa makini sana.

Mheshimiwa Spika, mimi naomba Idara hii sasa isimame imara, iweze kuwafuatilia watu hawa na kimsingi wanapopatikana basi taratibu, sheria na kanuni zilizopo ziweze kufanya kazi yake na tuondokane na suala hili la uhamiaji haramu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Sasa namwita Mheshimiwa Dkt. Henry Shekifu!

**MHE. DKT. HENRY D. SHEKIFU:** Mheshimiwa Spika, awali ya yote, nakushuku sana kwa kupata nafasi ya kuchangia Muswada huu. Kwanza, niseme ni ukweli usiopingika kwa maelezo ya Waziri kwamba, Muswada huu kwa jinsi ulivyokuja na ulivyosukwa, unajibu changamoto zilizopo, lakini pia taratibu zilizotumika ili kurekebisha changamoto.

Kwa hiyo, nichukue nafasi hii kumpongeza sana Waziri, jambo hili limekuja kwa wakati na niseme pengine limechelewa. Nasema limechelewa kwa sababu mwaka 2010 ndiyo ulikwa mwaka ambao mfumo au muundo ulikubalika. Hivi sasa karibu miaka minne Watumishi wa Uhamiaji hawana mfumo ambao unawatambua. Sasa nashukuru kwamba hili limekuja hivi sasa.

Mheshimiwa Spika, mimi nina mambo machache tu ya kutaka kuchangia. Kwanza, kuna suala la ushauri. Katika sheria hii, samahani sana, yako mambo ambayo ni muhimu yametajwa.

Kwanza, nizungumzie kifungu cha saba. Mimi nakubaliana na wale waliopendekeza kwamba, uteuzi wa *Assistant Commissioners* usifanywe na Rais, ufanywe na utaratibu wa kawaida wa kuteua watumishi wa ngazi za juu. *In fact* katika maeneo haya ambayo ni nyeti, afadhali kungekuwa na kitu kwa utaratibu wa kisasa kuwa *transparent,* kuwe na *Search Committee*. Iwepo Kamati ambayo itaratibu uteuzi wa watu hawa ili tupate watu safi. *Commissioner* awe ni *appointee* wa Rais, kwa sababu kwa kweli ni Idara muhimu na kubwa na yenye heshima kubwa, lakini hawa wengine wapite katika mchujo.

Haya mambo ya kusema atateuliwa na Rais, majina matatu, ndiyo maana tunafika mahala tunapata watu ambao hawakudhibitiwa na kuangaliwa kwa undani zaidi. Kukiwa na *Search Committee* ni rahisi sana kupata watu wazuri. Hili mimi nalikubali na ninamshauri sana Waziri aliangalie mara mbili, tatu, Serikali kwa ujumla, tubadilike twende na wakati, *we need good people.*

Mheshimiwa Spika, mambo mengine ambayo mimi nitayazungumzia ni yale ambayo ni ya jumla. Kwanza, tumewalaumu na wamelaumiwa ndugu zetu wa Uhamiaji. Tumewalaumu na wamelaumiwa ndugu zetu wa Uhamiaji, lakini kwa kweli saa nyingine mnyonge mnyongeni lakini haki yake mpeni. Wanafanya kazi katika mazingira magumu sana, mipaka ya nchi hii ni mikubwa sana, hawa watu hawana vyombo vya kufanyia kazi, huu ni ukweli. *(Makofi)*

Bahati nzuri Mheshimiwa Spika uliwahi kuniweka mimi katika Kamati ya Ulinzi na Usalama. Kwa bahati mbaya niliyoyaona ni magumu sana kwa Vyombo vyetu vya Ulinzi na Usalama. Sasa lazima tukitaka hawa watu wafanye kazi vizuri, waweze kulinda mipaka yetu vizuri, waweze kuangalia watu wanaoingia katika nchi yetu bila utaratibu, tuwape vyombo vya kufanyia kazi. Lazima tufanye hilo. Nami ningeshauri huko tunakokwenda Uhamiaji iwe ni mamlaka, ikiwezekana iwe *agency,* ikusanye fedha izitumie, Serikali isaidie pale panapohitajika, tutaona ufanisi.

Kweli inaweza kuwa chini ya Serikali lakini ifanye kazi kama *agency,* isipewe ka-*commission* sijui asilimia arobaini ndiyo wanapewa *retention*, hawawezi kuendesha kazi zao. Majengo wameanza mengi, lakini hayajengeki kwa sababu wanatengewa fedha chache. Ukienda kwenye mipaka yetu utasikitika, Idara zetu za Uhamiaji wamejibandika bandika maeneo ya ajabu. Ukiangalia upande wa wenzetu majengo mazuri.

Vifaa vya kufanyia kazi; mimi nasema udhaifu huu, Serikali mmekuja wakati mzuri, mmeliona hili, kubadilisha sheria ili Watumishi wa Uhamiaji wafanye kazi kama wengine. Waingie kama majeshi mengine yanavyopata haki, basi angalieni uwezo wao wa kupata vitendea kazi.

Ninashauri, ni ukweli kwamba upo upungufu ambao unafanywa na binadamu, huu tuukabili. Tuwape vifaa lakini na wao lazima wabadilike. Ndiyo maana mimi napendekeza kuwa, Makamishna Wasaidizi wawe *under Search Committee,* wawe watu wazuri watakaomsaidia *Commissioner General* kuchapa kazi yake vizuri. Kwa hiyo, ule upungufu ambao umesemwa na Wabunge ambao kwa kweli mwingine umetokea kwa mifano halisi, basi uangaliwe na tuwaombe wenzetu wa Uhamiaji wayaone, waanzishe vita vya kupambana na udhaifu ndani ya mfumo wao. Jeshi lisilo na nidhamu na uaminifu ni jeshi la hatari. Kwa hiyo, mimi nashauri hilo.

Lingine, kuna suala lililotamkwa la ajira kwa nasaba, inawezekana lakini ukweli uliopo ni ule ule utaratibu mzuri tu wa kuchekecha na kujenga ajira zinazokubalika.

Mheshimiwa Spika, mimi sioni kubwa la kuzungumzia, niipongeze tu Serikali kwa kuleta Muswada huu, japo umechelewa sasa usichelewa katika kuwekewa sahihi. Utumike mara moja kwa sababu muundo ulikwishakubalika tangu 2010 na tuweze kuhakikisha kwamba, Idara hii inapewa haki zote na inafanya kazi kama Majeshi mengine yanavyoheshimika. Tuwasaidie wapate nyenzo za kazi na wafanye kazi vizuri. *(Makofi)*

Baada ya kusema hivyo, naunga mkono hoja na ninaipongeza sana Serikali kwa kuchukua maamuzi sahihi. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Dkt. Lucy Nkya!

**MHE. DKT. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Niipongeze Wizara kwa kuleta Muswada huu, kwa sababu Uhamiaji ilikuwa ni kama tunavyozungumzia popo, huwajui kwamba hawa ni raia wenzetu wala ni Jeshi linalotambulika. Maadam sasa wametambulika kama Jeshi, ningeshauri huo utambuzi wao uendane na nidhamu ya kuendelea kuwapa heshima zaidi katika jamii yetu.

Mheshimiwa Spika, sitazungumza mengi ila ninachotaka kusema ni kwamba, maadam wametambulika hivyo sasa, Serikali iwawezeshe kuwa na mtandao ambao utaweza kuwapa taarifa za wahamiaji haramu kutoka kwenye jamii kama yalivyo Majeshi mengine yanavyopata taarifa ya uhalifu na mambo mengine katika jamii.

Mheshimiwa Spika, nitoe mfano; Jimbo langu liko ndani ndani huko Morogoro, lakini tumekuja kushtukia kuna wahamiaji wengi kutoka Burundi, wengine kutoka Congo, lakini wakifika kule wanadanganya kuwa wanatoka Kigoma. Mwananchi wa kawaida hajui kwamba kuna tatizo, ameona huyu amesema ametoka Kigoma, basi mwache aendelee kuishi. Jinsi muda unavyokwenda, unaona kidogo kidogo wanazidi kuingia msituni, wanazidi kuongezeka, lakini hawataki kujishughulisha kwenye mambo ambayo yatawafanya wajulikane kwamba wao siyo Watanzania.

Sasa ninachotaka kusema ni kwamba, tatizo nafikiri Jeshi hili pia halina wafanyakazi wa kutosha, nguvukazi watu; tunaomba waongezewe waweze kupata rasilimali watu wa kutosha. Kwa mfano, ukienda Morogoro unawahesabu, sasa watafanyaje kazi pale Morogoro za kuandika *passport*, kufuatilia vibali na mambo mengine na kuja kujua kuna mhamiaji haramu ambaye amekwenda Mahenge au amekwenda Kisaki au amekwenda kujificha katika Pori la Selous?

Mheshimiwa Spika, ninaomba Serikali iangalie namna ambavyo wanaweza wakawaongezea nguvu kazi ili waweze kufanya kazi yao vizuri na kuhakikisha hatupati watu ambao watakuja kutuletea matatizo ya kiusalama.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni kwamba, inakuwa ni ajabu kuona kuna Watanzania wametoka nje, unakuja kusikia wako huko wanateseka, lakini ni nani anawapa vibali vya kwenda kutumikishwa bila kujulikana? *Passport* za kitanzania wanazo; zinapatikanaje na unakuta wanasafirishwa kwenye kundi kubwa la watu, wanapita kwenye mipaka yetu, wanapitaje?

Mheshimiwa Spika, la mwisho ninalotaka kuuliza ni kwamba, katika nchi yetu sasa hivi ukienda Dar es Salaam na miji mingine mikubwa, tuna wahudumu wengi sana wa majumbani wanaotoka Malawi. Ukiwauliza wanakwambia sisi ni Watanzania. Mwingine anakuonesha hata *passport,* lakini wakikaa wenyewe wanapozungumza unasikia wakitaja vijiji vya kwao. Sasa tunajiuliza; je, katika Jeshi letu la Uhamiaji wana Kitengo cha Uchunguzi kujua katika mitaa yetu kuna watu wangapi?

Hapo ndiyo tunasema watengeneze mfumo wa kushirikiana na kupeleka mtu mmoja kwenye Mabaraza ya Maendeleo ya Kata ambayo tunajua kuna watu kama hao, wazungumze na Wenyeviti wetu wa Vitongoji na Vijiji, ambao watakuwa wanatoa taarifa kwa Jeshi letu, kwa sababu sidhani kama tuna hela za kuweza kuajiri watu wengi. Wenyeviti wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji na Wenyeviti wa Mitaa wakipata elimu vizuri na kuelewa Jeshi hili kazi yake siyo kutoa *passport* tu wala *work permit*, ni Jeshi ambalo linaangalia na kulinda Utanzania wetu na usalama wetu, watatoa ushirikiano wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niipongeze Serikali. Naomba niwapongeze na wao, najua wamesikia, wakiambiwa bado wana doa la rushwa, basi kuanzia sasa kwa sababu hii sheria inawapa mamlaka na heshima kubwa, watunze hiyo heshima yao kuhakikisha wanawahudumia Watanzania bila kuwawekea vikwazo ambavyo vitatoa viashiria vya rushwa.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mchangiaji wetu wa mwisho ni Mheshimiwa Zungu!

**MHE. MUSSA A. ZUNGU:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Nami niliomba nichangie kwa muda mchache tu kwa sababu Muswada huu tulishuughulikia Kamati yetu sisi pamoja na Kamati ya Mheshimiwa Mama Anna. Kwanza, nichukue nafasi hii kuwashukuru Kamati hizi mbili kwa namna zilivyofanya kazi kwa pamoja.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi yanapotokea mambo mazito, Kamati hizi hufanya kazi kwa pamoja. Ninakushukuru wewe vilevile kwa kuliruhusu hilo.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. Natoa pongezi sana kwa Wizara hii, ikiongozwa na Mheshimiwa Chikawe na Naibu wake na Katibu Mkuu.

Natoa pongezi vilevile kwa Vyombo hivi vya *Immigration* ambavyo vinaongozwa na *Commissioner General* Ambokile. Nimeona kwenye Taarifa ya Kambi ya Upinzani, Idara hii imelaumiwa sana kuwa labda ndiyo chanzo cha matatizo ya uhamiaji haramu nchini mwetu; siyo kweli kabisa.

Mheshimiwa Spika, matatizo ya *border control,* hakuna nchi ambayo ina matatizo na ina *technology* kubwa zaidi ya nchi yoyote duniani kama Marekani. Marekani wameweka *fence* kati ya nchi yake na nchi ya Mexico kuzuia wahamiaji ambao wanakwenda kutafuta maisha bora nchini humo. Bado wanashindwa kudhibiti uhamiaji haramu na *technology* waliyokuwa nayo, uwezo wa pesa waliokuwa nao, bado wanashindwa mbinu mbalimbali ambazo zinatumika na hawa wahamiaji.

Mheshimiwa Spika, tunachotakiwa sisi ni kuisaidia hii Idara, kuipatia bajeti ya kutosha na kuipatia vitendea kazi vya kutosha. Tuwasaidie waweze ku-*control* wahamiaji haramu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uhamiaji si uhamiaji haramu tu, kuna bandari haramu ambazo zipo katika maeneo hayo hayo ya Ukanda wa Pwani, ambao wengi wetu tupo na tunayaona na tunayasema humu ndani. Hayo hayaonekani, kwa sababu watu wengi wanapenda kuipiga tu Serikali bila kuwa na sababu maalum.

Mheshimiwa Spika, naomba tuipongeze Idara hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na katika mazingira magumu ambayo wamezungukwa nayo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna hoja ya maduhuli ya *visa.* Pesa hizi zinakusanywa na Idara ya Uhamiaji, lakini mara nyingi zinatumika kuendeshea maeneo mengine, sina haja ya kuyasema hapa. Ningeomba sasa kuwe na utaratibu na nafikiri kwenye bajeti hii tujengee hoja, asilimia kubwa ya maduhuli ya *visa* yabaki kuirudia Idara hii ili iweze sasa kujiendesha na iweze kufanya majukumu yake ya Kitaifa na ya Ulinzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, la mwisho, *I stand to be collected,* lakini ninavyokumbuka katika mjadala wa Katiba, Idara hii ilipendekezwa na Kamati zote iwemo kwenye Katiba ikitambulika kama Chombo cha Ulinzi. Ilipotoka Katiba hiki kipengele kilisahaulika. Sasa ninaomba, Idara ya Uhamiaji haiwezi kuwa Idara hivi hivi kama siyo Chombo cha Ulinzi. Idara hii ndiyo inayofanya kazi pamoja na Jeshi la Ulinzi kuwa na *border control* na kuhakikisha kuwa mipaka yetu na *beacon* za mipaka yetu iko salama.

Mheshimiwa Waziri yuko hapa na AG yuko hapa, naomba watafute sasa njia gani ya kuweza kutazamwa marekebisho, sijui kama marekebisho yanaweza kufanyika lakini itafutwe njia; Chombo hiki kitambulike rasmi kama Chombo cha Ulinzi, kwa sababu wanaingia katika vikao vyote vya ulinzi na wasifahamike jina lolote lingine zaidi ya wao ni Idara na ni sehemu ya Ulinzi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, nilikuomba muda mchache na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa mtoa hoja!

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, naomba awali ya yote, nikushukuru kwa kunipa nafasi ya kutoa ufafanuzi kwa wachangiaji mbalimbali ambao wamechangia kwenye hoja hii.

Mheshimiwa Spika, mchango wa kwanza umetoka kwenye Kamati ya Ulinzi na Usalama *jointly* na Kamati ya Mambo ya Nje. Kuna michango iliyotolewa na Kambi ya Upinzani na vilevile kuna wachangiaji kama watano wamechangia hoja hii.

Mheshimiwa Spika, kwanza, naomba niwashukuru wachangiaji. Kwa kiasi kikubwa michango yao inalenga kuboresha Muswada, lakini pia kuboresha Idara hii ya Uhamiaji ili tuhakikishe inafanya kazi zake kwa ufanisi mkubwa. Naomba niwahakikishie kwamba, michango yao haijapotea, imeingia kwenye masikio yenye kusikia ya Serikali na itafanyiwa kazi wala wasiwe na wasiwasi wowote.

Mheshimiwa Spika, baada ya hayo, naomba sasa niende kwenye hoja ambazo zilitolewa na Kamati. Kwanza, niwashukuru Kamati, wako *very constructive* na wametusaidia sana, siyo tu leo hapa Bungeni, lakini pia katika kufanya uchambuzi wa awali, mazungumzo na wadau na hatimaye kuja na *schedule* ambayo tunayo na tutaiwasilisha wakati utakapotoa ruhusa.

Kamati hii imetusaidia sana na michango yao ina nia ya kuendelea kuboresha Muswada, lakini pia kuboresha utendaji na kuhakikisha Tanzania hii inabaki ya Watanzania na inabaki salama siku zote.

Mheshimiwa Spika, Kamati mbali na maoni ya jumla, imependekeza kubadilisha baadhi ya vifungu. Wamependekeza Kifungu namba 17 kiongezwe kifungu kidogo cha (5), kinachozuia mtoto kuwekwa rumande wakati akisubiri kuondoshwa nchini kwake.

Mheshimiwa Spika, sote ni wazazi na kitakuwa ni kitu cha ajabu sana kusema Wizara hii inaweza ikapinga wazo hili zuri. Kwa hiyo, naomba niwahakikishie Kamati ile kwamba, wazo hili tunalichukua na tutalizingatia moja kwa moja na kulifanyia kazi katika kuboresha Muswada huu. Aidha, Kamati hii ilishauri kwamba, Kifungu cha 21 cha masharti ya kuachiwa kwa muda yaainishwe kwenye sheria. Hili ni wazo la kuboresha na hatuna sababu ya kusema halikubaliki. Tunalipokea wazo hili, tutalichambua kidogo na nina uhakika kwamba, tutalifanyia kazi na tutalichukua kwa ajili ya kuboresha Muswada huu.

Kwenye Taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani, kwanza, niseme kwamba, Kambi ya Upinzani imezungumza sana kwa maneno makali, ambayo kwa kawaida kama unamwambia mtu na unatarajia akuletee tija, unaweza ukamvunja moyo. Nafikiri tufike mahala tutazame mazingira wanayofanyia kazi Idara ya Uhamiaji, lakini pia tuelewe namna wanavyofanya kazi.

Naomba niseme kwamba, tukitegemea wafanyakazi 2000 wa Idara ya Uhamiaji wazuie wahamiaji haramu 6,000, haitawezekana kirahisi. Lazima tujue kwa nini wanashindwa watu 2,000. Kwanza, ni suala la watumishi wenyewe kuwa wachache. Nafasi zinatoka, lakini zinazotoka kwa kiasi kikubwa bado tuko nyuma sana kuweza kuwa na Idara ya Uhamiaji ambayo inafanya kazi mpaka sote turidhike. Kikubwa, tukubali kwamba sisi ndiyo ambao tunawaagiza watufanyie kazi na sisi mbali na kuwapuuza kuona ni watukutu, basi tuwasaidie kwa nyenzo na kuwapa angalau motisha ya lugha nzuri pale ambapo tunahisi hawajafanya vizuri.

Mheshimiwa Spika, suala la kuwapima Idara ya Uhamiaji kwa mafanikio ya wahamiaji haramu tu, itakuwa siyo haki; kwa sababu Idara ya Uhamiaji ina kazi na inafanya shughuli nyingi. Kama alivyosema Mheshimiwa Zungu, lazima tuangalie na tuelewe *international affairs*. Dunia ya sasa hivi ina matatizo makubwa sana ya uhamiaji haramu na mamia ya watu wako tayari wafe. Mediterranean kila siku maboti makubwa wanakufa kwa mamia, wale wanaokwenda Spain na wanaoenda Italy. Wenzetu wanaweka *camera* wanaona kule unakoondokea, lakini

bado watu hawa, kwa sababu tofauti, wako tayari wafe lakini watimize malengo yao. Hata hapa kwetu tumeona mifano tofauti, wamekufa Waethiopia, wamewekwa kwenye makontena mara ngapi. Juzi wengine wamekamatwa na wengine wamekufa kwa sababu ya njaa. Ni watu ambao *they are desperate* na wako tayari kufanya lolote. Lingine ni kwamba, mbinu ambazo zinatumika zinabadilika na kubwa zaidi, sisi wenyewe Watanzania tunashiriki katika hili.

Tunapochukua hatua ya kuwalaumu Idara ya Uhamiaji, tujiulize Watanzania sote kweli tunataka wahamiaji haramu wasije? Mbali ya vijiji ambako wanapitia, lakini hata kwenye *business* tunazofanya, mtu anaingiza pesa kwa kuwaleta wahamiaji haramu. Hatuwezi tukawalaumu watendaji peke yao kama sisi tunajiweka nyuma na tunashiriki katika uhalifu kwa namna moja au nyingine.

Kwa hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wabunge na Wananchi wote wa Tanzania kwamba, hebu tuamue kuwasaidia Idara ya Uhamiaji tuone. Tatizo la uhamiaji haramu ni kubwa kama nilivyosema, lakini naamini tunaweza kulipunguza kwa kiasi kikubwa. Sisi ndiyo ambao tunawakaribisha wanapokuja siku ya kwanza wakiwa hawajui mahali na tuziache hizi tabia ili tuweze kupata ulinzi unaoweza kutusaidia.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani mbali na kuwashutumu vibaya kama nilivyosema, lakini mwishoni walitoa *constructive ideas,* wakasema tufikirie kubadilisha vifungu hasa vya uteuzi.

Pia kuna Wajumbe mmoja mmoja kama Mheshimiwa Shekifu na Mheshimiwa Mbassa, walizungumzia suala la uteuzi. Naomba niseme kwamba, marekebisho tunayoyafanya ni kuitoa Idara ya Uhamiaji kwenye uraia kuiweka Jeshini na kuifanya iwe Kikosi Maalum cha Jeshi. Kwa sababu hiyo pamoja na sababu nyingine za kiutumishi, basi sisi tunahisi kwamba uteuzi wa Rais uendelee, kwa sababu hili ni Jeshi na Amiri Jeshi ndiye Rais na ndiyo yeye ambaye ataweza kuamini nani amuweke katika maeneo hayo ya Jeshi. Kama *Bill* hii ilivyosema kwenye mapendekezo ni kwamba, kwenye vyeo ambavyo ni vya kiutendaji moja kwa moja, basi shughuli hizo zinapelekwa kwenye Tume ya Polisi na Magereza ikijumuisha na Uhamiaji. Vilevile kuna watu wa chini ambao Kamishna Mkuu mwenyewe anaweza akawateua.

Kwa hiyo, hoja hii naisikia lakini nawashawishi tukubaliane kwamba, kwa sababu Uhamiaji ni Kikosi cha Jeshi na ndiyo marekebisho tunayofanya, uteuzi uendelee kufanywa na Amiri Jeshi Mkuu.

Walisema pia Kifungu cha 12 kinawapa mamlaka makubwa kufanya doria na upelelezi na wakashauri pengine yangefanywa na Jeshi la Polisi.

Kwenye nchi zote, labda nitoe historia; hapa Tanzania mara baada ya Uhuru na hata kipindi kirefu kilichopita baadaye, Idara ya Uhamiaji ilikuwa Kitengo kidogo sana cha Jeshi la Polisi, lakini wakati huo shughuli za Uhamiaji hazikuwa katika hali hii. Kwa kweli itashangaza sana leo tukizi-*combine* kazi za Uhamiaji na za Polisi tukaridhika kwamba sasa tunaweza tukafanya *patrol* ya Kipolisi ikamaliza matatizo ya kiuhamiaji. Niwaambie kwamba, hizi ni shughuli tofauti na ni lazima tuzifanye kwa weledi unaotakiwa kwa kila kazi.

Kwenye mapendekezo haya pamoja na kuwa Wanadiplomasia ambao wapo kwenye Balozi wangeweza kufanya kazi za utoaji wa *Visa* na *Passport,* lakini pia tunahisi Idara ya Uhamiaji watumishi wake watakapokuwa wanatosha, waende kila *mission* ya nchi yetu ili kuhakikisha kwamba, kazi ya uhamiaji inafanywa kwa weledi kama nyingine.

Katika hili naweza kusema tukubaliane tu kwamba, Uhamiaji na Polisi na hata Jeshi kama alivyoshauri Mheshimiwa Zungu, wanaweza wakashirikiana katika *patrol* au wakashirikiana katika *operations* ambazo zina malengo yanayofanana kiuhamiaji au Kipolisi. Kusema kwamba, Uhamiaji iachane na kazi ya kupeleleza, kazi ya kufuatilia, kazi ya kufanya *patrol,* nafikiri hili tukubaliane kwamba, linaweza likadhoofisha kuliko kuimarisha shughuli zetu.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 17 ndiyo hiki ambacho nimekizungumzia.

Wanashauri Kifungu cha 17(3) kinampa Afisa Uhamiaji wa cheo kuanzia *Superintendent* kuweza kuamuru mtu yeyote kuwekwa kizuizini kabla ya kuondolewa nchini.

Mheshimiwa Spika, Kifungu hiki kimewekwa hivyo ili kurahisisha utekelezaji wa sheria hii. Pale inapolazimika kupelekwa Mahakamani, basi tunawapa Idara ya Uhamiaji uwezo wa kuchukua *statements* ili wale ambao watawatilia shaka au wataona wamevunja sheria, wawakamate na wawapeleke Mahakamani kwa mujibu wa sheria za nchi.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa niende kwenye michango ya mchangiaji mmoja mmoja.

Mheshimiwa Leticia Nyerere, ameelezea hasa mazingira ya kazi za kiuhamiaji. Namshukuru amelisema hili vizuri na ninaamini umewatia moyo Maafisa wetu kukabiliana na changamoto ambazo zinawakabili. Kama ulivyosema, sheria wakati mwingine zinaweza kuwa nzuri lakini je, wana vitendea kazi vya kutosha au wao wenyewe wanatosha kuzisimamia sheria; hilo ni jambo muhimu ambalo nashukuru ameliona na ametufahamisha anachokijua.

Mheshimiwa Dkt. Antony Mbassa, kwa bahati mbaya sana amesema Idara hii ni tatizo. Siwezi kumwambia afute kauli hiyo, lakini namwambia Idara hii ni *saviour* ya Watanzania.

Idara ina changamoto nyingi, lakini bila ya watu hawa ambao wanafanya kazi hii, usalama wetu ni mdogo, umiliki wa haki zetu na rasilimali zetu ni mdogo. Mheshimiwa Mbassa unatoka kwenye maeneo ya kona, maeneo ya mwingiliano kama nilivyosema juzi na huko ndiko ambako tunahitaji tufanye kazi na tupate watu ambao watatusaidia kutupa taarifa ambazo zitasaidia kuilinda nchi hii. Kauli ya kusema uhamiaji ni tatizo, nafikiri ingefanywa ikawa nyepesi ili tushirikiane nao katika kutatua changamoto ambazo zipo katika maeneo fulani ya nchi zetu.

Umezungumzia pia kuhusu vibali vya muda mfupi. Vibali vya muda mfupi ni makubaliano wakati mwingine katika nchi zetu za Jumuiya ya Afrika Mashariki. Vipo vibali ambavyo Watanzania, Wakenya na Warwanda tunakubaliana kwamba kwa wakati mwingine tunaweza tukafanya vitu vya maana vikasaidia kuinua uchumi wa nchi zetu, lakini pia kujenga mshikamano wa Kiafrika Mashariki. Nina hakika kwamba, wapo watu ambao wanaingia kwa utaratibu wa namna hiyo na pale ambapo tutaona vibali hivyo vinatuletea matatizo ni vema tuambizane kuliko kufika mahali tukavisema kwenye *podium,* ambapo vinaletwa kama lawama *rather than constructive ideas* ambapo tungechangia sote tukajenga nchi.

Kuhusu uteuzi wa Makamishna nimelizungumzia. Suala la wahamiaji haramu narudia kusema kwamba ni kubwa na kama hatukushikamana na kushirikiana, tutaendelea kunyoosheana vidole. Tukiamua tu kwamba hatuwataki, mimi nina hakika hawawezi kuja. Wanakuja kwa magari ya Tanzania, wana marubani Watanzania na wanaingizwa kwenye nyumba za Watanzania. Watanzania tukiamua hili tutaliweza na ninawaomba kupitia Bunge hili Tukufu, hebu tushirikiane tuone kiasi gani tunaweza kupunguza kama hatukulimaliza tatizo. *(Makofi)*

Tukumbuke wahamiaji haramu ambao wanakuja sasa hivi wengi wanatoka Ethiopia kwa mfano, wanapita wapi na wapi mpaka wafike Tanzania? Kuna nchi kama Kenya, hili ni jambo ambalo nchi moja kama sisi hatuwezi kulimaliza ingawa tunaweza kulipunguza.

Chini ya Jumuiya ya Afrika Mashariki naelewa, lakini pia kwenye utaratibu mwingine wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini ya *SADC,* kuna makubaliano fulani ambayo baadaye tukiyatekeleza yanaweza yakatusaidia kwa pamoja. Sisi peke yetu lazima tuamue kwelikweli na tuache kazi nyingine tuifanye kazi hii.

Mheshimiwa Shekifu, amesema watumishi hawatambuliwi; ni kweli toka mwaka 2007 watumishi wa Idara ya Uhamiaji walitolewa kwenye utaratibu wa Utumishi wa Umma. Kipindi chote hicho mambo ambayo yanatendeka Idarani kwa kweli siyo ya kisheria.

Tuungane na wafanyakazi hawa, lakini pia tuungane na Wizara na Serikali kuhakikisha tunaweka *status* ya kisheria ambayo itawasaidia wafanyakazi na pia itasaidia ulinzi na nchi kusonga mbele baada ya kuhakikisha hawa wanapata mafao yao, lakini pia tunawapa moyo na vitendeakazi katika kufanya kazi kubwa tuliyowapa.

Mheshimiwa Shekifu pia amezungumzia kuhusu uteuzi, ambapo nafikiri anakubaliana nami kwamba hili ni eneo la kijeshi na siyo vizuri tukalifanya ni eneo la kawaida. Ni vema tukubaliane kwamba, Rais afanye uteuzi wa watu wakubwa wa juu halafu vyombo vingine vifanyie kazi jambo hili.

Jambo lingine ambalo amelizungumzia ni vitendea kazi, ambalo pia amelizungumzia Mheshimiwa Lucy Nkya. Ninakubaliana nanyi mia kwa mia kwamba, vitendea kazi walivyonavyo Idara ya Uhamiaji havitoshi pamoja na uchache wao na tushirikiane; kuna utaratibu wa *retention* ambao tuliuanzisha kwa nia nzuri na walianza ku-*retain* asilimia 69, ikaja asilimia 61 ikaonekana kubwa na sasa tupo kwenye asilimia 45.

Sisi sote tunataka mafanikio ya Idara ya Uhamaji wawe na vitendea kazi, wapate bajeti ambayo itawafikisha kwenye maeneo ambayo tunayazungumzia, kwenye wahamiaji haramu. Tushirikiane, Bunge hili ndiyo linapanga bajeti na linaisimamia Serikali. Tufike mahali tuhakikishe tunawapa bajeti inayostahili kwa kazi ambayo tunawapa ili tufurahi kwamba tunalowatuma wanalifanya na turidhike na kazi yao.

Nimezungumzia kuhusu watendaji wachache, ni suala hilohilo la kiuimarishaji. *In fact,* watenda kazi ambao wapo kwenye Idara ya Uhamiaji leo ni robo ya watendaji ambao tunawataka. Tuna kazi kubwa ya kuwaongeza ili tuhakikishe sasa tunaweza tukakaa kitako tukawalaumu. Kabla ya hapo, nafikiri tuwaunge mkono, tuwape moyo na watatuonyesha kwamba wana uwezo wa kufanya kazi.

Mwisho, Mheshimiwa Zungu aliendelea kuisaidia Serikali kusema kwamba matatizo siyo uhamiaji. Ameeleza mifano ya uhamiaji haramu ambayo inafanyika kwenye nchi zenye uwezo, nchi ambazo zinatoa bajeti kubwa katika Idara zao za Uhamiaji na bado wanalalamikia masuala haya.

Nimezungumza sana masuala ya Lampedusa na masuala ya Mediterranean huko na watu wanaotoka Libya, ni tatizo ambalo hata Umoja wa Mataifa umekaa kitako kusema tulifanye nini. Umoja wa Mataifa wanasema hawana fedha za kutosha kuliondoa hili tatizo. Sasa tushirikiane ili kuona kazi hii tunaifanya kwa masilahi ya nchi yetu.

Mwisho, kulikuwa na pendekezo la kushauri kwamba, Idara ya Uhamiaji tufikirie kufanya kazi pamoja na Jeshi. Idara ya Uhamiaji kwa baadhi ya wakati huwa inafanya kazi na Jeshi lakini pia na Polisi. Ushirikiano huu tutaendelea kuudumisha na tuone kwenye kazi ngumu wanashirikiana vipi ili kuhakikisha nchi yetu inabaki salama.

Mheshimiwa Spika, narudia kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kutoa maelezo. Nawashukuru Wajumbe wote wa Kamati kama nilivyosema mwanzo, Waheshimiwa Wawakilishi wa Kambi Rasmi ya Upinzani, kwa maoni na mazingatio ambayo walitaka tuyafanye.

Nawashukuru pia Wabunge mmoja mmoja ambao wameshiriki na wengine ambao tayari wamepata moyo kushirikiana na Wizara na kuu-*support* Muswada huu ili twende mbele halafu tuangalie.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unatengeneza masuala ya kiutumishi tu katika Idara ya Uhamiaji, bado tuna kazi kubwa tunaendelea kuifanya ya kurekebisha Sera na hapo ndipo tutakuja na sheria kubwa ambayo itatu-*set* kama *road map* ya kuhakikisha Idara ya Uhamiaji tunaitoa hapa ilipo na tunaipeleka kwenye eneo lingine.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Pili)*

**SPIKA:** Hoja hiyo imeungwa mkono. Waheshimiwa Wabunge, mtakumbuka kwamba, tuna Miswada miwili ambayo haijafikia uamuzi. Kwa hiyo, katika Kamati ya Bunge Zima tutaanza na Muswada wa kwanza, tutaupitia kifungu kwa kifungu tutauamua halafu tutaendelea na Muswada huu.

Katibu, hatua inayofuata!

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Silaha wa Mwaka 2014**
***(The Firearms and Ammunition Control Bill, 2014)***

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MWENYEKITI:** Najua tu unataka kuleta fujo, hebu simama useme. Sema tu haya!

**MBUNGE FULANI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama chini ya Kanuni ya 68, kuomba mwongozo wako kukisaidia Kiti chako na ninaenda chini ya Ibara ya 94 ya Katiba yetu ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Ibara ya 77(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge.

Ibara ya 77(2) inasema: "Mbunge yeyote atakayehudhuria anaweza kumjulisha Spika kwamba, Wabunge waliopo ni pungufu ya akidi inayohitajika kwa ajili ya shughuli inayoendelea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wabunge waliopo katika Bunge lako hawazidi 100 na Wabunge wote ni 353, nusu kwa mujibu wa sheria ni 176. Kama tuna hofu kidogo, naomba Wajumbe wahesabiwe. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Umemaliza?

**MHE. RASHID ALI ABDALLAH:** Ndiyo.

**MWENYEKITI:** Katika dunia kuna tabia ya kuchelewesha kazi. Kwa hiyo, tunaendelea, Katibu! *(Makofi/Kicheko)*

***Muswada wa Sheria ya Kudhibiti Silaha wa Mwaka 2014***
***(The Firearms and Ammunition Control Bill, 2014)***

Jina refu la Muswada

*(Jina Refu la Muswada lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 1
Ibara ya 2

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 3
Ibara ya 4
Ibara ya 5
Ibara ya 6
Ibara ya 7
Ibara ya 8
Ibara ya 9
Ibara ya 10
Ibara ya 11
Ibara ya 12
Ibara ya 13

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 14
Ibara ya 15

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

*Ibara ya 16*

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 17

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 17(1)(a) kinasema:-

*"Kwa kuzingatia vifungu vya 10 na 11, Msajili anaweza kutoa kibali cha kumiliki silaha kwa mtu yeyote kwa-*

*(a) Kipindi ambacho Msajili ataamua; na*
*(b) Kuzingatia masharti ambayo yanaweza kuainishwa na kuwekwa na Msajili."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunapendekeza kufuta maneno "Kipindi ambacho Msajili ataamua" na badala yake kuweka maneno "Kipindi ambacho hakitapungua miaka mitano ama hakitazidi miaka kumi ambapo baada ya kipindi hicho kibali kinaweza kuombwa tena."

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiacha maana hii kama ilivyo maana yake ni kwamba, utakuwa umempa *room* kubwa huyu Msajili anayetajwa hapa kuwa na maamuzi ya kufanya anavyotaka. Kwa sababu ni Sheria ya Umiliki wa Silaha tungependekeza kwamba maneno haya yatokee kama ambavyo tumeshauri.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua wasiwasi wa Mheshimiwa Lema, lakini kifungu hiki kinahusu kibali cha kumiliki kwa muda. Sasa kibali cha kumiliki kwa muda kikiwekewa muda usiopungua miaka mitano na kuendelea, sasa unakuwa ni umiliki wa kudumu. Kwa hiyo, inaondoa hasa msingi wa kwamba hiki ni kibali cha muda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba Ibara hii ibaki jinsi ilivyo kwenye Muswada.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

**MWENYEKITI:** Ahsante.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 18
Ibara ya 19

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 20

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 21
Ibara ya 22
Ibara ya 23
Ibara ya 24
Ibara ya 25

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 26

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu cha 26(2), marekebisho ambayo tunataka yachukuliwe ni pale inaposema:-

*(a) Pale ambapo uchunguzi chini ya kifungu kidogo cha (1) umekamilika na Msajili ameridhika kuwa kuna sababu za msingi za kuamini kuwa mtu hana sifa za kumiliki silaha, atatoa notisi kwa maandishi itakayowasilishwa kwa mtu huyo akimtaka kufika mbele yake katika*

*muda na sehemu iliyotajwa katika notisi hiyo ili kuonesha ni kwa sababu gani asitangazwe kuwa hana sifa ya kumiliki silaha; na*

*(b) Pale ambapo mtu ambaye kwake notisi imetolewa katika kifungu kidogo cha 2(a) anashindwa kuhudhuria bila sababu za msingi katika muda na sehemu iliyotajwa katika notisi atamtangaza kuwa hana sifa za kumiliki silaha."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hiki sisi tunapendekeza kiandikwe kama ifuatavyo:-

"*kwamba atatoa notisi ya maandishi itakayowasilishwa kwa mtu huyo ikimtaka kufika mbele ya Mkuu wa Polisi wa Mkoa husika ndani ya siku kumi na nne tangu tarehe ya kutolewa kwa notisi hiyo kwa ajili ya kuwasilisha utetezi wake."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni kwa sababu kwenye kifungu hiki katika Muswada unaoletwa na Serikali hawajaweka *time frame* ya huyu mtu kuitwa na kuja kusimama mbele ya Msajili. Kwa hiyo, inatia mashaka kwamba anaweza akaitwa leo na akaambiwa kwamba, anatakiwa asimame mbele ya Msajili kesho. Kifungu hiki kinasema akishindwa maana yake ni kwamba atakuwa amefutiwa usajili wa kumiliki silaha. Kwa hiyo, inatoa *room* ya uonevu hasa pale ambapo mamlaka husika zitakuwa zinapata watu ambao kwa kweli hawana nia njema.

**MWENYEKITI:** Ahsante. Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, natambua hofu aliyonayo Mheshimiwa Lema, lakini haya siyo maudhui ya msingi wa kifungu hiki. Analeta mapendekezo kwamba iwe kwa Mkuu wa Polisi tu badala ya Msajili lakini angeangalia sheria vizuri kifungu cha 8 ndicho kinachomtambua Msajili na kutaja kazi zake. Kifungu kidogo cha 3 kinampa mamlaka ya kukasimisha mamlaka yake haya kwa *authorized officer* na *authorized officer* ametajwa katika kifungu cha 3 ni *any police officer*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama wasiwasi wake ilikuwa ni kwamba labda Msajili hatakuwa anaonekana kila sehemu pale, hiyo imekuwa *taken care off*. Hii ya muda, taratibu zetu zinataka apewe muda unaomtosha yaani *reasonable time,* hata kama haikuandikwa hapa lakini inatakiwa iwe ni muda ambao unamtosha na vinginevyo atakuwa na haki ya kwenda Mahakamani kupinga kama inaonekana anaonewa hata kama hiyo haikutajwa kwenye Muswada kwa sababu ni haki yake ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba, masharti ya Muswada huu kama yalivyo kwenye Ibara hii ya 26(2) yabaki jinsi yalivyo.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ni vyema sana sheria ikaweka hii *time frame*. Anachokisema Mwanasheria Mkuu wa Serikali ni kwamba huyu mtu hata kama atakuwa ameonewa katika huo muda anaweza aka–*appeal* akaenda Mahakamani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini hizi mamlaka zetu zinazo-*deal* na haya mambo siyo kila mara zinapata watu waaminifu. Kwa hiyo, kama anasema kwamba, huyu mtu atapewa *a reasonable time*, kwa nini basi sheria angalau isi-*state* hiyo *reasonable time* ni kuanzia muda gani. Kuna ugumu sasa wa kusema angalau hiyo *reasonable time* itakuwa ni *fourteen days.* Kama Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali anaamini kwamba hawa watu watapewa muda wa kutosha kama ambavyo ame-*explain* hapa, sasa kwa nini hii sheria isi-*state* kwamba

*a reasonable time either* itakuwa ni *fourteen days* ama *twenty one* days kuliko iachwe ikawa wazi kama inavyoonekana sasa ambapo inaleta mashaka makubwa. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mwanasheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja yake ninaona umuhimu wake lakini haya masharti ya muda yanaweza yakawekwa kwenye kanuni ambazo zitatungwa na Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana ya kusimamia sheria hii.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 27

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 28

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa naKamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 29

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nimeleta marekebisho katika kifungu hicho, kwa kuwa kifungu hicho kinaeleza kwamba silaha au risasi zote zitahifadhiwa katika maghala ya umma na hazitaweza kutoka mpaka kibali cha Msajili. Kwa mujibu wa sheria hii, Msajili ni mmoja na tunaelewa ukubwa wa nchi hii. Maghala haya yanaweza yakawepo katika maeneo mbalimbali na ni ukweli kwamba wakati mwingine inaweza ikatokea dharura yoyote katika ghala lolote ambalo silaha au risasi zimehifadhiwa. Majanga hayo yanaweza kuwa ya moto, mafuriko au lingine lolote lile ambalo linaweza likatokea kwa namna moja ama nyingine na silaha hizi na risasi hazitaweza kutolewa bila kibali cha Msajili na Msajili ni mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, napendekeza kwamba pamoja na Msajili kutoa kibali lakini pia Mkuu wa Polisi wa Mkoa naye kwa idhini ya Msajili awe anaweza kutoa kibali pale ambapo inatokea dharura yoyote. Kwa hiyo, nafanya marekebisho kwa kutoa neno "Msajili" na kifungu sasa kisomeke:-

*"Silaha zilizohifadhiwa katika ghala la umma, kituo cha Polisi au sehemu nyingine yoyote inayoelezwa na Msajili, hazitatolewa ndani humo isipokuwa kwa kibali kilichosainiwa na Mkuu wa Polisi zilikohifadhiwa silaha hizo kwa niaba ya Msajili"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umuhimu wa hoja anayoisema Mheshimiwa Paresso lakini sheria hii jinsi ilivyoandikwa, Msajili kwanza anatajwa kwenye Ibara ya 8 ya Muswada huu halafu Ibara ndogo ya (3) inampa mamlaka ya kukasimisha mamlaka yake hayo kwa *authorized officer* ambaye ametajwa katika Ibara ya 3. Tafsiri ya huyu *authorized officer* inasomeka hivi:-

"*authorized officer means a police officer or any other officer designated as such by the Registrar to assist in the implementation of this Act"*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, katika mazingira kama haya, busara tu itamtaka kwa vyovyote vile iwavyo huyu Msajili ayakasimishe madaraka yake kwenye Mkoa. Kwa sababu kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge, hawezi kuwepo kila sehemu, ni lazima ata-*delegate* na kwenye ngazi ya Mkoa itakuwa ni kwa *Regional Police Commander* au kwa maafisa wengine wa Wilaya mpaka kwenye *office commanding stations* ili kuleta ufanisi katika utekelezaji wa sheria hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, naomba kushauri kwamba ibara hii nayo ibaki kwa jinsi ilivyo.

**MWEYEKITI:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakubaliana na hoja hiyo.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 30

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 31

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Kichwa cha Habari – Sehemu ya IV

*(Kichwa cha Habari cha Sehemu ya IV ya Muswada kilipitishwa pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 32
Ibara ya 33
Ibara ya 34
Ibara ya 35
Ibara ya 36
Ibara ya 37
Ibara ya 38
Ibara ya 39
Ibara ya 40
Ibara ya 41
Ibara ya 42
Ibara ya 43
Ibara ya 44
Ibara ya 45

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 46

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 47
Ibara ya 48

Ibara ya 49
Ibara ya 50
Ibara ya 51
Ibara ya 52
Ibara ya 53

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 54

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifungu hiki cha 54 kinasema:-

*"Hakuna mashtaka ama hatua zozote za kisheria zitakazochukuliwa dhidi ya Msajili au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa anayetekeleza majukumu yoyote chini ya sheria hii kwa lolote atakalolitenda kwa nia njema."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sisi tumependekeza kwamba kifungu hiki cha 54 kiandikwe upya kama ifuatavyo:-

*"Msajili au mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake chini ya sharia hii, atazingatia kanuni, taratibu na sheria za nchi wakati wa kutekeleza majukumu yake."*

Mheshimiwa Mwenyekiti, msingi wa kupendekeza hivi ni kwamba kwenye kifungu hiki Muswada ulioletwa na Serikali utamruhusu Askari yeyote kutekeleza majukumu yoyote chini ya sheria hii kwa lolote atakalolitenda kwa nia njema. Ukiangalia kifungu hiki ni kinga kwa mtu anayezuia silaha. Hii ikiachwa hivi inaweza ikaleta hofu kubwa sana kwa sababu nia njema ya kwako siyo nia njema kwangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tuna-*propose* kwamba Msajili ama mtu mwingine yeyote aliyeidhinishwa kutekeleza majukumu yake chini ya sheria hii azingatie kanuni, taratibu na sheria za nchi ili kuepuka mpango wa watu wabaya watakaojifanya wana nia njema kuumiza watu wengine.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naona umuhimu wa wasiwasi wa Mheshimiwa Lema, isipokuwa kifungu hiki kwa jinsi kilivyo hakizuii Afisa yeyote anayetekeleza majukumu yake kwa mujibu wa sheria hii kuchukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na kufikishwa Mahakamani. Wale ambao wanakingwa na sheria hii ni wale wanaotekeleza wajibu wao kwa nia njema. Sasa nia njema haiwezi ikaamuliwa tu na mtu mwingine yeyote, ina maana ni Mahakamani. Kwa hiyo, huyu mtu anashtakiwa Mahakamani halafu baadaye Mahakama inaangalia hivi kweli wewe ulikuwa unatekeleza shughuli zako kwa nia njema au hapana! Vinginevyo ukiondoa hii kinga hakuna mtu atakayefanya kazi kwenye Jeshi lile la Polisi. Kwa hiyo, ni lazima ibaki tu pale. Sitaki kuwa mwanasiasa lakini naona siku hizi vituo vya Polisi vinavamiwa na silaha zinachukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, mabadiliko haya hatuhitaji kuyaweka hapa kwa sababu kwa mujibu wa Ibara ya 29, kwanza kabla sijaenda kwenye Ibara, sheria inapotungwa *essence* yake ni kwamba itekelezwe yaani unatunga sheria ili kulazimisha utekelezaji wa hiyo sheria yenyewe, *thus why you come up with the law.*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa ukiacha hii, Ibara ya 26 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 (Toleo la mwaka 2005) inasema hivi:-

*"Kila mtu ana wajibu wa kufuata na kuitii Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kama una masharti kama haya huhitaji kuweka hapa tena kwamba kila mtu anastahili kuzingatia na sheria hii.

Mhshimiwa Mwenyekiti, halafu inatoa fursa katika Ibara ndogo ya (2) kwa kusema:-

"*Kila mtu ana haki, kwa kufuata utaratibu uliowekwa na sharia, kuchukua hatua za kisheria kuhakikisha hifadhi ya Katiba na sheria za nchi hii*".

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hizo mbili, naomba kushauri kwamba, Ibara ya 54 jinsi ilivyo kwenye Muswada huu ibaki jinsi ilivyo. *(Makofi)*

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Mwanasheria Mkuu wa Serikali anataka kulishawishi Bunge kwamba huyu mtu anayetekeleza haya majukumu kwa nia njema *incase* majukumu yale ikaja kuthibitika kwamba hayakuwa kwa nia njema atafikishwa Mahakamani. Hata hivyo, kifungu hiki kinasema kuwa hakuna mashtaka ama hatua zozote za kisheria zitakazochukuliwa dhidi ya Msajili au mwingine yeyote aliyeidhinishwa anayetekeleza majukumu yoyote au anayetekeleza majukumu yoyote chini ya sheria hii kwa lolote atakalolitenda kwa nia njema.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nia njema ni kitu gani? Usipoweka kikomo cha utekelezaji wa majukumu haya *especially* pale ambapo Askari anataka kum-*disarm* mtu silaha, amekutana na wewe barabarani, humjui kama ni Askari yuko *undercovered* anakusimamisha, anataka kuchukua silaha yako na wewe unataka ku-*protect* silaha yako kwa sababu hujui kama ni Askari, nia njema yake ikamtuma akupige risasi, huyu mtu kwa kifungu hiki kinasema hakuna mashtaka au hatua zozote za kisheria zitakazochukuliwa dhidi yake. Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba pamoja na hii nia njema, hii nia njema iwekewe mipaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimesema kwenye hotuba yangu leo Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwamba Mungu pamoja na upendo wake na ukarimu wake pamoja na rehema zake lakini Mungu ameweka Jehanamu, ana mipaka pia ya utendaji wake. Mimi nashauri hii nia njema iwekewe mipaka na kwamba utekelezaji wa majukumu yote ya kimsingi kama haya yafanyike katika utaratibu wa sheria na kanuni ili hiyo nia njema pia iwe *regulated* lakini ikiachwa kwa upana hivi kwa kweli itakuwa ni hatari sana.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Lema mnasema kitu kimoja kwamba hata huyo wa nia njema siyo kwamba hatafikishwa Mahakamani, mpaka Mahakama i-*prove* kwamba nia yake ilikuwa njema vinginevyo ana matatizo. Kwa hiyo, unaposema haya ni hayahaya yaliyoko, *what you are saying* siyo kitu kipya kipo, nia njema yenyewe unapelekwa Mahakama ndiyo wakagundue kuwa ulikuwa una nia njema. Hivyo hivyo aliyevunja sheria unavyopendekeza wewe, itakwenda Mahakamani na kusema kuwa umevunja sheria hizohizo. Kwa hiyo, tunasema kitu kimoja na lugha ni moja, hii nyingine ni ya kisheria na hii nyingine ni ile ya kusikia tu, afanye hivi au afanye hivi.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 55

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 56
Ibara ya 57

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 58

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kifucha cha 58(2) kinaelezea suala la ofisi za masijala kuu na usimamizi wa hizo masijala. Kwa mujibu pia wa kifungu cha 4, msimamizi mkuu wa Sheria hii ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha ameachiwa Inspekta Jenerali wa Polisi. Kifungu cha 58(2) kinasema masijala kuu ya silaha itakuwa chini ya usimamizi wa Inspekta wa Jenerali wa Polisi au Afisa mwingine kadri ambavyo Waziri atakavyomteua. Kwa hiyo, napendekeza ili kuweka msingi mzuri wa kifungu cha 4 kwa maana ya msingi mzima wa sheria hii kuwa msimamizi mkuu awe ni Inspekta wa Polisi. Kwa hiyo, napendekeza yale maneno 'au Afisa mwingine kadri ambavyo Waziri atakavyomteua' yaondoke na usimamizi wa masijala hii yabaki kwa Inspekta wa Polisi tu. Ahsante.

**SPIKA:** Mwanasheria Mkuu.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeshindwa kuelewa wasiwasi wa Mheshimiwa Paresso lakini sheria inapotamka na inapoweka mamlaka kwa Waziri, inapomtaja pale kuna sababu ya kumtaja, ni lazima awe na shughuli fulani ya kufanya na hii shughuli ukiangalia sana ni ya kiutawala tu na kwa vyovyote vile Mheshimiwa Waziri hawezi kutekeleza wajibu huu bila kwanza kuwa ameshauriwa na Inspekta Jenerali wa Polisi au na Maafisa wa Jesho la Polisi. Kwa hiyo, naomba kushauri kwamba hii Ibara jinsi ilivyoandikwa haina matatizo ibaki hivihivi jinsi ilivyo kwenye Muswada.

**SPIKA:** Mheshimiwa Paresso.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, labda AG hajanielewa. Ukienda kifungu cha 4, masharti ya jumla ya kiutawala yanasema kwa madhumuni ya usimamizi na utekelezaji wa sheria hii, Inspekta Jenerali wa Polisi atakuwa ni msimamizi wa Kitaifa. Ukirudi kwenye kifungu cha 58 chote na hicho cha (2) kinaeleza ofisi za masijala kuu ya silaha, kinasema masijala kuu ya silaha itakuwa chini ya usimamizi wa Inspekta Jenerali wa Polisi au Afisa mwingine kadri Waziri atakavyomteua kwa ajili ya kuingiza taarifa za vibali na leseni zilizotolewa chini ya sharia hii. Maana yake ni kwamba kifungu hiki kama kinakwenda kumpa mamlaka Waziri ya kumteua mtu mwingine kadri atakavyoona inafaa inakwenda kinyume na msingi wa masharti ya kiutawala katika kifungu cha 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nachopendekeza ni kuondoa haya mamlaka ya Waziri kwamba amteue Afisa mwingine kwa kadri atakavyoona inafaa maana yake anataka kupunguza madaraka ya Inspekta Jenerali wa Polisi yaliyoanishwa katika kifungu cha 4 kwamba ndiye atakuwa ni msimamizi mkuu wa Sheria hii ya Udhibiti wa Silaha. Kwa hiyo, nachopendekeza ni kuondoa yale mamlaka kwamba Waziri atateua mtu mwingine maana yake unapunguza msingi wa Sheria wa *IGP* kuwa msimamizi mkuu wa sheria hii. Kwa hiyo, bado nina msimamo uleule kwamba kifungu hiki kiondolewe.

**SPIKA:** Mwanasheria.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nadhani shida ni matumizi ya neno msimamizi mkuu kwa sababu kwenye *version* ya Kiingereza imeandikwa ni *focal point*, sasa *focal point* maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba kuna mamlaka nyingine juu. Kwa jinsi ilivyo mimi naomba kushauri kwamba Ibara hii ibaki jinsi ilivyo kuna maana yake.

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu, tuelezee hiyo maana yake.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mapema nilisema kwamba Waziri anapopewa mamlaka kwenye sheria kuna maana yake na hizi ni shughuli za *overall supervision* ya *admnistration* za kisera kwenye hilo eneo. Sasa itafikia hatua labda Waziri anaona kwamba hawa tu peke yake hawatoshi ni lazima amteue na mtu mwingine. Kwa hiyo, ikitokea hivyo, ndiyo hiki kifungu kinakuja ku-*cover* hali hiyo, itategemea na masuala ya kisera ambayo mtu wa Majeshi hayajui, mimi ndivyo ninavyoelewa.

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 59
Ibara ya 60

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 61

*(Ibara iliyotajwa hapo juu ilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 62
Ibara ya 63

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 64
Ibara ya 65
Ibara ya 66
Ibara ya 67
Ibara ya 68

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Ibara ya 69
Ibara ya 70
Ibara mpya ya 71

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Ibara ya 72
Ibara ya 73
Ibara ya 74
Ibara ya 75
Ibara ya 76

*(Ibara zilizotajwa hapo juu zilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 1

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 2

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

Jedwali la 3

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila mabadiliko yoyote)*

Jedwali la 4

*(Jedwali lililotajwa hapo juu lilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima pamoja na marekebisho yake)*

*(Bunge lilirudia)*

**Muswada wa Sheria wa Kudhibiti Silaha wa Mwaka 2014**
***(The Firearms and Immunition Control Bill, 2014)***

*(Kusomwa Mara ya Tatu)*

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Spika, baada ya Bunge lako Tukufu kukaa kama Kamati na kupitisha Muswada wa Sheria ya Usimamizi na Udhibiti wa Silaha na Risasi ya mwaka 2014, kifungu kwa kifungu pamoja na marekebisho yake, naliomba sasa Bunge lako Tukufu lipitishe Muswada huu.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA FEDHA:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Muswada wa Sheria ya Serikali Ulisomwa Mara ya Tatu na Kupitishwa na Bunge)*

**KAMATI YA BUNGE ZIMA**

**Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria ya Uhamiaji wa Mwaka 2014**
***(The Immigration (Ammendment) Bill, 2014)***

**MWENYEKITI:** Mheshimiwa Mnyaa.

**MHE. ENG. MOHAMMED HABIB JUMA MNYAA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuhusu hili tunalotaka kuingia hivi sasa kwamba ni jambo la Uhamiaji, ni jambo la Muungano, ni jambo ambalo limetajwa katika Orodha ya Pili ya Katiba. Ikiwa utaniruhusu nisome imesemwa kwamba sheria ambazo mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka upande wa Tanzania Bara na upande wa Tanzania Zanzibar ikiwemo Sura ya 54 ya Sheria ya Uhamiaji kama ilivyo katika Nyongeza ya Pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilitaka mwongozo wako tu, je, utaratibu wa kupitisha suala hili utakuwa ni wa kawaida kama ulivyotupitisha hivi sasa au tutafuata kanuni ya *two third majority?* Naomba mwongozo wako.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, sijui ni kwa nini Mheshimiwa Mnyaa ameleta hoja hii sasa kwa sababu hata Muswada ambao umepitishwa na Bunge hili Tukufu muda mfupi uliopita ungeingia kwenye masharti kama haya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kushauri kama utaniruhusu…

**MWENYEKITI:** Nimekuruhusu hivyo.

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nitoe ufafanuzi wa kutosha ili kusudi Waheshimiwa Wabunge walijue suala hili vizuri.

**MWENYEKITI:** Mwanasheria Mkuu, naomba ukae kwanza, kwa mujibu wa Kanuni ya 28 naongeza muda wangu wa dakika 30 baada ya saa ya kuahirisha Bunge. Mwanasheria Mkuu endelea!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 98(1)(a) na (b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 inaelekeza ifuatavyo, ninanukuu:-
*"Bunge laweza kutunga sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii kwa kufuata Kanuni zifuatazo:-*

*(a) Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii (isipokuwa yale yanayohusika na aya ya (b) ya Ibara hii ndogo) au masharti yoyote ya Sheria yoyote iliyotajwa katika Orodha ya Kwanza katika Nyongeza ya Pili utaungwa mkono kwa kura za Wabunge ambao idadi yao haipungui theluthi mbili ya Wabunge wote.*

*(b)Muswada wa Sheria kwa ajili ya kubadilisha masharti yoyote ya Katiba hii au masharti yoyote ya Sheria yoyote yanayohusika na jambo lolote kati ya mambo yaliyotajwa katika Orodha ya Pili iliyoko kwenye Nyongeza ya Pili iliyoko mwishoni mwa Katiba hii, utapitishwa tu iwapo utaungwa mkono kwa kura theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar.*

*(2) Kwa madhumuni ya ufafanuzi wa masharti ya Ibara ndogo ya (1), kubadilisha masharti ya Katiba hii ama masharti ya Sheria maana yake ifahamike kuwa ni pamoja na kurekebisha au kusahihisha masharti hayo au kufuta na kuweka masharti mengine badala yake au kusisitiza au kubadilisha matumizi ya masharti hayo".*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo ya Muungano yametamkwa katika Ibara ya 4 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kuorodheshwa katika Nyongeza ya Kwanza ya Katiba hiyo. Miongoni mwa mambo hayo ni kodi ya mapato inayolipwa na watu binafsi na masharika, ushuru wa forodha, ushuru wa bidhaa zinazotengenezwa nchini Tanzania unaosimamiwa na Idara ya Forodha, uraia, uhamiaji na kadhalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Miswada ya Sheria ikiwemo ile Sheria iliyotajwa katika Orodha ya Kwanza kwenye Nyongeza ya Pili inapitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. Miongoni mwa sheria hizo ni Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 ambapo ukiangalia ile sheria inatumika pande zote za Muungano, Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995

ambayo ni sheria yote, Sheria ya Kuthibitisha Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1964 ambayo ni sheria yote inatumika kwa pande zote mbili kwa ujumla wake na Sheria ya Kuthibitisha Tanganyika kuwa Jamhuri ya Muungano ya mwaka 1962 kwa kifungu cha (3), (27), (18) na (26).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukichukua hii Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania unaona imetajwa hii Sheria ya Uhamiaji na masharti yake yanapitishwa kwa theluthi mbili ya Wabunge wote ambayo ndiyo tunafanya *amendment* hapa. Sheria ya Uhamiaji ya mwaka 1995, Sheria ya Uraia ya mwaka 1995 na Sheria ya Kuthibitisha Mapatano ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar ya mwaka 1965, zinatumika Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar kwa ujumla wake lakini bado zinapitishwa kwa utaratibu wa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. Sheria ya Kuthibitisha Tanganyika kuwa Jamhuri ya mwaka 1962 ambayo baadhi ya vifungu au Ibara zake kwa maudhui yake inagusa Muungano, bado inapitishwa kwa kuungwa mkono kwa theluthi mbili ya Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, kutokana na mwongozo huu wa Kikatiba pale ambapo sheria za kawaida zinazotumika kwa ujumla wake katika pande zote mbili za Muungano au sehemu tu ya sheria hizo zinatumika katika pande zote za Muungano sheria hizo zitapitishwa Bungeni kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote. Naposema sheria za kawaida ni kama hizi, ni tofauti sasa na Sheria za Mabadiliko ya Katiba ile Miswada nitakuja kuzungumzia huko mbele. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, Muswada kama huu wa *amendment* kwenye hii Sheria ya Uhamiaji ambayo kwa mujibu wa Katiba inapitishwa tu, imetajwa kwenye ile *Schedule* ya Pili, Nyongeza ya Kwanza, kwa theluthi mbili ya Wabunge wote, haihitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Zanzibar na theluthi mbili ya Wabunge kutoka Bara. Hii ni pamoja na Miswada ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu hiyo, Muswada ambao mabadiliko yake yanahitaji kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili za Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(b) yameorodheshwa katika Nyongeza ya Pili, Orodha ya Pili katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Mambo hayo ni kuwapo kwa Jamhuri ya Muungano, kuwapo kwa Ofisi ya Rais wa Jamhuri ya Muungano, Madaraka ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano, kuwapo kwa Bunge la Jamhuri ya Muungano, Madaraka ya Serikali ya Zanzibar, Mahakama Kuu ya Zanzibar, Orodha ya Mambo ya Muungano na idadi ya Wabunge kutoka Zanzibar. Haya ni masuala ya Kikatiba, kama unaleta Muswada wa mabadiliko ya Katiba kubadilisha miongoni mwa haya ndipo utakapohitaji *formula* hii ya *two third* kutoka *either sides of the Union*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, mambo hayo kama yalivyo kwa asili yake ni ya Kikatiba kwa kuwa yametajwa katika Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Muswada wa Sheria ya mabadiliko ya mambo hayo unakuwa ni Muswada wa Sheria ya Mabadiliko ya Katiba. Ndiyo maana mabadiliko ya mambo hayo sharti yaungwe mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. Kwa sababu hiyo, kama Muswada husika ungekuwa ni wa kubadilisha masharti ya Orodha ya Mambo ya Muungano kwa kuongeza, kusisitiza au kufuta baadhi ya mambo katika Orodha ya Mambo ya Muungano, ili Bunge liupitishe ingepaswa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Bara na theluthi mbili ya Wabunge wote kutoka Tanzania Zanzibar. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Muswada huu wa mabadiliko ya Sheria ya Uhamiaji hauhitaji *formula* hii na hii ni sambamba na Miswada mingine iliyopo mbele yetu. Kwa mfano,

Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2014, Muswada wa Takwimu ambao haubadilishi chochote katika Orodha ya Mambo ya Muungano, unaungwa mkono kwa utaratibu huu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia kuenda kupiga kura, ni pale tu ambapo kunakuwa na sababu ya kupiga kura. Kwa mfano, kama ilivyohojiwa jana hapa kwenye ule Muswada wa Ajira, hakukuwa na hata Mheshimiwa Mbunge mmoja aliyesema haungi mkono huo, hulazimiki hata kupiga kura, ule ulikuwa unatumika Bara tu. Kama hapa, kwa mfano hakuna Mbunge aliyesema haungi mkono, hauwezi kwenda kuhesabu, kila ukikaa watu wanaanza kupiga kura muda wenyewe haupo. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufafanuzi huu wa Katiba, natoa ushauri kwamba Muswada huu wa mabadiliko kwenye hii Sheria ya Uhamiaji na Muswada wa Sheria ya Usimamizi wa Kodi ya mwaka 2014, Muswada wa Sheria ya Takwimu, 2014 na mingine ya aina hii na Miswada yote ya Sheria ambazo kwa maudhui yake hazibadilishi masharti ya Katiba kwa mambo yaliyotajwa katika Nyongeza ya Pili ya Orodha ya Pili, kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(b) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inapitishwa kwa kuungwa mkono na theluthi mbili ya Wabunge wote kwa mujibu wa Ibara ya 98(1)(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la msingi linalopaswa kuzingatiwa ni ushirikishaji ipasavyo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar wakati wa mchakato wa utungaji wa sheria zinazotumika katika pande zote mbili za Jamhuri ya Muungano ili kulinda maslahi ya pande zote mbili katika Muungano. Kwa maana hiyo basi, ikiwa Serikali ya Mapinduzi ilishirikishwa ipasavyo katika uandaaji wa Miswada ya Sheria hiyo, inatosha na hapa Bunge likiridhika linaweza kuipitisha kwa kufuata wingi wa kura.

**WABUNGE FULANI:** Aaaaaah!

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:** Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye hili, Serikali hizi mbili, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zinafanya kazi kwa karibu sana. Mimi kwenye suala hili pia nilimshirikisha Ndugu yangu, Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar naye anaukubali kwamba huu ndiyo msimamo wa Kikatiba kuhusu upitishaji wa Miswada ya aina hii na amethibitisha kwa maandishi. Kwa mujibu wa Sheria ya Uendeshaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Zanzibar kama ilivyo kwa Sheria ya Uendeshaji wa Utekelezaji wa Shughuli za Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ushauri wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali ndiyo unakuwa msimamo wa Serikali katika suala hilo wanaloshauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja na kuwasilisha. *(Makofi)*

*(Hapa baadhi ya Waheshimiwa Wabunge walisimama)*

**MWENYEKITI:** Naomba mkae chini mimi nimesimama. Kwa sababu niliombwa mwongozo Bunge linarudia.

*(Bunge lilirudia)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kutokana na mwongozo nilioombwa na kutokana na kwamba nataka kushauriana na wahusika kwa undani zaidi, kwa hiyo, naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. *(Makofi)*

*(Saa 1.47 usiku Bunge liliahirishwa hadi siku ya Ijumaa,*
*Tarehe 20 Machi, 2015, Saa Tatu Asubuhi)*